# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 21 Juni, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Swali la kwanza ni la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga na litaulizwa na Mheshimiwa Venant Daud.

Na. 651

### Kupandisha Hadhi Shule za Sekondari Manonga

**MHE. VENANT D. PROTAS K.n.y. MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi shule za Sekondari Manonga, Seif Gulamali, Simbo na Nkinga kuwa za kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ina jumla ya shule tano za kidato cha tano na sita. Tathmini iliyofanywa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika shule za Sekondari Manonga, Seif Gulamali, Simbo na Nkinga ilibaini kuwa shule hizo zina upungufu wa miundombinu inayohitajika kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita ikiwemo mabweni na bwalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Igunga itatenga bajeti pamoja na kushirikiana na wananchi kukamilisha ujenzi wa miundombinu inayohitajika ikiwa ni pamoja na kuomba kusajiliwa kwa shule hizo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia baada ya kukamilika ili ziweze kupandishwa hadhi na kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant Daud.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu ya Serikali Wananchi wa Jimbo la Manonga wamekuwa wakijitolea miradi mbalimbali na wanafunzi wanaokwenda kusoma katika shule za kidato cha tano na sita katika Jimbo la Manonga wanatoka Tanzania nzima.

Je, Serikali hamuoni haja sasa kwa kuwa mna upungufu wa shule za kidato cha tano na sita mkaziongezea miundombinu shule hizo za Manonga ili wanafunzi waweze kupata elimu nzuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; matatizo yaliyoko katika Jimbo la Manonga ndivyo ilivyo Jimbo la Igalula katika Shule ya Sekondari Tura. Miundombinu ya mabweni iko safi watoto wanasoma vizuri tunapokea wanafunzi kutoka mikoa

mbalimbali, lakini kuna chgangamoto ya bwalo la chakula. Ikifika mwezi wa 11 wakati wa masika watoto wanakosa sehemu ya kupatia chakula. Je, lini Serikali mtapeleka bwalo la chakula kwenye Sekondari ya Tura ambayo ina kidato cha tano na sita sasa hivi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Kuhusiana na swali lake la kwanza naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba jukumu kimsingi la kujenga miundombinu ya shule za *primary* na za sekondari ni jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kazi ya Serikali Kuu ni kuongeza nguvu tu ili kuziunga mkono Halmashauri pale zinapokuwa zimeonyesha jitihada ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nichukue fursa hii kuendelea kusisitiza na kumkumbusha Mkurugenzi lakini na Mbunge wote washirikiane ili Halmashauri iweze kutenga fedha katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu hii inayohitajika inajengwa na shule hizi zinaweza kuombewa kupanda hadhi kuwa shule za kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi Serikali imeelekeza nguvu kubwa sana katika kuimarisha miundombinu ya shule ambazo zimeshapangiwa wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita ambacho katika Jimbo la Manonga Shule ya Ziba na Shule ya Choma zimetengewa na zinapelekewa shilingi milioni 692 kwa ajili ya kujenga mabweni madarasa na vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na bwalo la chakula, naomba niendelee kusisitiza kwamba Halmashauri ziweze kufanya jitihada za kutenga bajeti kutoka kwenye mapato ya ndani ili kuweza kukamilisha miundombinu hii. Pia Serikali Kuu pale kunapokuwa na uhitaji

mkubwa na yenyewe itaendelea kuunga mkono jitihada hizi zinazokuwa tayari zimeanza kufanywa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia utaratibu huo huo, jitihada za Serikali Kuu na jitihada pia za Mamlaka za Serikali za Mitaa tutashirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba bwalo hili la chakula katika shule uliyoitaja Mheshimiwa Mbunge linajengwa ili wanafunzi wetu waweze kupata miundombinu mizuri katika shule hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mlalo tunazo sekondari 31 na sekondari za Mkundi, Mtumbi pamoja na Mtaya zote hizi miundombinu yake inaruhusu uanzishwaji wa madarasa ya kidato cha tano na sita. Je, Serikali iko tyari kuzifanyia kazi shule hizi ili ziweze kuwa na kidato cha tano na sita? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Mbunge amekuwa ni mahiri sana katika kuhakikisha anapambania changamoto za wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali hili. Kama shule hizi alizozitaja za Mkundi, Mtumbi na Mtale zina miundombinu hitajika basi hatua inayofuata ni Mkurugenzi kuweza kupeleka maombi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kuomba kupandishwa hadhi kwa shule hizi kwa kidato cha tano na cha sita. Kwa hiyo naomba nichukue fursa hii kumwelekeza Mkurugenzi aweze kufanya tathmini katika shule hizi ili kuona kama zina miundombinu hitajika aweze kupeleka maombi ya kupandisha hadhi shule hizi ili ziweze kuwa shule za kidato cha tano na cha sita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuwapa wananchi wa Kilimanjaro pole kwa kuondokewa na Katibu Tawala wetu. Nilikuwa nauliza swali, Shule ya Sekondari Ng'uni imekuwa na majengo chakavu sana na wananchi wamejitahidi kuanza ujenzi wa maabara pale shuleni. Je ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya kumalizia majengo haya lakini pia na mabweni ya wanafunzi katika Shule ya Sekondari Ng'uni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yenye tija kabisa kwa ajili ya wananchi wake. Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia miundombinu chakavu na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea na utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la ujenzi wa mabweni. Kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya awali nimesema kwamba Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuendeleza kujenga miundombinu muhimu katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa utaratibu huohuo naomba nichukue nafasi hii kuendelea kusisitiza kwamba Mkurugenzi mshirikiane pamoja ili kuhakikisha kwamba mnatenga fedha katika mapato ya ndani kwa ajili ya kuendeleza miundombinu hii muhimu. Pia, kama nilivyotangulia kusema, Serikali Kuu itaongeza nguvu kwa ajili ya kuhakikisha pale jitihada zinapokuwa tayari zimeanzishwa Serikali iweze kuunga mkono ili kuhakikisha miundombinu hii muhimu inakamilishwa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge toa shaka Serikali itahakikisha ushirikiano na utaratibu huo mabweni haya yanajengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali linalofuata la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mwita.

Na. 652

**Hitaji la Nyumba za Walimu Nchini**

**MHE. MWITA M. WAITARA K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa nyumba za walimu wa Sekondari nchini na kukarabati zilizochakaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa changamoto ya upungufu wa nyumba za walimu wa Shule za msingi na Sekondari nchini ambapo inatakiwa kutatuliwa. Katika mwaka 2022/2023 na 2023/2024, Serikali kupitia fedha za programu za kuimarisha elimu ya awali na msingi *(BOOST)* na sekondari *(SEQUIP)* pamoja na fedha za Serikali Kuu, imejenga nyumba 860 za walimu wa shule za msingi na sekondari zitakazochukua familia 2,018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025, Serikali itajenga jumla ya nyumba za walimu 562 zitakazochukua familia 1,124. Serikali itaendelea kutenga fedha kupitia programu za miradi mbalimbali na Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu ili walimu wetu wapate mahali bora pa kuishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa kijana wangu aliyepata ajali katika *Waitara Cup* kule Sirari na

namshukuru Mungu kwamba wahuni wote na shetani wameshindwa na Mungu ameshinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza kwa Serikali; swali la kwanza. Serikali ipo tayari kuleta takwimu za maboma ya nyumba za walimu msingi na sekondari nchi nzima kwenye majimbo yote ambayo wananchi wameweka nguvu zao kuyajenga na yameishia kwenye lenta na kuonyesha mkakati namna ambayo watakamilisha maboma hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Halmashauri yangu ya *Tarime DC* ina mapato makubwa. Serikali ipo tayari kutoa maelekeza mahususi kukamilisha maboma yote ambayo wananchi wangu wamechangia nguvukazi ili wapate nguvu kuendelea kuchangia maboma mengine baada ya kukamilisha yale ambayo wameshiriki kuyajenga? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake haya yenye tija. Kuhusiana na swali lake la kwanza, Serikali tayari imeshafanya tathmini ya kubaini ni maboma mangapi kwenye sekta ya elimu pamoja na sekta ya afya ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na tayari tathmini imekamilika na Serikali inafanya taratibu za kuhakikisha fedha inapatikana ili kuweza kuunga mkono jitihada zile za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la takwimu Mheshimiwa Mbunge tunaweza tukawasiliana nikakupatia lakini tayari Serikali ilishafanya tathmini kubaini idadi ya mabama na kiasi gani cha fedha kinahitajika kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili; Halmashauri anayotoka yeye anasema ina mapato makubwa na kwamba tayari kuna maboma ambayo wananchi walianza kuyajenga. Nitumie nafasi hii kuendelea kusisitiza kwamba pale

kunapokuwa na juhudi za wananchi Halmashauri na Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa zinakuwa na uwezo na ni lazima ziweze kutenga fedha na kuzingatia vipaumbele kuweza kuunga mkono jitihada za kuendeleza miundombinu na hasa hii muhimu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nichukue nafasi hii kuendelea kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri kutoka anapotokea Mheshimiwa Mbunge ili waweze kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuendelea kuendeleza miundombinu hii muhimu katika sekta ya elimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je ni lini sasa Serikali itajenga shule ya sekondari ndani ya Jimbo la Temeke kwenye Kata ya Makangarawe kwa sababu tulikuwa hatuna eneo lakini sasa hivi tumepata eneo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia programu ya *SEQUIP* imekuwa ikijenga miundombinu ya shule zetu hizi katika kata. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge bila shaka shule hii uliyoitaja ya sekondari itajengwa kupitia *program* hii ya *SEQUIP*. Kwa hiyo Serikali itaendelea kufanya tathmini na kuweka vipaumbele na shule shule hii Serikali itakuja kujenga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa. Ni lini Serikali itajenga nyumba za walimu katika shule za Sekondari za Jimbo la Newala Vijijini ili kuwapunguzia umbali walimu ambao wanakaa mbali na shule? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga nyumba za walimu kupitia taratibu mbalimbali na kupitia utaratibu wa *program*. Kwa mfano programu ya *GPE, TSP* na kupitia mradi wa *SEQUIP* Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba inatenga fedha mahususi kabisa kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inatambua kwamba jukumu lote la kujenga nyumba za walimu haliwezi kutekelezwa na Serikali kuu peke yake. Ndiyo maana tunasisitiza na Halmashauri zenyewe ziweze kutenga fedha kutoka kwenye mapato yake ya ndani na Wakurugenzi waweze kufanya tathmini sahihi ya kujua uhitaji wa nyumba hizi za walimu ili kwa pamoja kupitia miradi hii inayotoka Serikali Kuu na kupitia mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa pamoja tuweze kushirikiana kuhakikisha kwamba walimu wanajengewa nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa muktadha huo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuhakikisha fedha zinapatikana kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu Tanzania nzima lakini pia hususan katika Mkoa na Jimbo analotoka Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea swali linalofuata Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 653

**Changamoto za Walimu Mkoa wa Mara**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, hatua gani zinachukuliwa ili kupunguza changamoto ya walimu katika shule za msingi na sekondari mkoani Mara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kila mwaka kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023, Serikali iliajiri walimu 29,879 wakiwemo walimu 16,598 wa shule za msingi na walimu 13,281 wa shule za sekondari. Mkoa wa Mara ulipangiwa walimu 754 wa shule za msingi na walimu 412 wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023/2024 Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 ambao watapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu mkubwa ikiwemo Mkoa wa Mara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ni dhahiri kwamba Serikali kwa sasa imewekeza sana kwenye kujenga miundombinu ya shule kwa maana ya kuongeza madarasa kwa shule za msingi na sekondari. Vilevile kupitia elimu bila ada imehamasisha wananchi wengi kuweza kupeleka watoto wao shule. Sasa hii kasi ya kuajiri walimu 12,000 kwa mwaka ni kasi ndogo sana ukilinganisha na upungufu wa walimu uliopo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani Mkoa wa Mara kwa shule za msingi tuna uhitaji wa walimu 14,000 lakini waliopo ni 8,000 tu. Tuna upungufu wa walimu 6,000 na kitu, walimu wanaojitolea ni 785 kwa shule za msingi na sekondari ni 284. Serikali inapokuwa inaajiri walimu haitoi kipaumbele kwa hawa wanaojitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, ni kwa nini msishushe waraka kwenda halmashauri kutoka kwenye *own source* zao walau waweze kutenga kati ya shilingi 100,000 mpaka 200,000 kuwapa kama *token* hawa wanaojitolea ku-*supplement* ile ambayo wazazi wanachanga ili watoto wetu waendelee kupata masomo na haki ya kufundishwa kama wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, hata Dira yetu ya Maendeleo inasema uchumi shindanishi na viwanda kwa maendeleo ya watu. Sasa ukiangalia takwimu za walimu wanaofundisha masomo ya sayansi Mkoa wa Mara tunauhitaji wa walimu 1,900 wakati tunao walimu 1,000 tu. Sasa hivi Serikali inajenga shule za sayansi kwa wasichana kwenye mikoa yetu hii. Serikali inachukua jitihada gani kuhakikisha kwamba inaajiri walimu wengi wa sayansi ili kwenda kuziba haya mapengo? Kwa sababu usipokuwa na walimu wa sayansi, watoto wanamaliza bila kupata elimu na viwanda vyenyewe tunavyovileta hapa Tanzania havitapata wajuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri sana. Kama alivyosema yeye mwenyewe ametambua jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata elimu iliyo bora na ndiyo maana kwa sasa hivi tunatekeleza Mpango wa Elimu Bila Ada na matokeo yake udahili umeongezeka na mahitaji ya miundombinu ya elimu yameongezeka na uhitaji wa walimu umeongezeka na Serikali imekuwa na mikakati tofauti tofauti kuhakikisha inaboresha miundombuinu, lakini pia kwenye eneo la walimu Serikali inachukua hatua, mfano ajira, kwa hiyo, Serikali tayari kila mwaka inahakikisha kwamba inaajiri walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Serikali inatumia mpango wa walimu wa kujitolea na Mheshimiwa Mbunge hapa amefanya rejea. Kwa hiyo, Serikali kwa kutumia utaratibu huo inakuwa inahakikisha kwamba inaongeza pia idadi ya walimu wanaohitajika. Nitatoa tu mfano, katika Mkoa wa Mara kuna walimu wa kujitolea 625 katika shule za *primary* na walimu 185 wa kujitolea katika shule za sekondari. Serikali pia inatumia mbinu ya kutumia TEHAMA na hivi sasa Serikali imeanzisha ujenzi wa madarasa janja *(smart classes)* ambayo yanatumia TEHAMA na

mwalimu mmoja anaweza kufundisha shule tofauti tofauti au shule zaidi ya moja na nje ya mkoa mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inatumia na imeanzisha utaratibu wa kuanza kuwatumia wanafunzi wa ualimu na kuwapa ule mwaka mmoja wanakuwa wanafanya mafunzo kwa vitendo *(internship)*. Hii yote ni mikakati ya kuhakikisha kwamba Serikali inapunguza ukali wa upungufu wa walimu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge katika swali lako hili la kwanza Serikali itaendelea na utaratibu wa kutoa miongozo mbalimbali na kutumia hii mikakati ili kuhakikisha kwamba inabuni namna nzuri zaidi ya kuweza kuongeza walimu. Kama vile Serikali inavyohakikisha kwamba inajenga miundombinu mizuri ya kutosheleza ongezeko la udahili wa wanafunzi, basi hivyo hivyo itahakikisha kwamba inaongeza walimu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka za Serikali za Mitaa tumeshawaelekeza kwamba wanaweza wakatumia mapato ya ndani kwa ajili ya kulipa walimu wanaojitolea ili na wenyewe kuchangia katika kupunguza upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili ameuliza kuhusiana na walimu wa sayansi; Serikali itazingatia katika ajira hizi lakini katika upatikanaji wa walimu kwa njia nilizozitaja hapo awali, kwamba wanapatikana walimu wa sayansi na hasa huko vijijini kwa sababu huo ndiyo mpango wa Serikali na ndiyo mpango wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu iliyobora. Pia amejielekeza katika kuhakikisha tunajiimarisha katika masomo ya kisayansi. Kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuhakikisha tunapata walimu walio bora wa kutosheleza kufundisha masomo ya kisayansi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa halmashauri zilizo na

uhaba mkubwa sana wa walimu hasa katika Kata ya Ilangu, Ipwaga, Mnyagala na Isengule kwenye shule za sekondari.

Je, ni lini wataleta walimu ili waweze kufanya kazi kwenye maeneo ya kata hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mbunge, swali lake ni la msingi na kama nilivyotangulia kujibu hapo awali, Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 mwaka huu. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na yeye kwenye jimbo lake atapata mgao wa walimu hawa 12,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza mbinu na mikakati mbalimbali ambayo pia inatumiwa na Serikali kupunguza ukali wa upungufu wa walimu. Mkakati mmojawapo ni kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa na zenyewe zinajipanga kutenga bajeti kwenye mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuweza kuajiri walimu kwa mikataba ili waweze kupunguza ukali wa uhitaji wa walimu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kwa njia hizi Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inaleta walimu shuleni katika jimbo lako lakini pia inatumia mbinu tofauti tofauti za kupunguza ukali wa upungufu wa walimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbogwe ina changamoto ya upungufu wa walimu, je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri walimu wanaojitolea kwenye Halmashauri ya Mbogwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu awali kwamba Serikali itaendelea kuajiri walimu na katika mgao wa walimu hawa 12,000 wanaotarajiwa kuajiriwa, Mheshimiwa Mbunge na wewe utapata mgao wa walimu kwenye shule zilizopo katika jimbo lako, lakini kupitia mapato ya ndani ya halmashauri pia mnaweza mkatenga bajeti maalumu kwa ajili ya kuhakikisha mnaweza kuajiri kwa mikataba pia kuwalipa posho walimu wanaojitolea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; kuhusu shule za mijini na shule za vijijini, za mijini huwa zinakuwa na walimu wengi ukilinganisha na shule za vijijini. Sasa Serikali ina mpango gani wa kutoa kipaumbele kwenye shule za vijijini pindi ajira za walimu zitakapotoka, hususani Tunduru Kaskazini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 na katika mgao wa walimu hao bila shaka Mheshimiwa Mbunge utapata mgao wako. Hoja yako ya kuzingatia uhitaji mkubwa unakuwepo kwenye maeneo ya mjini ni ya msingi na katika mkakati mmojawapo ukiacha tu ajira, Serikali imekuwa ikitumia utaratibu wa kufanya msawazo wa walimu, yaani kutazama yale maeneo ambayo yana upungufu mkubwa na kuweza kufanya msawazo kwa kuhamisha walimu kutoka kwenye maeneo ambayo yana walimu wengi zaidi kuliko maeneo yenye upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali itaendelea kutumia taratibu hizo za kufanya msawazo wa walimu ili kupunguza ukali wa upungufu wa walimu katika shule zilizopo pembezoni katika jimbo lako Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa walimu nchini ni tatizo kubwa sana ukilinganisha na ongezeko la shule za msingi na sekondari kwa kila mwaka zinazojengwa vijijini, lakini miaka kumi iliyopita kulikuwa na upungufu mkubwa sana wa walimu wa sayansi, Serikali ilifanya mkakati Chuo cha *UDOM* kuweka *special courses* kwa ajili ya kuongeza idadi ya walimu nchini na tumefanikiwa, lakini walimu hao bado wako mitaani na hakuna ajira. Nini mpango wa Serikali wa kuajiri walimu wa sayansi kwenye shule zetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu awali kwamba Serikali imekuwa ikiajiri walimu kila mwaka. Mathalani mwaka huu 2023 yaani mwezi wa tano Serikali iliajiri walimu 13,130. Pia nimesema katika awamu inayofuata Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kuajiri walimu kwa kuzingatia pia upatikanaji wa fedha, bajeti na vipaumbele, lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa kupata walimu na ndiyo maana nimeeleza mikakati mbalimbali hapa ambayo inatumika na Serikali kuhakikisha kwamba inapunguza ukali wa upungufu wa walimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, Jimbo la Busanda lina sekondari ya *high school* inaitwa *Butundwe Secondary School* ambayo ina mchepuo wa kilimo, lakini ina upungufu wa walimu wa kilimo.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba shule hiyo inapata walimu wa kutosha wa kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 na katika ajira hizo Serikali inazingatia pia mahitaji mbalimbali ikiwemo umuhimu wa kupata walimu wa masomo ya kilimo katika shule yako hiyo.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba inaweza kukuletea walimu wa kilimo katika shule yako hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa awamu tatu sasa Serikali haijapeleka hata mwalimu mmoja kwenye Jimbo langu la Lulindi kwa maana ajira tatu zimepita. Je, Serikali itatuhakikishiaje awamu hii sasa tutapata walimu katika shule zetu za Lulindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu huko awali, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ajira 12,000 mgao utapita pia katika jimbo lake. Kwa hiyo, awe na amani Mheshimiwa Mbunge kwa kuzingatia mahitaji ya walimu katika jimbo lake na yeye atapata mgao wa walimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 654

**Ujenzi wa Mitaro Barabara za Milimani Kilimanjaro**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga mitaro ili kuzuia uharibifu wa barabara unaosababishwa na mvua katika maeneo ya milimani Mkoani Kilimanjaro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na uharibifu wa barabara za milimani unaosababishwa na mvua, Serikali kupitia bajeti zake inahakikisha kuwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara katika maeneo hayo, ujenzi wa mifereji unapewa kipaumbele ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha zege na ujenzi wa mikanda ya zege *(concrete strips)* katika maeneo yenye miinuko mikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 shilingi bilioni 2.057 zilitumika kujenga mifereji yenye urefu wa mita 8,066, mikanda ya zege *(concrete strips)* mita 600 na barabara za zege mita 4,985 katika maeneo ya milimani katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Serikali imepanga kutumia shilingi bilioni 2.077 kwa ajili ya kujenga barabara za zege mita 3,425, mikanda ya zege *(concrete strips),* mita 2,500 na mifereji ya maji ya mvua mita 2,250 katika maeneo ya milimani mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti katika miaka ijayo kwa ajili ya kujenga barabara za zege, mikanda ya zege *(concrete strips)* na mifereji ya maji ya mvua katika maeneo ya milimani Mkoani Kilimanjaro kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naishukuru Serikali kwa juhudi za kutenga fedha za kujenga

mitaro hiyo, lakini kwa kuwa tatizo hili ni kubwa sana na ni la siku nyingi na ni endelevu, naomba kufahamu, je, Serikali imeshafanya usanifu kwenye maeneo gani ya kuleta suluhisho la kudumu katika maeneo yote hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tatizo hili liko Mkoa wote wa Kilimanjaro katika majimbo yote tisa, kuanzia Jimbo la Siha, Hai, Moshi Vijijini, Vunjo, Rombo, Mwanga, Jiimbo la Same Mashariki hadi Same Magharibi na hata Manispaa ya Moshi huwa inaathirika na tatizo hili. *(Makofi)*

Sasa swali langu, kwa kuwa maji hayo yakitoka kwenye milima yanatirirka hovyo barabarani, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabwawa ya kukinga maji hayo ili yatumike kwenye kilimo au mifugo na tatizo hili kuisha kabisa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake haya muhimu sana na yenye tija. Naomba nimjibu maswali yake yote mawili kwa pamoja kuwa tafiti tayari zilifanyika mwaka 2014 katika Wilaya ya Siha na Serikali ilibaini kwamba ujenzi wa barabara za zege una tija sana, lakini ikabaini pia kutua *paving blocks* na *strip concretes* na ujenzi wa majaribio ulifanyika katika barabara ya Lawate – Kibong'oto na kimsingi majaribio yalionesha ufanisi mkubwa.

Kwa hiyo, kwa hivi sasa baada ya kufanya *performance evaluation,* majaribio na kuonesha ufanisi sasa mkoa unatekeleza ujenzi wa miundombinu hii katika maeneo mengine ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge suala lake ni la muhimu sana na Serikali tayari imeshakuwa na mipango na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha inajenga miundombinu iliyobora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mapendekezo, mawazo na ushauri wako wa ujenzi wa mabwawa ya kupokea maji hayo kwa ajili ya matumizi ya kilimo, ni maoni na mawazo mazuri na sisi kama Serikali tunayapokea, kuyachakata na kuona namna nzuri ya kufanya utekelezaji wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha zege barabara zilizopo kwenye miinuko katika Milima ya Matumbi inayoanzia Pungutini kupitia Mwengei kwenda Kibata hadi Kipatimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiboresha kufanya ujenzi na marekebisho ya miundombinu ya barabara kwa kuzingatia pia topografia ya eneo husika na kama nilivyotangulia kutolea mfano katika maeneo ya Kilimanjaro ambayo yana miinuko. Serikali imekuwa ikitumia teknolojia ya kuweka zege ambayo inakuwa na ubora zaidi na inaweza kuhimili changamoto mbalimbali za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika utaratibu huo huo Serikali itaendelea kuhakikisha inatafuta fedha kuhakikisha kwamba miundombinu bora hii ya zege na hasa katika maeneo ya miinuko katika jimbo lake yanaweza kujengwa ili nao waweze kupata barabara zilizobora zitakazopitika katika mwaka mzima na zitakazoweza kuhimili misukosuko ya kimazingira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatriopia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ninavyoongea sasa hivi barabara ya kutoka Nkwenda kwenda Mabira, pia barabara ya kutoka Kakanja

kupita Kikukuru mpaka kwenda Kitwe hazipitiki na sasa ni wakati wa kiangazi na ni maeneo makubwa ambayo sasa yanazalisha kahawa. Nini mkakati wa dharura wa kutengeneza hiyo barabara ili tuweze kupeleka kahawa yetu sokoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikichukua hatua za dharura kufanya marekebisho katika maeneo ya barabara ambazo mawasiliano yamekatika na imekuwa ikifanya hivyo katika maeneo mbalimbali ya nchi, hasa ukizingatia athari ambazo zimetokana na mvua kubwa ambayo imekuwa ikinyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusiana na barabara hii ya Nkwenda – Mabira na Barabara ya Kakanza – Kitwe, ambayo anasema ni muhimu sana hasa katika biashara ya kahawa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi Serikali tumepokea na kwa sababu kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuhakikisha inarudisha mawasiliano ya barabara kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika nakuhakikishia, Mheshimiwa Mbunge, suala hili tumelipokea, kwa ajili ya kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Nusrat Shabani Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Tunza Malapo.

Na. 655

**Vijiji vya Mkoa wa Singida Kuunganishiwa Umeme**

**MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, ni lini vijiji vyote vya Mkoa wa Singida vitaunganishiwa umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida una jumla ya vijiji 441 ambapo kati ya hivyo, vijiji 439 vimekwishapatiwa umeme na vijiji viwili bado havijapatiwa umeme. Kazi ya kukipatia umeme Kijiji cha Ndwamuganga inaendelea ambapo ujenzi wa miundombinu umeshakamilika. Hatua inayofuata ni *TANESCO* kufanya ukaguzi, ili kujiridhisha na kazi kabla ya kuwasha umeme katika kijiji hicho. Aidha, kwa Kijiji cha Mkenene, kulikuwa na changamoto ya kukifikia kutokana na kufurika kwa Mto Iyumbu. Kwa sasa, hali imetulia na mkandarasi ameshaanza hatua za awali za kupeleka nguzo, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kupeleka umeme katika kijiji hicho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza. Sisi kule kwetu Mtwara, kwenye majimbo ya Tandahimba, Newala Vijijini pamoja na Lulindi bado kuna vijiji vingi havijapatiwa umeme. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha vijiji vile ambavyo vimebaki vinapatiwa umeme kwa haraka? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba, vijiji vyote nchini vinapatiwa umeme na kama ambavyo mmeidhinisha bajeti ya Wizara husika, yapo mafungu

yametengwa, kwa ajili ya kazi hiyo. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira, jambo hili litakamilika kama tulivyoahidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itaanza mradi wa usambazaji wa umeme kilometa mbili katika Jimbo la Babati Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari mikakati ipo katika hatua za mwisho kuhakikisha kwamba, umeme unafikishwa katika Jimbo la Babati Vijijini. Namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati tunatekeleza jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Wilaya ya Ngara, vijiji 14 bado havijawasha umeme. Ningependa kujua ni lini Serikali itawasha vijiji hivyo, ili kuwaondolea adha wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kule Ngara vijiji 14 havijawashiwa umeme. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tunayo mikakati ya kuhakikisha kwamba, ndani

ya kipindi kifupi vijiji vyote nchini, siyo hivyo vya Ngara tu, lakini vijiji vyote nchini vitapatiwa umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Ninafahamu kwamba, sasa tayari tumeshawasha mtambo namba mbili wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa hiyo, tatizo la umeme limeisha. Ni nini kinasababisha kukatika-katika kwa umeme katika baadhi ya maeneo kwa sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Serikali imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha upatikanaji wa umeme unaimarika kutokana na kuongezeka na kuzalishwa kwa umeme kupitia Bwawa la Mwalimu Nyerere. Vilevile, kama ambavyo tumekuwa tukisema mara nyingi hapa, miundombinu yetu ya kusambaza umeme na yenyewe imekuwa na changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hii ndiyo ambayo inachangia katika kukatika-katika kwa umeme, lakini kama ambavyo tumeonesha kwenye bajeti yetu, Serikali imetenga fedha nyingi, kwa ajili ya kuboresha usambazaji wa umeme kwa kuboresha njia za usambazaji. Namuomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wawe na subira wakati tunakamilisha utengenezaji wa miundombinu hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, naishukuru Serikali kwa kuendelea kusambaza umeme kwa hali ya juu katika maeneo, lakini nataka kujua katika maeneo ambayo yameachwa na yako karibu na laini kubwa ni

lini wataweka katika maeneo ya Lutongo, Iponyabugali, Kasamwa, Kabangaja, Monze, Iramba A, Uwerashinga, *list* ni ndefu mpaka mitaa 21, ni lini wataweka umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, kipaumbele kimekuwa kufikisha umeme kwenye vijiji, lakini ni kweli, vilevile kwamba, wakati tunapitisha laini kubwa yapo maeneo ambayo yameachwa. Mkakati wa Serikali sasa ni kuja na mpango wa kuhakikisha kule kote ambako laini kubwa imepita sasa ni kujielekeza kwenye kuhakikisha tunashusha nyaya na *transformer* kuhakikisha maeneo haya nayo yanawekewa umeme. Kwa hiyo, namuondoa hofu Mheshimiwa Mbunge, vitongoji hivi na maeneo haya yatapatiwa umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge tuna shughuli zinazoendelea nje ya kikao hiki cha Bunge.

Kuna Kamati Maalum ina kazi maalum na Wajumbe wake walikuwa na maswali. Mniruhusu nisitishe Wizara ya Nishati, itarejea tena kuendelea kujibu maswali. Naomba niende kwenye Swali Na. 658 la Wizara ya Kilimo na baada ya swali hili nitarejea tena kwenye Nishati.

Kwa hiyo, ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ninakwenda kwenye Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naanza kwa kumpa pole Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Nurdin Babu, pamoja na Wananchi wa Kilimanjaro kwa msiba wa Afisa Tawala wetu wa Mkoa.

Na. 658

**Kurejesha Ruzuku ya Pembejeo za Dawa kwa Wakulima wa Kahawa**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarejesha utoaji wa ruzuku ya pembejeo za dawa kwa wakulima wa kahawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya soko la kahawa inayozalishwa kwa teknolojia ya kilimo hai, kwa maana ya *organic coffee,* ambayo husababisha wakulima kupata bei nzuri katika soko, Serikali inahamasisha wakulima kutumia njia mbadala ya matumizi ya dawa kwenye uzalishaji wa kahawa ikiwa ni pamoja na kupanda miche chotara ambayo inazalishwa na kusambazwa bure na Bodi ya Kahawa Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (*TaCRI*). Aidha, miche ambayo inazalishwa na kusambazwa kwa wakulima ina ukinzani na magojwa makuu ya kahawa ya chole buni na kutu ya majani ambayo ndiyo yaliyokuwa yanasababisha mahitaji ya matumizi makubwa ya dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa 2023/2024, jumla ya miche 21,899,560 ilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima wa kahawa katika mikoa yote inayozalisha kahawa hapa nchini. Kati ya miche hiyo, Mkoa wa Kilimanjaro ulipata miche 1,664,635 ambayo imesambazwa kwa wakulima ambapo Wilaya ya Moshi

imepata jumla ya miche 328,110 na kusambazwa kwa wakulima kupitia Vyama vya Ushirika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi, maswali ya nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu hayo, miche wanayoigawa huwa ina ukinzani wa magonjwa na siyo wadudu. Sasa kwa kuwa wakulima wengi hawawezi kumudu kununua viuatilifu vya wadudu, je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha matumizi ya dawa za kiasili kama vile utupa, ili kukabiliana na wadudu wanaoharibu kahawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kahawa huwa inahitaji maji mengi sana na maji haya yamekuwa yanapatikana kupitia mifereji ya asili. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wananchi wa Jimbo langu la Moshi Vijijini kurekebisha mifereji ya asili, ili waweze kumwagilia kahawa zao ukiwepo ule Mfereji wa Makeresho ambao ulikuwepo kwenye bajeti? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, cha kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, Profesa Ndakidemi, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake la Moshi Vijijini, hususan katika kuhamasisha kilimo cha kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namthibitishia kwamba, nimezungumza na wataalamu na tumekubaliana kwamba, sisi tutakuwa tayari kuhamasisha hususan matumizi ya dawa za asili, ili kutoondoa ubora wa kahawa ambayo inazalishwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara tuko tayari kusajili watu wote ambao wanazalisha viuatilifu vya asili, kama ambavyo wanafanya *bio-plants* walioko Moshi na tumekubaliana tutanunua kwa ruzuku katika mwaka unaokuja karibu lita 20,000.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo mipango na mikakati ya Serikali, ili kuhakikisha tunawasaidia watu wa zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifereji. Tulishaliweka katika bajeti yetu na sasa hivi tunachokifanya ni kuendelea tu kupitia, ili tuje tutafute mkandarasi tuweze kuiboresha na kuwa ya kisasa, ili wananchi waweze kumwagilia kipindi chote na wapate maji ya uhakika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wananchi wa Tarafa ya Nambis katika Jimbo la Mbulu Mjini wanajitahidi sana kulima zao la kahawa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea miche bora ya kahawa kupitia ruzuku ya Serikali, ili waweze kuleta tija zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namuambia tu kwamba, miche tunayo, muda wowote wakulima waje tuwakabidhi. Ndiyo maana unaona hata kwenye jibu la msingi, tumezalisha miche milioni 21.89 na tumegawa yote bure. Kwa hiyo, watufikie tu na sisi tutaifikisha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku katika mbegu ya mahindi ambayo kwa sasa bei yake iko juu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mkakati wa Serikali ni kutoa ruzuku kwa pembejeo. Pembejeo tunamaanisha ni mbegu pamoja na mbolea kwa hiyo, hata kwenye mbegu kuna pembejeo. Changamoto ambayo ilitokea wakati uliopita ni kwamba, mbegu ambazo zinazalishwa

au zinaagizwa kutoka nje ya nchi na kampuni binafsi ndiyo walau bei yake ilikuwa iko juu kidogo tofauti na zile mbegu ambazo tunazizalisha sisi wenyewe kupitia taasisi yetu ya *ASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana utaona kulikuwa na tofauti kubwa sana. Bei ya *ASA* ilikuwa ni wastani wa shilingi 7,000 wakati wale wengine walifika kuanzia shilingi 16,000 mpaka shilingi 20,000. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kuweka msisitizo na ku-*control* bei, ili kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata bei halisi ambayo inaweza kuwasaidia kila mmoja kumudu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri utaendelea na awamu ya pili ya maswali. Naomba nimrejeshe Naibu Waziri, Wizara ya Nishati, kwa Swali Namba 656.

Mheshimiwa Edwin Enossy Swale, Mbunge wa Lupembe. Swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

Na. 656

**Kupeleka Umeme wa *REA* Kwenye Vitongoji vya Jimbo la Lupembe**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA K.n.y. MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme wa *REA* kwenye Vitongoji vya Jimbo la Lupembe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lupembe lina vitongoji 227 ambapo vitongoji 118 vimekwishapatiwa umeme na vitongoji 109 bado havina umeme. Hata hivyo, vitongoji 19 vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Ujazilizi IIB ambapo mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu. Vilevile vitongoji 15 vitapatiwa

umeme kupitia Mradi wa Vitongoji 15 kila Jimbo, ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kuanza hivi punde. Hivyo, vitasalia vitongoji 75 ambavyo vitapatiwa umeme kupitia mradi mkubwa wa "*Hamlet Electrification Project*" ambao utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2024/2025 kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwenye miradi hii ya vitongoji ambayo nimeitaja *concern* kubwa ni Kijiji cha Madeke ambacho mradi huu ulianza mwaka 2021 mpaka leo bado. Inaelekea kama kuna uzembe unaosababisha mradi huu usifanyike kwa spidi kubwa. Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha Kijiji cha Madeke kinapatiwa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Halmashauri ya Mji wa Njombe tuna maeneo ambayo yalikuwa *identified* ya uwekezaji na bajeti imeshaletwa kwenye Wizara, kwa ajili ya maeneo ya Ngaranga na Magoda. Ni lini sasa Serikali itakamilisha kupeleka umeme kwenye maeneo haya ya uwekezaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge Mwanyika kwa maswali mawili ya nyongeza. Moja ni kuhusiana na Kijiji cha Madeke; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge wakandarasi ambao wanatekeleza mradi wa kupeleka umeme vijijini tunawasimamia kwa weledi mkubwa sana na ndiyo maana mpaka leo ni vijiji 400 tu kati ya vijiji 12,800 ndiyo vimebaki kupelekewa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutamfuatilia mkandarasi na tutamsimamia kwa nguvu sana, ili kuhakikisha anatumia muda ambao tumeutenga, kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye vijiji ifikapo Mwezi Juni mwaka huu.

Pia, tutafuatilia, ili kuona mkandarasi ana changamoto gani na kisha baada ya hapo tutamsimamia kwa nguvu sana, ili mradi huu ukamilike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na sehemu ya Ngaranga pamoja na Mbagoda, ambapo kumetengwa fedha kwa ajili ya uwekezaji; kwa hili namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kufuatilia kwa karibu, ili kuhakikisha kwamba, mradi huu unaanza kutekelezeka. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na ninamuahidi tutaendelea kufuatilia kuona utekelezaji wake unaanza hivi karibuni. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali imedhamiria kupeleka umeme vijijini kote nchini ikiwemo kwenye jimbo langu ambako vijiji vingi vinapatiwa umeme. Ni lini mtaanza kutekeleza kupeleka umeme katika vitongoji 15 katika Jimbo la Manyoni Magharibi, Halmashauri ya Itigi, ambavyo tulileta hapa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali kuhusu vitongoji 15. Kama nilivyosema mapema wiki hii, tupo katika hatua za mwisho za kumalizia, ili kuweza kuwapata wakandarasi katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, suala la kupeleka umeme kwenye vitongoji, ambako tuko mwishoni kumalizia, ni suala ambalo ni la kipaumbele kwenye Serikali ya Awamu ya Sita. Ndiyo maana hata mwaka wa fedha unaokuja, 2025, tumetenga fedha nyingine, kwa ajilai ya kuanza mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 20,000 ambapo kwa mwaka wa fedha 2025 tutapeleka umeme kwenye vitongoji 4,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunalifanya jambo hili kwa kasi kuhakikisha kwamba tunaanza kupeleka umeme vitongojini. Kwa jimbo la Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha pia kazi inaanza na vitongoji 15 vinapatiwa umeme huku tukisubiri mradi wa 2024/2025 ambao unaanza kupeleka umeme kwenye vitongoji 20,000, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mkoa wa Simiyu una vitongoji vingi sana ambavyo havijapata umeme wa *REA*. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA* katika vitongoji hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kupeleka umeme kwenye vitongoji ambavyo bado havina umeme katika Mkoa wa Simiyu; tayari tuna miradi ambayo inaendelea ikiwemo miradi ya ujazilizi. Kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kupeleka umeme ili wananchi waweze kunufaika na umeme, ndiyo maana tumebuni miradi mbalimbali ya kuhakikisha umeme unafika kwenye vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama nilivyosema hapo awali, kila Jimbo la Mkoa wa Simiyu, hivi karibuni itapata vile vitongoji 15. Katika mgawanyo wa vitongoji katika mradi wa mwaka 2024, pia tutazingatia ili majimbo ya Mkoa wa Simiyu na yenyewe yaweze kupata umeme, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nampongeza mdogo wangu Mheshimiwa Judith, kwa kweli anafanya kazi nzuri, ana uwezo wa kujibu maswali vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua, kwenye Jimbo la Bunda Mjini, kati ya kata 14, kata saba ziko vijijini na bado hii programu ya kupeleka umeme vijijini haijafika. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha vitongoji vya Jimbo la Bunda Mjini hasa kwenye kata za vijijini zinapata umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namshukuru sana Mheshimiwa Ester Bulaya kwa swali lake. Kuhusiana na umeme katika Jimbo la Bunda Mjini, kuna changamoto kweli kwenye Jimbo la Bunda Mjini, kuna maeneo ya mji na kuna maeneo ya vijijini. Ndiyo maana kwa mwaka ujao wa fedha, tayari tumeshafanya utaratibu kwanza kuhakikisha mitaa ya Bunda Mjini ambayo haina umeme, inapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ya vitongoji, tutaendelea kupeleka umeme kwa miradi ya umeme ambayo tunayo ya kupeleka umeme kwenye vitongoji ikiwemo vile vitongoji 15. Pia tutahakikisha katika mradi ujao wa vitongoji 2025 na Bunda Mjini na vitongoji vyake vitazingatiwa kupata umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni lini mkandarasi wa mradi wa umeme jazilizi kwenye vitongoji ataanza kazi katika Jimbo la Tunduru Kusini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kweli kwenye Jimbo la Tunduru Kusini tunategemea kuwa na umeme jazilizi, pia, baadhi ya maeneo ambayo bado yalikuwa hayajapelekewa umeme kwenye vijiji, ilikuwa inarudisha nyuma zoezi kwa sababu kwanza ilikuwa tufike kwenye vijiji. Kwa kuwa sasa hivi tunaenda mwishoni katika mradi wetu wa kupeleka umeme vijijini, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, mradi wa

ujazilizi utakuja Tunduru Kusini na wananchi watapata umeme katika vile vitongoji ambavyo viko kwenye mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge ambaye anafanya kazi nzuri kwamba vitongoji vya Tunduru Kusini vitapelekewa umeme na wananchi wataweza kunufaika na huduma hii ya umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Serikali ya CCM imefanya kazi kubwa sana ya kupeleka umeme kwenye vitongoji mbalimbali na vijiji lakini sasa kwa sababu tuna-*sort* vitongoji, unakuta kitongoji A kimetoka kimekwenda kupata umeme, nguzo zimepita katika vitongoji C, B zimeacha, wenyewe wale A wamepata.

Serikali ina mkakati gani wa kutafuta *transformer* na nguzo ndogo, kuwapelekea mameneja wa *TANESCO* wa maeneo ya Bunda hasa Jimbo langu la Bunda ili vitongoji ambavyo vina nguzo kubwa, vipewe umeme kwenye maeneo ambayo yamepitiwa na nguzo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namshukuru Mheshimiwa Mbunge Getere kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kupeleka umeme kwenye vitongoji ambavyo viko mbele zaidi lakini havijapatiwa umeme na cha nyuma kimepatiwa umeme. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, maendeleo ni hatua, ilibidi tuanze kupeleka umeme kwenye vijiji ili tuweze kufikia yale maeneo ya vitongoji ambavyo havina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama vile ambavyo tulianza kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji, tunavyomaliza sasa, tunakuja hatua ya kupeleka umeme kwenye vitongoji. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge,

vitongoji vitapata umeme kulingana na jinsi ambavyo tunasogea. Vilevile, namuhakikishia kwa kuwa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha vitongoji vinapata umeme na Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba tumetoka kwenye vitongoji elfu sitini naa, lakini leo hii tupo kwenye vitongoji 33,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kazi kubwa imefanyika, naomba atuazime imani ili tuendelee kupeleka umeme kwenye vitongoji. Nataka kumtia moyo yeye pamoja na Wananchi wa Jimbo la Bunda kwamba watapata umeme, ni kwamba tu inabidi tuvumiliane kwa sababu maendeleo ni hatua, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaenda swali linalofuata. Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Kabudi, Mbunge wa Kilosa, sasa aulize swali lake.

Na. 657

**Ujenzi wa *Sub-Station* ya Umeme Dumila**

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga *Substation* ya umeme katika eneo la Dumila – Kilosa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu wa Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* itatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Morogoro hadi Dumila yenye urefu wa kilometa 66 na ujenzi wa kituo cha kupoza Umeme katika eneo la Magole – Dumila kupitia mpango wa Gridi Imara awamu ya pili unaotarajia kuanza mara tu baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizofanyika katika hatua za awali za mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na taratibu za

kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huu zinaendelea. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha eneo la Dumila na maeneo jirani kuwa na umeme wa uhakika na gharama za mradi ni takribani dola za Marekani milioni 39, ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali ya swali langu, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza la nyongeza, je, ni lini Serikali itaimarisha ofisi ya *TANESCO* Dumila ili iweze kutoa huduma bora na kuweza kusambaza umeme katika Mji wa Dumila ambao unakua kwa kasi kubwa sana na sasa una wakazi zaidi ya 40,000?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nguzo zimekuwa zinabadilishwa katika *line* ya sasa ya umeme na nguzo hizo bado ni bora na zinaweza kutumika. Je, Serikali inafikiriaje kuhusu kutumia nguzo hizo kueneza umeme katika vitongoji mbalimbali vya eneo la Jimbo la Kilosa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nampongeza Mheshimiwa Mbunge Profesa Palamagamba John Kabudi kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuhusu kuimarisha ofisi ya Dumila ambapo kwenye hilo eneo la Mheshimiwa Mbunge kuna makazi zaidi ya 40,000. Kwa kweli, ni dhamira ya Serikali kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi ili waendelee kupata umeme wa uhakika. Kama mtakumbuka, yalikuwa maelekezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, katika kuhakikisha kwanza, wafanyakazi wa shirika wanafanya kazi kwa weledi na kwa kweli amefanikiwa sana katika hilo. Pili, kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha

huduma za umeme katika majimbo yote na katika maeneo yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha Ofisi ya Dumila, tayari tulishaanza kufanyia kazi, siyo tu kwa Dumila, bali kwa majimbo mengine yote ambapo ofisi za *TANESCO* zipo. Kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pale kwenye mapungufu, tutaenda kuyaangalia na kuhakikisha kwamba Wananchi wa Dumila wanaendelea kupata huduma nzuri ya umeme ili kuboresha shughuli zao za maendeleo na za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na nguzo za umeme, tumepokea Mheshimiwa Mbunge na tunao mkakati wa kueneza nguzo kwa miaka mitano ijayo. Tutaenda kuangalia kwa eneo hili la Dumila mkakati wake umekuwaje ili kuhakikisha kwamba nguzo ambazo zinatakiwa zinaenda. Nafahamu Wananchi wa Dumila ni wananchi ambao kwa kweli wanajishughulisha sana hususan katika viwanda vidogo vidogo vya kukoboa mpunga. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutaenda kuliangalia hili ili liweze kutekelezeka nawananchi waweze kuendelea vizuri na shughuli zao za maendeleo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mwaka jana niliuliza swali hapa kuhusiana na ujenzi wa *sub-station* Wilaya ya Mbinga na Serikali iliahidi kujenga *sub-station* mwaka huu. Je, ni lini sasa *sub-station* ya Wilaya ya Mbinga itajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na namshukuru Mheshimiwa Benaya kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, mradi wa kujenga kituo cha kupoza umeme pale Mbinga, upo katika hatua za kuweza kutekelezwa. Kama mnafahamu, mradi huu unatakiwa uanze kwa awamu ya pili baada ya awamu ya kwanza ya sasa hivi

kukamilika. Kwa kweli kwa awamu ya kwanza tumefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa Mheshimiwa Profesa Kabudi kwamba unatekelezeka ndani ya awamu ya pili na ndivyo hivyo kwa kituo cha kupooza umeme Mbinga. Kwa kweli tutasimamia kwa weledi mkubwa sana na nguvu kubwa sana ili *sub-station* ya Mbinga iweze kujengwa. Kwa kweli kwa pale Mbinga, kwa sasa hivi tumefanya miradi mikubwa sana, kwanza tumeanza ku-*stabilize line* ambayo inapeleka umeme kutoka Songea hadi Mbinga. Vilevile, *line* za Mbinga Vijijini kwa sababu umeme ulikuwa unakatika katika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo tumeanza kupeleka miradi ikiwemo miradi ya ujalizi ambayo kwa kweli Mbinga Vijijini ina miradi mingi sana, ina vitongoji vingi sana vya ujazilizi na inategemea kuanza hivi karibuni. Tutaendelea kuboresha ili kuhakikisha wananchi hawa wa Mbinga Vijijini wanendelea kupata umeme mzuri ili waweze kuboresha shughuli zao za maendeleo kwa sababu wananchi wa Mbinga Vijijini ni wachapakazi na wanajiendeleza sana katika maeneo ya viwanda vidogo katika maeneo ya kahawa na mahindi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuanza ujenzi wa kituo cha kupooza umeme pale Hanang mwaka 2022 na iliahidi itakamilisha mwaka 2023 mpaka sasa hakuna kilichoanza. Je, Serikali inaahidi nini Wana-Hanang ambao umeme kila siku unakatika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupeleka kituo cha kupooza umeme Hanang, ni kweli kituo cha kupooza umeme Hanang, kipo pia katika awamu ya pili ya utekelezaji. Kwa hiyo nampongeza kwa kazi yake nzauri anayofanya na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo tunaleta miradi mingi Hanang, tunamhakikishia kwamba baada ya kumaliza awamu ya kwanza, basi tutaenda awamu ya pili. Wananchi wa Hanang watapata umeme mzuri kwa ajili ya shughuli zao za maendeleo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe subira tutatekeleza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na kipindi chetu cha maswali, kuna tangazo muhimu.

Mheshimiwa Spika amepokea taarifa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Kiongozi na Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hatakuwepo Dodoma kuanzia tarehe 21 Juni kwa sababu za kikazi. Katika kipindi hicho chote ambacho hatakuwepo, shughuli zote zinazomuhusu kama Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni zitasimamiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 659

**Kukabiliana na Ongezeko la Bei za Pembejeo**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na ongezeko la bei ya pembejeo za kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ili kukabiliana na ongezeko la bei ya pembejeo, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa mazao yote hapa nchini ili kuwapa unafuu wa bei ya mbolea, kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani;

(ii) Kuratibu ununuzi wa pamoja *(Bulk Procurement)* wa pembejeo za mazao ya korosho, pamba na tumbaku kwa kuagiza kutoka kwenye chanzo cha uzalishaji;

(iii) Kuhamasisha kampuni za pembejeo kutumia reli kusafirisha pembejeo kwenda mikoani ili kupunguza gharama za usafirishaji;

(iv) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa pembejeo za kilimo nchini ili kupunguza utegemezi wa kuagiza kutoka nje ya nchi;

(v) Kuainisha na kutangaza bei elekezi za mbegu bora kila mwaka ili kudhibiti upandaji holela wa bei za mbegu; na mwisho

(vi) Kushirikisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu ndani ya nchi kwa kuingia mikataba ya muda mrefu na Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA)* na *TARI* ili kuzalisha mbegu bora kwa kutumia mashamba ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua jitihada na bidii ambayo Serikali inaifanya katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya kilimo. Pia kuna changamoto kubwa sana kwenye upatikanaji wa pembejeo za kilimo hususan mbegu. Kwenye taarifa yenu inaonesha kuna utoshelevu wa 40% tu maana yake hata nusu hatujafika. Sasa nataka kujua mkakati wa Serikali ni upi ili kuhakikisha tunapata mbegu bora na za uhakika ili kuepusha changamoto ambayo wakulima wamekuwa wakikabiliana nayo kila wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu namba mbili, nataka kujua, Serikali mna mpango gani wa kushawishi wawekezaji ili waje kuwekeza ndani ya nchi, viwanda vikubwa vya mbolea ili tupate mbolea kwa bei rahisi na kwa uhakika zaidi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nami naendelea kumwondoa hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya mikakati yetu ni kama ambavyo nimeitaja katika jibu la msingi, lakini tutaendelea kutumia mifumo ya kuagiza ili kupunguza bei kwa wakulima kwa sababu tunaamini kabisa ili tuweze kupata tija, ni lazima tuongeze matumizi ya mbegu bora pamoja na mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo haya yapo katika mkakati na tuamini kwamba tulikotoka na tulipo, tuko sehemu nzuri zaidi na mwelekeo tunakokwenda ni kuzuri zaidi. Tunaamini kwamba jambo hili, itafikia mahali tutakuwa na utoshelevu kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu mpango wa uwekezaji wa kutengeneza viwanda vya mbolea hapa nchini, hilo lipo katika mipango ya Serikali. Sasa hivi tunafanya mazungumzo na wawekezaji kupitia Balozi zetu kama ambavyo kule Ubalozi wa Qatar wanahangaika na watu wa *Qatar Energy* ili waweze kutusaidia kuzalisha mbolea hapa nchini. Katika hatua za awali, waweze kutuletea mbolea ambayo sasa tutaanza kuitumia kabla ya kuwekeza katika viwanda. kwa hiyo hii ni mipango ya Serikali ambayo tupo nayo, kwa hiyo tuna mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu na yote ipo katika mchakato wa kukamilika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, nataka tu kutoa *clarification* kidogo kwenye eneo la mbolea. Mmepitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo juzi, kwenye bajeti kuna fedha zilitengwa kwa ajili ya *TFC*. Pamoja na uwekezaki unaoendelea hapa wa *ITRACOM*, *expansion* ya Minjingu, lakini Serikali kupitia Kampuni yake ya *TFC*, inaanza kujenga kiwanda cha *blending* kikubwa cha tani 300,000 na tunaanza kukijenga Mkoani Pwani. Ilikuwa *dream* ya nchi kwa muda mrefu, tunaanza mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima wa pamba anapouza pamba yake anakatwa shilingi 300 kwa kila kilo na kulipa kwa ajili ya pembejeo kwa Bodi ya Pamba bila kuangalia matumizi ya pembejeo ambayo inalingana na kile kiasi anachokatwa. Je, kwa kuwa mfumo huu unasababisha bei ya pamba kuwa chini, Serikali haioni haja ya kutafuta mfumo mwingine wa kumkata mkulima ili akatwe kulingana na kile alichokitumia *(pay as you use)*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani umemwelewa. Samahani, nadhani Mheshimiwa Waziri Hussein Bashe ana majibu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ugharamiaji pamba, gharama ya shilingi 300 inawekwa katika mfumo wa mjengeko bei ambapo tunatazama gharama zote za uzalishaji, lakini gharama hizi za shilingi 300 tunazipunguza kutokana na *profit margin* ya mnunuzi kwa sababu tunaangalia *future market*, tunaangalia price ya *export* na *exchange difference* ya *price*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *profit* anayoipata kutokana na *exchange rate*, tunaipunguza pale ili irudi kumhudumia mkulima. Mifumo hiyo mingine yote mfano huo wa ulipe kutokana na mahitaji, toka miaka ya 1990, ni mifumo ambayo imejaribiwa na imeshindikana. Mfumo sahihi ambao tunaamini kama Serikali ni mfumo huu wa mnunuzi kukatwa shilingi 300 na baada ya hapo mnunuzi anaweka kwenye mfuko, mkulima anapewa pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya pamba hivi karibuni ilianza na shilingi elfu moja na mia moja leo ipo shilingi 1,300 na minada inaendelea na mkulima bei anayoipata mnadani hakatwi hata shilingi 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia swali linalofuata, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero sasa aulize swali lake.

Na. 660

**Hitaji la Kilimo cha Umwagiliaji – Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza:-

Je, kati ya mwaka 2021 – 2022 Serikali ilianzisha miradi mingapi mipya ya umwagiliaji ili kukuza kilimo cha mpunga katika Jimbo la Kilombero?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kilombero ni miongoni mwa Majimbo ambayo yana maeneo makubwa yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji hii ikijumuisha bonde la Kilombero lenyewe pamoja na skimu ya Msolwa Ujamaa ambayo imefanyiwa ukarabati na kukamilika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeingia Mkataba na Mshauri Elekezi *Saba Engineering PLC* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika bonde la Kilombero ili kujua gharama halisi za kujenga miundombinu ya umwagiliaji kabla ya kuingizwa katika mpango wa ujenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nashukuru majibu ya Serikali na huyo Mkandarasi ambaye Mheshimiwa Waziri alinikabidhi alisema pia atafanya *study* ya namna gani ya kupunguza mafuriko katika Mto Lumemo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, Serikali imetujengea mradi wa umwagiliaji Mkula, Kata ya Mkula na Godauni la Kata ya Mkula zaidi ya miaka miwili sasa godauni hilo halijakamilika kwa sababu Mkandarasi hajalipwa pesa zake. Je, ni lini Serikali itamlipa Mkandarasi huyu ili akabidhi godauni kwa wananchini? *(Makofi)*

Swali la pili, juzi nikiwa ziara Jimboni nimezungumza na wakulima wa miwa, mpunga, wabeba mizigo, wenye mashine za kukoboa, makuli wanaomba sana kuzungumza na Mheshimiwa

Waziri Bashe, wanampenda sana. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri Bashe atafanya ziara Jimbo la Kilombero Halmashauri ya Mji wa Ifakara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hilo swali la pili nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri hawezi kujibu, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kwamba, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero kwamba mkandarasi ambaye anatengeneza ile *Scheme* ya Mkula pamoja na godauni lake ni kwamba tumepata zile *document* zake kwa ajili ya malipo na zimeishatufikia, kwa hiyo kinachofanyika sasa hivi tu ni mchakato, tumeishazipeleka Wizara ya Fedha wapo katika hatua za mwisho, wakishamaliza maana yake atalipwa ili aweze kumalizia ule mradi na kukabidhi kwa wananchi. Kwa hiyo, jambo hili Mheshimiwa Mbunge tunalifahamu na tunalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Waziri kufika amesikia, akishindwa kufika yeye mimi mwenyewe nitafika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, nikushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge uliyoyajibu kwa niaba ya Serikali.

Sasa tunahamia Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 661

**Reli ya Mwendokasi kutoka Mtwara-Mbamba Bay**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga reli ya mwendokasi ya kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Uchukuzi, Mheshimiwa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* imekamilisha kazi ya upembuzi na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli ya Mtwara - Mbamba Bay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma yenye kilometa 1000. Aidha kwa sasa Serikali inaendelea na utafutaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kiasi cha shilingi 702,625,000 kimetegwa kwa ajili ya kumwajiri mshauri elekezi *(transaction advisor)* atakayekuwa na jukumu la kuandaa andiko, makabrasha ya zabuni na kutusaidia kumpata mwekezaji kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi *(PPP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumuomba Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, pamoja na wananchi wa Mtwara, Ruvuma na Lindi na Mikoa ya Kusini na Watanzania kuwa na subira wakati Serikali inaendelea kukamilisha maandalizi ya kuanza ujenzi wa njia hii kwa kiwango cha *Standard Gauge*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Je, Serikali inajua faida zitakazopatikana kutokana na ujenzi wa njia ya reli ya mwendokasi kutoka Mtwara kwenda Mbamba *Bay* Wilayani Nyasa? *(Makofi)*

(b) Je, ni kwa nini Serikali inachelewesha kuanza ujenzi wa njia ya reli ya mwendokasi kutoka Mtwara kwenda Mbamba *Bay? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, kwanza nianze kumshukuru Mheshimiwa Msongozi kwa sababu yeye pamoja na Wabunge wengi ambao nina uhakika watasimama tu kwa ajili ya kuhoji swali hili, wamekuwa wakihitaji kwa muda mrefu kuona *SGR* inajengwa kutoka upande wa *Southern Corridor* na Serikali inafahamu umuhimu wa jambo hili. Unapozungumza *SGR* ya Kusini lazima ufungamanishe Liganga na Mchuchuma pamoja na Bandari. Nini Serikali imefanya mpaka sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza tumekwishalipa fidia mwaka jana wananchi 1,142 takribani shilingi bilioni 15.4. Hii ni *commitment* ya juu kabisa ya kuona jinsi ambavyo tunataka jambo hili likamilike mapema iwezekanavyo. Hatua ya pili tumekwishaanza ujenzi wa bandari ya Mbamba Bay na hivi ninavyozungumza tupo hatua za mwishoni kuanza kujenga Bandari ya Kisiwa Mgao – Mtwara. Kwa sababu unapozungumza reli hiyo lazima uzungumzie namna ya kusafirisha chuma pamoja na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya tatu tunaboresha viwanja vya ndege kuanzia Njombe ambayo tupo kwenye usanifu wa kina lakini Mtwara pamoja na Lindi ambayo tunajenga pia kingine kipya. Kama nilivyosema hata katika bajeti hii tumetenga takribani milioni 702 yote hiyo ni kuelekea kuhakikisha kwamba tunafanya jambo hilo linakamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatua nyingine ambayo tunaifanya tunapojenga Reli ya *SGR* kutoka Dar es Salaam - Mwanza mpaka Kigoma takribani kilometa 2,102 hiyo ni kuonesha utayari wa Serikali katika kujenga Reli ya *SGR* Kusini. Kwa sababu unaanza hatua ya kwanza unamaliza hatua ya pili halafu unakwenda hatua zingine ambazo zinafuatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza tayari tumejenga 2,102 reli kwa maana kama nchi na inakuwa ni nchi ya tano. Kwa hiyo, tukijenga na kilometa 1,000 na *Mtwara Corridor* 1,000 tutakuwa na 3,000 kama na mia tatu au na mia nne. Hivyo, tutakuwa ni nchi ya tatu duniani kwa kujenga reli ndefu zaidi na kwa nchi ya kwanza kwa nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida zake kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge. Tuna faida nyingi ambazo tunazipata tukifanikiwa kujenga Reli ya Kusini kama nilivyosema Reli ya Kusini inafungamanishwa pamoja na Liganga na Mchuchuma ambayo Liganga na Mchumchuma tuna madini ya *Vanadian*, takribani pengine asilimia 0.4 kila mzigo unaopata pale ndani. Tuna *vanadian* na *titanian* ambayo inatengenezea *engine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili inatusaidia kwenda kupata umeme *megawatt* 600 ambayo takribani 250 inakwenda kuyeyusha chuma na 350 inakwenda kuingia kwenye Gridi ya Taifa, nchi yetu ina changamoto ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi reli hii itatusaidia sasa kuchukua malighafi zile zote kwa maana ya Mchuchuma yale makaa ya mawe kusafirisha, kuyatoa pale yale yalipo kuyapeleka duniani yanapohitajika kwa wingi zaidi sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo taifa letu litapata fedha nyingi zaidi. Kama haitoshi pia itatuwezesha kufungamanisha nchi yetu kwenye viwanda, takribani milioni 2.9 ya chuma tutazalisha kwa mwaka wakati sisi mahitaji yetu tunakalibia milioni moja. Hivyo, basi niendelee kumuomba Mheshimiwa Mbunge, nafahamu yeye ni mkulima na angependa kujua faida kubwa ambazo zinapatikana kusafirisha mazao mbalimbali kwenye ukanda wa Kusini kupeleka nchi jirani na nchi za mbali kupitia reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kumuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali inakamilisha mchakato huu na hatimaye tutaenda kuanza ujenzi huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kabla sijakukaribisha Mheshimiwa Mariam Kisangi, Waheshimiwa Wabunge wale ambao tunafuta ushauri wa mambo mbalimbali kwa viongozi mbalimbali tufanye hivyo kwa utulivu sana ili kuwezesha Naibu Mawaziri, Serikali inapojibu kwa Wabunge majibu hayo yaweze kusikika. Tafadhali wale wote ambao tunatafuta ushauri kutoka kwa viongozi ambao wapo ndani ya Bunge tufanye kwa utulivu mkubwa ahsante sana, Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiboresha treni ya Gerezani mpaka Pugu ambayo inajulikana kwa jina la treni ya Mwakyembe kwa kuweka kituo chenye uwakika maeneo ya Pugu pale pale wanapomalizia safari inasimama kwa dakika tano, jambo ambalo linawafanya watu washindwe hata kuteremka kwa vizuri. Pia kuweka vituo katika eneo la Gongolamboto, Ukonga, Kipawa, Vituka, Kiwalani pamoja na Yombo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwelekeza Mkurugenzi wa *TRC* kufanya tathimini juu ya ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge na hatimaye kuweza kuboresha huduma hiyo ili wananchi waweze kunufaika kama ilivyoombwa na Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, wananchi wengine wa Jimbo la Nyasa ikiwemo watoto wetu na wajukuu wanaishi Dar es Salaam. Hivi karibuni tuliona kwenye vyombo vya habari ile treni ya Mwakyembe ikiwa imejaza kwa kiwango kikubwa sana watoto, kiasi cha kukosa sehemu za wao kuwemo mle kwenye treni kwa utulivu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mabehewa maalum kwa ajili ya hao watoto wakiwemo wenzao ili kuhakikisha usalama wao unakuwa mzuri zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza kuchukuliwa kama ni sehemu ya ushauri, lakini tumekuwa tukisema hapa Bungeni jinsi Serikali ya Awamu ya Sita ilivyojipanga katika kuboresha mfumo wa reli kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kupitia *TAZARA* kama nilivyosema hapo kwa ujumla miundombinu yake ni mibovu na vitendea kazi ni vibovu, kwa hiyo Serikali Maraisi watatu wamekubaliana, wapo kwenye mazungumzo ili tuboreshe njia nzima kutoka Dar es Salaam mpaka Kapiri Mposhi – Zambia takribani ni kilometa 1,860.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kupitia maboresho hayo tutapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ili iende sambamba na kuboresha treni zetu. Amezungumza treni ya Mwakyembe kuna ile ya Udzungwa na zingine zote kwa lengo la kuboresha usafiri hasa kwa vijana wetu ambao ni wanafunzi kama alivyokuwa ameshauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa niaba ya Serikali umejibu vizuri maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Nina mkaribisha Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka aulize swali lake.

Na. 662

**Halmashauri ya Liwale Kurejeshewa Fedha za Miradi ya Kimkakati**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itairejeshea Halmashauri ya Liwale fedha za miradi ya kimkakati iliyorudishwa Hazina ili iweze kujenga stendi ya Kisasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mjaibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa stendi ya kisasa ya Liwale ni moja kati ya miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato kwa Halmashauri ambapo Serikali iliingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Liwale Mkoani Lindi kwa gharama ya shilingi bilioni 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2024 kiasi cha shilingi milioni 452.8 kimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo ambapo fedha hizi zimetolewa kulingana na madai yaliyowasilishwa kulingana na mpango kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha 2024/2025, kiasi cha shilingi milioni 412.8 kimetengwa kwa ajili ya mradi huo. Aidha, kwa shughuli ambazo hazikutekelezwa kulingana na mkataba kutokana na sababu mbalimbali, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale inaelekezwa kutenga bajeti ya kugharamia shughuli hizo. Azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa mradi wa stendi ya kisasa ya Liwale unatekelezwa kulingana na mkataba ulivyopangwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotia matumaini, lakini kwa sababu ya mradi huu ni wa muda mrefu sana, una zaidi ya miaka sita sasa, umekumbwa na misukosuko mingi sana. Sasa naomba kupata kauli ya Serikali nini uwezo wao wa kusukuma mradi huu mwaka huu ukaanza kwa sababu tu umechelewa sana na wanaliwale wanauhitaji sana.

Swali la pili sambamba na mradi huu wa Stendi ya Kisasa, Liwale tulikuwa na shida kubwa sana ya kuwa na soko la kisasa, iliandikwa miradi hii yote miwili sambamba. Je, Serikali iko tayari sasa kutupatia fedha na mradi huu wa soko la kisasa ukaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kabla ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kuchauka nimpongeze sana kwa namna anavyofuatilia miradi hii hasa huu wa stendi ya kisasa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza kama nilivyozungumza au kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba tayari fedha imetengwa milioni 412 ya mwaka ujao wa fedha 2024/2025, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi ule hautasimama utaendelea kujengwa kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira katika soko ila nimhakikishie tu kwamba ndani ya bajeti ya mwaka huu soko lile limetengewa fedha na Serikali ipo tayari kwa ujenzi wa soko hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumehitimisha idadi ya maswali ambayo tulikuwanayo kwa leo, tulikuwa na maelekezo ya Mheshimiwa Spika kuhusiana na wale ambao tunatafuta ushauri kwa Waheshimiwa Mawaziri akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu, tuhakikishe kwamba hatutumii zaidi ya dakika tano ili kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge wengine kupata fursa ya kukutana na viongozi, kwa sababu wakati mwingine ni fursa pekee ya kuweza kukutana nao kwa masuala ya Majimboni mwetu. Kwa hiyo, tujitahidi kutumia muda mfupi inavyowezekana ili kuacha fursa kwa Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wana mahitaji hayo hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunayo matangazo mengine, tunayo matangazo ya wageni walipo Bungeni.

Kwanza, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 59 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Kata ya Msimbu iliyopo Kisarawe Mkoa wa Pwani, karibuni sana. Hawa kwa lugha maarufu tunaita Wajumbe, karibuni sana Wajumbe. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao wageni Sita wa Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi ambao ni wasaidizi wake kutoka Ofisi ya Mbunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni familia yake kutoka Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 12 wa Waheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Jonas Mbunda Mbunge na Mheshimiwa Benaya Kapinga Mbunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa na Sekretarieti ya Wilaya ya Mbinga Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, ambao ni wanachama wa Tawi la Simba Mjengoni kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Rose Busiga Mbunge ambao ni Wahadhiri kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Kampasi ya Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mbunge Ng'wasi Damas Kamani, ambaye ni rafiki yake waliosoma wote *St. Augustine* University *(SAUT)* Kozi ya Sheria, mwaka 2012 – 2016, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mbunge Antipas Zeno Mgungusi ambao ni waandaaji wa *Tanga City Marathon*, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Mbunge Aziza Ally, ambao ni wajasiriamali kutoka Wilaya ya Igunga Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Mbunge Selemani Moshi Kakoso, ambao ni Viongozi wa Kata, Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Tanganyika Jimbo la Mpanda Vijijini, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wageni watano ambao ni Watanzania wanaoishi Atlanta nchini Marekani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 73 na walimu 13 wa Shule ya Msingi Notre Dame ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 51 na walimu saba wa *Great Vision Nursery and Primary School* kutoka Mbagala Jijini Dar es Salaam. Wako wapi? Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 58 na walimu watano kutoka Shule ya Awali na Msingi *Prestige* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 21 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi Ilboru *Lutheran* ya Jijini Arusha, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 60 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari *Peace House* ya Jijini Arusha. Kama wameingia karibuni, wengine nadhani wapo huku, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Hoja za Serikali. Hoja ambayo ililetwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na Hoja ambayo ililetwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa ruzuku ya uhai na afya ambayo imetuwezesha kukutana tena leo asubuhi hii. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuiendeleza nchi yetu, ambayo bajeti hii itakuwa na msukumo mkubwa zaidi katika kuleta maendeleo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wote wa Wizara ya Fedha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Katibu Mkuu na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Bwana Lawrence Mafuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nijikite katika mambo ambayo, zaidi yatagusa upande wa mipango. Nakubaliana na wale wote waliozungumza kwamba mipango ndio moyo na nguzo ya Taifa letu. Nakubaliana kabisa na nukuu ya Mheshimiwa Waziri *Professor* Kitila Mkumbo kutoka kwa Mheshimiwa Hayati Benjamin Mkapa kuhusu umuhimu wa mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, miongongi mwa mambo ambayo aliyasema mara kwa mara, alisema; “kupanga ni kuchagua.” Kwa hiyo, tunachokipanga tuchague kile ambacho kitasukuma maendeleo ya nchi yetu na watu wake ikiwa ni pamoja na maslahi yao pia matilaba *(aspirations)* zao. Hawa Watanzania wana-*aspire* nini na wana matilaba gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande huo ningependa nizungumzie suala moja muhimu ambalo Taifa hili hatuna budi kuliwekea umuhimu mkubwa na kuwekeza fedha nyingi tunavyoweza, kwa sababu sasa tunawekeza fedha kidogo katika eneo hilo, nalo ni eneo la *Research and Development* (Utafiti na Maendeleo). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali huko nyuma kuona umuhimu wa utafiti na maendeleo, ilianzisha Shirika la *TIRDO* ili liwe ndio Shirika la kuchochea *research and development* (utafiti na maendeleo) kwa upande wa viwanda. Ikaanzisha kiwanda cha *CAMARTEC* kule Arusha iwe ndio chombo cha utafiti na utengenezaji wa bidhaa kwa ajili ya kuboresha kilimo chetu. Pia ilianzisha taasisi mbalimbali za utafiti; *TAWIRI* kwa ajili ya wanyamapori, *TAFIRI* kwa ajili ya uvuvi, *TAFORI* kwa ajili ya misitu, *NIMR* kwa ajili ya madawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la utafiti ni lazima sasa tuliwekee kipaumbele. Tusipofanya hivyo tutakuwa hatucheleweshi maendeleo ya sasa tu, lakini tutakuwa tunadumaza na kufubaza maendeleo ya miaka ijayo. Taifa hili halina budi sasa kuanza kuwekeza kwa maendeleo makubwa ya miaka 50 au 60 ijayo na kufanya hivyo, moja, ni kuimarisha vituo hivi vya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuiboresha *TIRDO* ifanye *research* katika *industrial research organization* na haya yote tulijifunza kutoka India. *National Planning Commission* tulijifunza kutoka India, *TIRDO* tulijifunza kutoka India, *NEMC* tulijifunza kutoka India na *COSTECH* tulijifunza kutoka India. Tufanye tathmini, tujue hayo

mafunzo tuliyoyatoa huko huku kumekuwa na upungufu gani ili tuyaimarishe na tujiimarishe katika *research. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuimarishe *research* katika vyuo vyetu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilikuwa na taasisi nzuri sana ambayo nashangaa na mimi ni mmoja wao, kwa nini baadaye tuliibadili? Ilikuwa inaitwa *Institute of Production Innovation* (Taasisi ya Ubunifu katika Uzalishaji) baadaye tukaibadili na Profesa Schoeman kutoka Ujerumani akahamia Namibia. Leo Namibia ndio wenye *Institute of Production Innovation* bora zaidi katika Bara la Afrika, wakati wazo lilitoka kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa vyuo vikuu vyetu viimarishwe katika eneo hili la *RnD,* ili viweze kushiriki katika kufanya utafiti utakaotufaa katika miaka ijayo. Pia sasa tuwekeze katika maeneo mengine ya utafiti na eneo moja ambalo napendekeza tuweke katika utafiti ni *Space Science* na *Space Economy* (Uchumi wa Anga na Sayansi ya Anga). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili sizungumzii jambo la kubuni. Tayari pale Chuo cha *St. Joseph University of Tanzania* wanayo *St. Joseph University of Tanzania Satellite Development Team,* ambayo inaongozwa na Dkt. Amani Bura, kijana Mtanzania ambaye amesoma India na China na sasa wametengeneza *satellite* ambayo ina uwezo wa kukusanya *data* na taarifa kuhusu mazao na mabadiliko ya tabianchi. Sasa hivi wanahangaika kupata shirika litakaloweza kurusha hiyo *satellite* yao kwenda angani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa wakizungumza na Shirika la India na Urusi. Nadhani jambo hili sasa Serikali ingelichukua liwe lake, ili kuhakikisha *satellite* hiyo inarushwa ambayo imetengenezwa na Watanzania chini ya Mtanzania Dkt. Amani Bura, kijana ambaye ni mbunifu na amekwenda katika jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru *COSTECH* ambayo ilitoa shilingi milioni 40 kwa mradi huo. Sasa miradi ya aina hiyo iwe mingi na huu wa *St. Joseph University of Tanzania* wa *satellite*

uimarishwe na hawa vijana wapewe moyo na ikiwezekana watambuliwe kwamba, wamefanya jambo ambalo watu tulidhani ni suala la ndoto. Wakati Profesa Henry Mgombelo na Dkt. Mnenei wakizungumzia mambo haya miaka ya 1980, tulidhani ni ndoto lakini leo Dkt. Amani Bura na wenzake wameliwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile twende mbali zaidi tuongee na China, India na Urusi waje wajenge *launching pad* hapa ya kurusha *rockets* za kupeleka *satellite* angani. Sisi Tanzania tuna maeneo ambayo wanaweza kujenga *launching pad* ya *rocket* za kupeleka *satellite*. Inaweza kuwa Mafia, Kilwa na mahali popote pale. Jambo hili tulifanye haraka. Sisi shida yetu wakati mwingine tunakwenda goigoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuongee na India, China na Urusi, ili Tanzania katika Bara la Afrika sisi ndio tuwe na mitambo ya kurusha *rockets* za kupeleka *satellite* angani na ukichukua sisi tupo karibu na Ukanda wa Ikweta na tuna anga ambalo ni angavu kwa muda mrefu na hali ya hewa ambayo haina matatizo ya mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo jambo lingine ambalo ningependa kulichangia. Ukurasa wa 45 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi inazungumzia kuanzisha kilimo cha mimea dawa kitakachotoa malighafi kwa ajili ya kiwanda cha kuzalisha dawa zitokanazo na mimeadawa. Ukurasa wa 139 unazungumzia kuanzisha kituo kikubwa cha utafiti na uchunguzi wa mimeadawa na kuanzisha kiwanda cha kimkakati cha kuzalisha dawa zitokanazo na mimea yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wiki mbili nilikuwa nimealikwa nchini China na Chama cha Kikomunisti cha China kwa ziara ya wiki mbili ya wataalamu kutoka katika *think tanks,* wataalamu 27 kutoka nchi 23; katika hizo tatu ni za Afrika. Wachina walinipa heshima mimi kuwa ndio kiongozi wa wabobezi hao wote kutoka duniani katika ziara hiyo. Tumetembelea maeneo mbalimbali tumeona wanavyopanga China miaka 50 ijayo ambavyo maisha

ya watu yatakuwa bora. Moja ya mambo ambayo wamewekeza ni utengenezaji wa dawa kutokana na mimeadawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadam Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeeleza hilo, mimi ningeihimiza Serikali sasa; nililisema hili katika Bunge hili na narudia tena twende India na sasa twende China kile kiwanda kina zaidi ya umri wa miaka 300 kikitengeneza dawa mbalimbali za mimeadawa. Hili limo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, tusisite kwenda kule. Wenzetu China wamekwishafika katika eneo la Mwezi ambalo dunia hatuioni toka Mungu aumbe, lakini bado hawajadharau mimeadawa yao, bado hawajadharau maarifa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependekeza kabisa Serikali, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango tulichukue hili jambo kwa uzito mkubwa (ukurasa wa 45 na 139 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi) ili tuweze kulitekeleza na kuliendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa hapa nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa jielekeze kuhitimisha, dakika 10 zimekwisha. Ninakuongezea dakika tano.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninahitimisha kwa kusema kwamba, Serikali ichague mikoa ambayo itakuwa *engine* ya kusukuma uchumi wa nchi hii. Hivyo ndivyo wamefanya Wachina kwa Jimbo la Jiangsu na Fujian. Sisi hapa Tanzania Mkoa ambao unaweza kuwa ndio Mkoa wa kusukuma uchumi wa nchi hii ni Mkoa wa Morogoro. Jambo hilo walilitambua Wajerumani, Waingereza na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Tuwekeze katika Mkoa wa Morogoro katika nishati ya maji mabwawa yote matatu, Kihansi, Kidatu na Mwalimu Nyerere yapo Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Morogoro ina kila aina ya ambayo inaweza kusukuma uchumi wa nchi hii. Pia katika Mkoa wa Morogoro wilaya ya kuwekeza zaidi ni Wilaya ya Kilosa, kwa sababu ndio Wilaya unganishi ya reli tatu; Reli ya *SGR, TAZARA* na

Kati. Pia, ukichukua ile *triangle* ya Kimamba – Kilosa – Ilonga ndipo kwenye utafiti mkubwa wa kilimo. Tukiwekeza katika Wilaya ya Kilosa kujenga reli mpya kutoka Dumila kwenda Mkata *Station* na kuigeuza Mkata *Station* kuwa ndio kituo kikubwa cha machinjio ya ng'ombe ili nyama hiyo iingie katika Reli ya *SGR* kuja Dodoma kwenye Kiwanja cha Msalato kwenda Dar es Salaam kiwanja cha ndege, kwenda nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwekeza na kuchagua mikoa michache miwili au mitatu na kuifanya kuwa ndio *engine locomotives* za kusukuma uchumi wa nchi yetu hii, ninaamini tutapiga hatua kubwa. Mimi nina imani kubwa kabisa na Wizara ya Mipango na Tume ya Mipango na nipo tayari kukaa nao tuangalie jinsi ya kuja na mpangomkakati wa kimaendeleo wa Wilaya ya Kilosa, Jimbo la Kilosa na Mkoa wa Morogoro, ili Mkoa wa Morogoro iwe ndio Jiangsu na Fujian ya Tanzania, ili iweze kupiga hatua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja bajeti hii ipite, ili kazi ya maendeleo chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, atafuatia Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani na Mheshimiwa Mohamed Lujuo.

Mheshimiwa Balozi Liberata, tafadhali.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie kwenye Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa 2024/2025, hoja mbili zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na pacha wangu Mheshimiwa Dkt.

Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha kwa hotuba na wasilisho zuri sana la Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali vinavyotupatia mwanga wa mbele tunapokwenda na kutupatia matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kuunda Wizara ya Mipango inayojitegemea na Wizara ya Fedha maana uzoefu umeonesha kwamba mipango lazima iongoze hazina na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika inafurahisha kuona Mawaziri wetu pamoja na Naibu Mawaziri wakiwa wameketi pamoja kama mapacha katika kuwasilisha Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025. Unaona kabisa kwamba mpango na bajeti vinasomana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nimefurahishwa na mtiririko mzuri wa Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali kuanzia shabaha, malengo, misingi ya bajeti, vipaumbele, ufuatiliaji na tathmini na mafanikio ya Serikali ya Awamu wa Sita na kuimarika kwa sekta za uzalishaji, viwango vya kodi na kadhalika. Katika kusikiliza kwangu na kusoma hotuba zote mbili nimevutiwa na mambo matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu *(people centered development)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimevutiwa na msisitizo wa usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nimevutiwa na maeneo ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/2026 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimevutiwa na msisitizo wa kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma.

Niseme kwamba, Tanzania ya Viwanda inawezekana, tukiamua itawezekana. Nchi yetu imejaaliwa nguzo muhimu za kuwezesha Tanzania kuwa Tanznaia ya Viwanda kama hivyo vilivyosemwa hapa. Tuna jiografia za kimkakati, madini, maji ya kutosha pia tuna nguvukazi ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia diplomasia nzuri ambayo imetufungulia fursa za Masoko ya Ulaya, Asia na Mabara yote. Pia, tuna masoko yanayotuzunguka ambayo tunayamudu kwa hali yetu ya sasa katika Afrika Mashariki na *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu tuna amani na utulivu ambao peke yake ni kigezo muhimu katika maamuzi ya uwekezaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha amelisisitiza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na vyote hivi bado sisi hatujaweza kuwa Tanzania ya Viwanda. Hii maana yake nini? Maana yake kuna kitu kinakosa. Tunakosa ufungamanishaji *(packaging)* wa vitu hivi, ili kuvitafsiri katika matokeo ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maarifa na teknolojia, tunayo mahusiano mazuri na karibu na dunia nzima, tuyatumie kuvuta maarifa hayo na teknolojia hizo nchini. Tutumie fursa ya upepo wa dunia kuelekea kwenye nishati ya kijani, kuvutia viwanda kwa kutumia madini ya kimkakati yaliyopo nchini ambayo kesho ndiyo yatatufikisha katika dunia ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuhusu sekta ya viwanda katika Mkoa wa Kagera; Mkoa wa Kagera unasikitisha kwamba ni mkoa ambao una rasilimali zote, una madini na unaweza ukawa kitivo cha viwanda, lakini mpaka leo tunavyoongea sijui kama kuna kiwanda ambacho wanakiita kama kiwanda. Kwa hiyo, mimi rai yangu kwa Serikali ni kwamba kwa kweli hatuwezi kufika mbali kama hatuupi umuhimu wa sera ya viwanda ambayo inaimarisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kabla hujaniondoa, niseme kwamba ili tufanikishe utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti Kuu ya Serikali, tunahitaji tuwe na mfumo thabiti na endelevu na ufuatiliaji na tathmini *(monitoring and evaluation)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema ataviongezea nguvu vitengo vyote vya ufuatiliaji na tathmini, lakini nikumbushe, huko nyuma Kamati ya Bunge ya Bajeti ilishauri kuwepo sheria na sera maalumu ambazo zimeambatanishwa kuwa ndiyo msingi katika kuhakikisha masuala ya ufuatiliaji na tathmini yanakuwepo katika utekelezaji. Ni vyema ushauri huo ukazingatiwa katika utekelezaji wa bajeti na mpango wetu wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, pia kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni ajiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nimpongeze sana Waziri wa Fedha kwa bajeti hii ambayo ameileta ambayo matumaini yangu kama fedha hizi tutazipitisha, basi Watanzania wanaenda kupata neema ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Wizara ya Fedha, lakini niipongeze na Wizara ya Kilimo kwa kuleta *Finance Bill* ya mabadiliko ya Sheria ile ya Sukari. Taifa hili tumekuwa mateka kwa muda mrefu kwenye sekta ya sukari, kwa zaidi ya miaka 25, miaka 50, tumekuwa mateka kwenye sekta ya sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mawaziri waliotangulia hapa kwenye Wizara ya Kilimo, Wabunge wenzangu waliokuwepo hapa watakubaliana nami, tumekuwa na Mheshimiwa Tizeba hapa, tatizo la sukari limekuwepo kwenye

Taifa hili, bei zikiwa zinapanda na kushuka, tumekuwa na Mheshimiwa Hasunga, tumemekuwa na tatizo la sukari zikiwa zinapanda na kushuka, lakini hata Bunge lako hili Tukufu mwaka huu tunaosema, tumesimama Wabunge hapa tukiwa tunalalamikia bei kubwa ya sukari. Sisi Wabunge tutakuwa watu wa ajabu kwa *Finance Bill* hii inayokuja ya kufanya marekebisho kwenye suala la sukari, tukaja Wabunge tukafarakana wakati tunamtetea mlaji Mtanzania wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu hapa Ramadhani ikiwa inakaribia, tukiwa Bungeni hapa Wabunge wamesimama sukari shilingi 8,000 kwenye majimbo yao. Wakuu wa Mikoa wanasema sukari shilingi 7,000 kwenye mikoa yao. Serikali inahangaika kwenda kufungua ma-*godown* ya watu kwa ajili ya suala la sukari. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, leo itakuwa ni jambo la ajabu na la kusikitisha Serikali inachukua hatua Watanzania wapate sukari kwa bei nafuu, akasimama mjinga mmoja mimi simjui, akatetea jambo la bei inayopanda ya sukari na kuongea vitu visivyoeleweka. (Makofi)* **[Maneno Hayo Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kanuni zinatukataza kutumia neno mjinga, ninaomba uliondoe kwenye *Hansard*.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilisoma Kiswahili na kwa sababu wewe ni mtaalamu wa Kiswahili, daktari wewe, kabla sijaliondoa neno ungenipa fasili sahihi ya neno mjinga ili niweze kuliondoa vizuri na Watanzania wajue tafsiri ya mjinga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ninaomba uketi, ninaomba uketi Mheshimiwa Mbunge. Sekretarieti mtatuandalia kanuni, nitakuruhusu baada ya kanuni kusomwa.

Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanzia pale ambapo Mheshimiwa Bulaya alianza jana ambaye ni Mama Kikokotoo ama amekuwa ni sauti ya watumishi wa umma kwa kipindi kirefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanzia kwenye historia kwa sababu tuko na Waziri wa Mipango na Waziri wa Mipango amesema, moja kati ya utekelezaji wako wa mpango wa mwaka 2021 – 2025 ni kuchochea maendeleo ya watu. Sasa watu tunaowazungumza ni pamoja na watumishi wetu wa umma, watumishi wa sekta binafsi na ni bahati mbaya sana Makatibu Wakuu wetu, wataalamu wanaowasaidia ninyi ndiyo watu ambao tunawazungumzia hapa. Kwa hiyo, kama tunazungumzia maendeleo ya watu na hasa katika eneo hili la mafao ya wastaafu, ni muhimu mkalichukulia kwa uzito mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na historia kwa nini tumefika hapa tulipo, nikirejea Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma ya mwaka 2021/2022, ukurasa wa 23 akizungumzia mkopo wa *PSPF* kwenda Bodi ya Mikopo, kipindi hicho ilikuwa shilingi bilioni 58, akasema; "Serikali kuingilia maamuzi katika Mifuko ya Pensheni ndiyo chanzo cha matatizo ya kifedha ya Mifuko hii." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 58 wa Taarifa hiyo hiyo unasema, "Ukaguzi wa Mifuko uliofanyika *(Actuarial Evaluation)* ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010, ulionesha mambo yafuatayo; "Ilionesha kwamba hali ya Mifuko ni mbaya, ukadiriaji wa thamani ulibaini hasara ya shilingi trilioni 6.487 kwa mwaka unaoishia Juni, 2010." Hatuwezi kwenda mbele bila kuangalia historia ya namna gani Serikali imechangia hili na kwa namna gani lazima mchukue hatua za ziada kuokoa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya mwaka 2012/2013 ilikuwa na maneno sawasawa na maneno ya ripoti niliyotoka kuisoma. Nenda kwenye ripoti ya mwaka 2013/2014; hii ripoti ilipelekea kuundwa kwa Kikosi Kazi Maalumu kilichojumuisha Serikali yenyewe na wataalamu mbalimbali. Tarehe 24 Oktoba, 2014, taarifa iliwasilishwa kwenye Kamati ya *PAC* kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wote walikubaliana nini mwaka 2014; kwamba Deni la Serikali jipya kwa kipindi kile lilikuwa shilingi trilioni 1.875 pamoja na shilingi trilioni 7.1 ambalo ni deni linalodaiwa na *PSSSF* tangu mwaka 1999. Kilitokea nini, watumishi wa umma walikuwa wanachanga fedha ili wakistaafu walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PSSSF* ilivyoanzishwa na sheria zake, zile fedha ambazo watumishi walichanga Serikali mlisema, tunaomba muwalipe hao ambao walikuwa ni watumishi kabla ya mwaka 1999 ambao kimsingi Serikali ilitakiwa ninyi ndiyo muwalipe, mkaomba mfuko ulipe kwa pesa za watu wengine waliochangia mkisema mtarejesha. Mpaka mwaka 2013/2014 Serikali mlikuwa mnadaiwa shilingi trilioni 7.9075, lazima tuangalie *past* ili uweke mipango thabiti ya kwenda kulinda watumishi wetu, 40% mlichokisema *is peanut* kwa sababu ndani yake kuna mambo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya mwaka 2017/2018, *page* 94; deni jipya la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 2.398, hii ni kutoka ile shilingi trilioni moja niliyozungumza. Hii haijumuishi shilingi trilioni 7.1 la *pre 1998*, kwa hiyo, mpaka mwaka 2017/2018 Serikali na *CAG* anasema hivi; "mifuko yote ya hifadhi ina madai makubwa ambayo ni chechefu. Mengi ya madeni ya Serikali na taasisi zake yalikuwa hayajalipwa mpaka tarehe 30 Juni, 2018, zaidi ya 98% ya madeni hayajalipwa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunazungumzia leo kuwa yameiva, kwa hiyo, tunapozungumza haya mambo angalieni wataalamu wenu ambao kutwa, kucha wanakaa na ninyi wanawasaidia, angalieni ma-*Accounting Officers* ambao kutwa, kucha wanakaa wanawasaidia... *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, Taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ninaomba utulie, utakuwa na muda wa kujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpatia taarifa Mheshimiwa Halima Mdee kwamba Deni la Serikali lilikuwa ni shilingi bilioni 731, lakini tayari Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya kuingia madarakani imeshalipa zaidi ya shilingi bilioni 500 katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni ambalo lilikuwa ni la *pre 1998* lilikuwa ni *4.6 trillion* ambalo pia mwaka 2021 Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imelipa kwa *non-cash bond* zaidi ya shilingi trilioni 2.18. Kwa hiyo, niliona nimpatie taarifa hiyo mchangiaji Mheshimiwa Halima Mdee. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ninataka nikusaide kwamba kwanza...

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu Mheshimiwa, sijakuruhusu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, unapokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siwezi kupokea taarifa yake kwa sababu ninataka akasome ripoti ya mwaka 2013/2014. Deni la *pre 1998* lilikuwa shilingi trilioni 7.1, deni pamoja na riba, ninyi mnajua mlichokifanya mkalishusha *from* shilingi trilioni *seven* mkalipeleka shilingi trilioni nne. Mlijifutia riba kwa sababu *you have that mandate, yes, that* shilingi trilioni *four* ambacho nilikuwa ninakuja. Mmelipa shilingi trilioni mbili ya *non-*

*cash bond*; wewe unajua *bonds* zinavyo-*operate,* pesa haipo mfukoni, mnalipwa vile vi-*interests* na ndiyo maana tumesema, mpaka sasa hivi, kwanza hiyo shilingi trilioni tatu mliitoa kimagumashi, hiyo tuachane nayo, hiyo shilingi trilioni nne yenyewe hamjailipa inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha zinaonekana zipo lakini *in reality* hazipo kwa sababu ni *bond*, sijui kama tunaelewana, ninadhani unanielewa kwa sababu na wewe unamiliki *bond*.

Kwa hiyo, tunaomba, hoja zilikuwa nini, baada ya hii mifuko kuvurugwa vurugwa na ripoti ya mwisho ya mwaka 2014 ya kusema mifuko imevurugwa vurugwa, mkaleta sheria, sheria ya kuunganisha mifuko. Tukawaambia hapa mmeleta sheria, kikokotoo, *formula* ile tuiweke kwenye sheria ili maslahi ya watumishi yawe yamelindwa ndani ya sheria. Ndiyo inakuja 540 iliyokuwepo *as against* 580.

Mheshimiwa Jenista alikuwa Waziri hapa, mkang'ang'aniza iende kwenye kanuni, tukasema ikienda kwenye kanuni Waziri atajiamulia ataleta vitu vya hovyo, ikaenda kwenye kanuni vikaja vitu vya hovyo 580. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ilikuwa ni mishahara gani inatumika kupiga mahesabu? Mishahara hii ya mwisho au mishahara *average* ya miaka mitatu? Mkasema kwa kipindi gani? Mkasema mtaweka kwenye kanuni. Mmeweka kwenye kanuni, hivi unaweza ukatafutiwa *average* ya mshahara wa miaka mitatu ili kujua *fate* yako ya baadaye? Hivi ni kweli, *are we human beings*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kweli dhamira ipo na nimesikia juzi mnasema ooh sisi tutalipa, alisema jana Mheshimiwa Ester, mnalipa kwa *mandate* ipi? Yaani ni nani anawapa mamlaka Serikali kulipa? Lipeni cha watu, pelekeni pesa kwenye mifuko, mifuko ijiendeshe watu walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashangaa Serikali haizungumzi, juzi Rais anasema uwekezaji unafanyika kwenye

mifuko isiyoeleweka eleweka, ninakuona mdogo wangu uko Nairobi unazindua kitega uchumi, nani anajenga kitega uchumi? Ndiyo maana Mheshimiwa Profesa Mkumbo, jukumu lako wewe ndiyo maana uko Ofisi ya Rais, wenzako shirikisha mawazo ya *yes,* lakini *you have to coordinate,* lazima Serikali izungumze; siyo leo Rais anazungumza hiki, kesho Msaidizi wa Rais yuko *busy* kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *feasibility study* imefanywa na nani? Imethibitishwa na nani? Kwamba *that investment* ya kujenga ghorofa 22 inaenda kufanyika Nairobi? Ina faida kwa mifuko? Hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme hivi; hii 40% ni cha mtoto kwa sababu 580 iko pale pale ambayo ni mbaya. Muda ambao u-*buy* hii *average* ya mishahara inapatikana ni kipindi kirefu sana ambayo ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leteni sheria hapa Bungeni, tuijadili sheria upya, tuangalie upya maslahi ya hawa wafanyakazi, ndiyo tutasema kweli Serikali mna dhamira. Mnavyotwambia mwaka 2029 maana yake mnatwambia yale yale, Mheshimiwa Dkt. Magufuli aliona kimewaka akasema wanaahirisha mpaka mwaka 2023. Pale katika watu wakaondoka zao, ilivyofika mwaka 2023, Mungu amlaze mahali pema peponi, ukarudi utaratibu wa zamani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifanye mambo kwa sababu tuna mtu anataka kufanya kwa matamanio na utashi wake. Tufanye mambo ambayo yatakuwa na ulinzi, *whoever* atakayekuja *in future*, mtumishi wa umma aangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wakandarasi, ni hivi... *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba na mimi uniongeze tano.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hapana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeniongeza hata moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, muda wako umeisha. Ahsante, tunakushukuru sana, ahsante Mheshimiwa Mdee, tafadhali. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ili kuwa na mwenendo mzuri wa uchangiaji Bungeni na kulinda heshima za wachangiaji wengine na Watanzania wengine ambao wanaweza kuwa na maoni tofauti na ya kwetu, nilimwomba Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani asitishe mchango wake ili niweze kumpa nafasi baadaye kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Katani ametumia neno mjinga akieleza kwamba wale ambao wana maoni tofauti na yale ambayo anayaeleza ni wajinga.

Waheshimiwa Wabunge, nimefuatilia mijadala ya Waheshimiwa Wabunge na mijadala ya nje ya Bunge, wapo wenye maoni yanayotofautiana na anayotoa Mheshimiwa Katani ambao pia ni Wabunge na wameyasema na yapo kwenye *Hansard* za Bunge. Nikiruhusu neno hili, maana yake nitakubaliana kwamba Wabunge waliokuwa na maoni tofauti na ya Mheshimiwa Mbunge Katani ni wajinga.

Waheshimiwa Wabunge, alinitaka nichukue tafsiri ya neno mjinga na nimechukua tafsiri ya Kamusi Kuu ya Kiswahili. Imetafsiri neno 'mjinga' kama "mtu asiye na uelewa wa jambo fulani" lakini neno mbadala la neno 'mjinga' ni "mbumbumbu, baradhuli" na ni neno ambalo ni kinyume cha neno "mwerevu," kinyume cha neno "mwelewa." *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge tunaongozwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, mwaka 2023. Kanuni ya 71(h) na (j), kwanza naanza na (i) inasema; "Mbunge hatatoa lugha ya matusi au ishara inayoashiria matusi au kumsemea vibaya

Mbunge au mtu mwingine" na (j) "Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine."

Waheshimiwa Wabunge, kwa tafsiri niliyoisoma kwenye Kamusi Kuu ya Kiswahili, neno mjinga linadhalilisha watu wengine. Naomba nimualike Mheshimiwa Mbunge afute kauli yake, ili aendelee na mchango wake. Karibu Mheshimiwa Katani. *(Makofi)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta kauli ya neno mjinga. Naliondoa kabisa kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, endelea.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa namaanisha kwenye mchango wangu ni Serikali inapofanya *intervention* sukari inapouzwa shilingi 6,000, sukari inapouzwa shilingi 7,000, sukari inauzwa shilingi 5,000, Serikali ikaingilia kati ku-*rescue situation,* kwa ajili ya wananchi wa Tanzania wapate sukari kwa bei nafuu. Akapatikana mtu akataka kutetea watu ambao kwenye Taifa hili ndiyo wanafanya hizo *cartel* ambazo, wengine tunao ushahidi, tunaweza kukupa ushahidi ukiutaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nikupe mfano mmoja. Sukari inayouzwa kwenye Taifa hili mkulima wa miwa anayelima miwa Kagera, mkulima wa miwa anayelima miwa Kilombero, mimi ni Mmakonde, Wamakonde sisi kazi yetu ni wamachinga, tunatembea tembea; bei ya tani moja ya miwa Kilombero na Kagera ni tofauti, lakini bei ya sukari ni ile ile wanayoifanya. Leo inakuja Sheria hapa inataka kufanya mabadiliko, jiulize, ukanda huu wakala wa kuuza sukari yupo mmoja, yupo Dodoma hapa, Mkoa wa Manyara hakuna wakala wa sukari pale, pana jambo gani hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kwenye Taifa hili watu saba waweze ku-*drive* Watanzania milioni 61. Haiwezekani, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, mimi nawapa *comfort,* Watanzania wana akili wanaona dhamira ya

Serikali ya Dkt. Samia, wanaona kinachofanywa na Serikali. Isingewezekana kwa miaka yote tumekaa Bungeni hapa kila mwaka sukari inapanda bei Serikali ikae kimya, ikichukua hatua basi kunakuwa na maneno chungunzima, nawaomba waandishi wetu wa habari wakati unaandika habari, muandishi mzuri wa habari, lazima a-*balance story*. Yapo magazeti yameandika habari *page* nne, sijaona *balance* ya *story* ya upande wa Serikali wanasema nini, lakini wameweka taarifa kwenye magazeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Bunge una namna ya kutuongoza. Kipindi kilichopita wapo watu waliandika taarifa ambazo hazikuwa na ukweli na Bunge lilichukua hatua kuwaita na kuwahoji, ili kujua ukweli wa kile kitu na kwenye hili linaloendelea, magazeti kuandika habari ambazo hawajafanya *due diligence* ya upande wa pili na wenyewe ikiwezekana waitwe wahojiwe tupate ukweli. Hatutaweza kukubali kuendelea watu saba, yaani ni sawa na umechukua ng'ombe wako, halafu mkia sasa ndiyo unaongoza ng'ombe. Yaani watu saba wenye viwanda saba, wao nim kia, sasa ndio wanataka waendeshe watu milioni 61 Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili haliwezekani na Waheshimiwa Wabunge wenzangu Bunge hili tulilonalo ambalo hatujamaliza, wote hapa tumelalamika bei ya sukari. Inapokuja *finance bill* leo twendeni tukaiunge mkono Serikali tufanye mabadiliko kwenye sekta ya sukari tutakuwa na *stability* kwenye bei zetu za sukari hapa. *Otherwise* kila mwaka tutakuwa tunakaa, ikikaribia Ramadhani sukari inakuwa shilingi 7,000, ukikaribia sijui muda gani sukari shilingi 8,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeenda *deep* sana kwenye mambo haya yanayoendelea ya sukari, hao waliopewa vibali hawajaagiza sukari, vibali vyenyewe wameviuza kwa hiyo, wana migogoro wenyewe, migogoro mingine inakuja ndani. Mimi nawaomba wabunge wenzangu kama njaa zetu zitatoka tumboni zikahamia kichwani, hili Bunge litakuwa la ajabu. Kama njaa zetu zitatoka tumboni kuhamia kichwani hili Bunge litakuwa la ajabu sana, tutashindwa kufikiri kwa kichwa. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, lugha ya staha ni kitu ambacho ni muhimu sana na hasa kwa, siyo tu Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa mtu mwingine yeyote. Kusema njaa zitatoka kichwani zinaenda tumboni au tumboni kwenda kichwani, hiki kitu hakijakaa sawasawa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Mheshimiwa mchangiaji atumie lugha nyingine kuliko hii anayotumia kwa Waheshimiwa Wabunge, ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nimefuatilia hoja ya Mheshimiwa Katani, ametumia lugha ya sanaa. Nadhani kwa mamlaka niliyonayo namruhusu aendelee. *(Makofi)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kukupongeza na unanipa matumaini makubwa kwamba *Ph.D* yako haikuwa ya kuungaunga. Kiswahili sanifu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa namaanisha ni kwenye Bunge hili tuwe tunayatafakari yale tunayoyalilia na pale Serikali inapochukua hatua, kwa ajili ya kumlinda Mtanzania wa kawaida aliyepo Tandahimba, Mtanzania wa kawaida aliyepo Madaba, Mtanzania wa kawaida aliyepo Kiteto, Mtanzania wa kawaida aliyepo Longido, Wabunge tunapaswa kusimama pamoja kuitetea Serikali yetu. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, yapo mambo ya msingi yanafanywa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye mabadiliko haya ya Sheria ya Sukari, *Finance Bill* inayokuja miongoni mwa dhamira zake ni kwenda kumlinda mlaji wa sukari wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa wazi inawatetea sana hawa waendeshaji wenye viwanda vya sukari. Wanapewa

maeneo, wanapewa na *incentive* huko, lakini hawasemi, ni miongoni mwa mabadiliko ambayo Serikali inaendelea kuwatetea watu wenye viwanda. Nachelea kusema uweke watu wako vizuri, haya yanayoendelea mimi najua wapo watu wenye fedha wanazunguka huko nje wanakutana na baadhi ya wabunge kutaka kukwamisha dhamira njema ya Serikali. Ukienda kwenye Hoteli ya Esperanza pale nimekuta watu wanajadili kufanya *sabotage* ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Wabunge wenzetu. Sasa tunapotetea Watanzania ndipo pale...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, namuunga mkono mchangiaji, *uncle* wangu Mheshimiwa Katani, anachangia vizuri sana, lakini Bunge hili lipo *live*. Suala hili la sukari limegusa Watanzania wengi sana na watu wanafuatilia Bunge kuhusu huu mjadala. Kwa kuwa, Mheshimiwa Katani, mjomba wangu, amewaona hotelini Wabunge wenzetu wanajadili kufanya *sabotage,* hili suala tungemuomba Mheshimiwa atusaidie kututajia kwa sababu, hawa ni kama wahaini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, unapokea Taarifa ya Mheshimiwa Kasheku Musukuma?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea na nachangia kwa tahadhari kwa sababu jambo hili ndiyo maana unaona nazungumza mambo yale ya Kitaifa, tunasubiri mamlaka nyingine zitakapomaliza tutakapotakiwa kutajana, tutatajana wakati ukifika. Kwa hiyo, mjomba wangu usiwe na shaka, tutatajana tu hapa ndani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, muda wako umekwisha lakini. *(Kicheko)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ninakupa dakika mbili kama huna uhakika una wajibu wa kulinda heshima ya Wabunge. Naomba uondoe maelezo yanayosema kwamba, Wabunge wameshiriki kwenye huo mchakato tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa lakini nitakutafuta kwa wakati wako kukupa taarifa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nadhani maelezo yale yameondolewa kwenye *Hansard* ya Bunge kwa sababu, Waheshimiwa Wabunge tusilete Bungeni shutuma ambazo hatuwezi kuzithibitisha, shutuma ambazo zinashusha hadhi ya Bunge na shutuma ambazo zinashusha heshima ya Wabunge. Michango yetu ni mizuri, lakini tujiepushe sana na kauli ambazo Kiti cha Spika kitakudai uthibitisho ambao unaweza ukashindwa kuuleta, kitu ambacho hakitatujengea heshima. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Katani, nakushukuru sana kwa ushirikiano ulionipa, kama Mwenyekiti. Sasa ninamuita Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, atafuatia Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii muhimu ya Serikali.

Kwanza kabisa nawapongeza sana Mawaziri wote, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Profesa Kitila na Manaibu wao pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hizi muhimu. Naomba nichukue nafasi hii ya kipekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ya kipekee kwa namna ambavyo

anawatendea wema wananchi wa Tanzania, lakini kwa namna ya kipekee ambavyo anawatendea wema Wananchi wa Jimbo la Chemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina maeneo machache sana ya kuchangia. Eneo la kwanza ambalo ninataka kusema kidogo ni namna ambavyo fedha zinagawanywa kwenye maeneo yetu. Ni kweli kabisa kwamba, hapa leo tunapitisha Bajeti ya Serikali na tunaamini fedha hizi zinapaswa zigawanywe sawa kwenye miradi ya maendeleo katika Wilaya zote Tanzania, lakini kumekuwa na uwiano hafifu sana wa kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano kidogo. Tunafahamu fedha za maji hazikutoka zote kwenye bajeti iliyopita, lakini yapo maeneo ambayo miradi imepelekewa fedha 90%, yapo maeneo ambayo miradi imepelekewa fedha kwa 35%. Sasa mimi naomba, tunapitisha bajeti hii, mimi nina miradi 17 ya maji, kwenye bajeti hii naogopa kwamba tunapitisha bajeti ambayo inaenda kuhudumia miradi 17 ya maji, lakini fedha zikienda 35% maana yake miradi hii inaenda kukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoumiza zaidi ni ile kwamba, maeneo mengine fedha imetoka 35%, maeneo mengine imetoka 90%. Mimi naomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kama kuna hali yoyote ya upatikanaji hafifu wa fedha au mapato kidogo yametikisika, tutoe fedha kwa *ratio* sawa kwenye Halmashauri zetu au kwenye Wilaya zetu. Hii inaweza kusaidia sana kutoka pamoja kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba, tunaenda kujenga bwawa kubwa pale Farkwa. Mradi huu umekuwa wa muda mrefu sana, bahati nzuri safari hii kandarasi imetangazwa. Namuomba Mheshimiwa Waziri anayetoa fedha, hebu tuletee fedha, ili tumalize jambo hili la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kidogo kuhusu mapato. Wabunge wote hapa wamechangia kwamba kuna shida ya ukusanyaji wa mapato na hii haina mjadala. Hatunashaka hata kidogo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, hatuna shaka na Mheshimiwa Profesa Kitila, lakini hii changamoto imekuwa kubwa. Ni kweli kwamba, Watanzania hawalipi kodi, je, nani anayepaswa kukusanya hizo kodi? Ukifuatilia takwimu kwa miaka mitatu hii, ukienda *BRELA* utakuta watu waliokuwa *registered* kwenye biashara *Group A* au *Grade A* ni zaidi ya 53,000, lakini *margin* ya kodi *average* kwa miaka mitatu mfululizo ni ileile shilingi trilioni 2.3, trilioni 2.1 sasa hao wanaoongezeka hawalipi kodi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu changamoto hii ndiyo inayotuletea shida kwenye majimbo huko, ndiyo inayotuletea shida kwenye Wilaya huko. Wenzangu hapa wanasema kwenye mfuko wa maji zaidi ya shilingi bilioni 200 hazikutoka; haziwezi kutoka kama kuna makusanyo hafifu kwa sababu, Serikali haina duka. Sasa tusibaki tu kila siku tunalalamika kwamba, fedha za mapato hazikusanywi, Watanzania hawalipi kodi, lakini tuna watu tumewapa kazi ya kuhakikisha wanakusanya fedha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nani tumlaumu? Tumlaumu Mheshimiwa Waziri? Tumlaumu Naibu Waziri? Tumlaumu Katibu Mkuu au tumlaumu nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri ni lazima kama Bunge tuangalie sasa ni nini changamoto ya fedha hizi kutokukusanywa. Mtu mmoja amesema hapa yeye tukimpa ile Bandari tu ya Dar es Salaam inatosha kutuletea hizi fedha zote tunazopata kwa mwezi. Sasa maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, kuna *loophole* nyingi ambazo zinasababisha upotevu huo wa mapato. Sasa mimi naomba nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, hili jambo limesemwa sana, kila mwaka linasemwa hilo hilo na hakuna tamko rasmi la ni nini tufanye, ili tuhakikishe tunakusanya kodi hizo na hilo ndilo linalotuletea matatizo mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni mipango yetu. Nimesikia Wabunge wengi wanasema kuhusu mipango na ukweli migogoro yote ya ardhi, shida zote hizi za fedha kutokupelekwa sawa maana yake ni ukosefu wa mipango, maana yake ni tuna

shida kwenye mipango. Unakuta jimbo linaupatikanaji wa maji 92%, lipo lingine lina 32%, tafsiri yake ni tuna mipango isiyo sawa. Sasa namuomba Mheshimiwa Prof. Kitila, ambaye namuamini sana, changamoto nyingi tulizonazo zinaweza kutibiwa kama tu tutakuwa na mipango mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ambayo inatekelezeka, mipango ambayo kila siku tukija hapa Bungeni tunasema hayohayo, lakini hayatekelezeki. Namuomba sasa Mheshimiwa Profesa, namfahamu ni ndugu yangu, rafiki yangu wa muda mrefu, hebu tubadilishie sasa. Ukienda kule kwangu, kila mwaka nasema hapa, kuna watu, wakulima zaidi ya 1,197 mashamba yao yapo wilaya nyingine na hauruhusiwi kwenda kulima kwa sababu, ya mipango haipo sawa. Ninaamini sana tukiwa na mipango mizuri ardhi yetu yote nchini tutaipima na kila mtu atajua kipato chake na tutapunguza karaha hii ya migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme maneno mawili, matatu, kuhusu hali halisi ya majimboni. Naomba sana Waziri, tuna changamoto ya vipaumbele vya Serikali kubadilika na hili ninafikiri Wabunge wote wameliona. Ukifuatilia Bajeti za Kisekta ni kama kipaumbele cha Serikali kime-*shift*, nataka niseme fedha za barabara sasahivi ni kama zimekuwa kidogo sana na ninyi mnafahamu kwamba, ili tuweze kukusanya kodi ni lazima tuwe na barabara nzuri. Fedha za Wizara ya Maji zimepungua sana na wewe unajua kabisa, ili mtu awe na afya nzuri aweze kukusanya kodi ni lazima apate maji. Mimi nawaomba sana, sasa ninataka kuwaona watalaamu hawa ni namna gani wana-*shift* kwenye vile vipaumbele muhimu vya Watanzania kwenda kwenye vipaumbele ambavyo sisi Wabunge wengi hatuvielewi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombeni sana katika hilo hebu tuangalie namna bora ya kuhakikisha kwamba, tunabaki kwenye vipaumbele vyetu muhimu ili nchi yetu iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Monni. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, atafuatia Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate na Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2024/2025. Bajeti hii inayoombwa ni Pesa za Kitanzania trilioni 49.8. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia nimpongeze Waziri wa Fedha, kwa kazi nzuri pamoja na Mawaziri wengine wote, kwa kweli wanamsaidia kwa ukaribu sana na kwa umahiri mkubwa Mheshimiwa Rais wetu kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu leo utajikita kwenye kuishauri Serikali namna ya kukuza uchumi kwenye eneo la lishe, lakini pia kwenye eneo la usalama wa chakula. Serikali imeweka mpango mzuri sana wa kuhakikisha kwamba kwenye eneo la lishe ili wananchi waweze kupata afya bora na waweze kuendelea kuzalisha na kulizalishia Taifa mapato yaliyo mengi zaidi kwenye eneo la uzalishaji ni kupitia ufugaji wa vizimba katika Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitenga pesa zaidi ya shilingi bilioni 20 kupeleka kwenye maeneo hayo ili kufanyika uwekezaji wa vizimba hivyo. Vizimba hivyo vimefanyika zaidi kwenye ukanda wa Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika lakini tunafahamu kwamba katika nchi yetu ya Tanzania tunayo maziwa zaidi ya hayo ikiwepo Ziwa Nyasa. Naamini kabisa hata wawekezaji wa vizimba hivi walioko kwenye maeneo ya Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika nao pia walipata mafunzo, walielimishwa na ndiyo maana wakaweza kufanya uwekezaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha, mimi mwaka huu nikisimama hapa ni kusikitika tu juu ya suala la uendelezaji wa masuala ya kiuchumi katika Mkoa wangu wa Ruvuma hususani kwenye Ziwa Nyasa. Kuhusu Ziwa Tanganyika alisimama Mheshimiwa Mbunge hapa jana alikuwa analalamika kwamba wao wamepata vizimba 29 tu. Naomba nimwambie Mheshimiwa

Mbunge huyo kwamba, sisi katika Ziwa Nyasa hakuna kizimba hata kimoja. Mnataka kutuambia kwamba, Wavuvi wa Ziwa Nyasa Wawekezaji wa Mkoa wa Ruvuma hawana uwezo wa kuelewa kama wataelimishwa juu ya uwekezaji wa vizimba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kusiwe na ubaguzi kwenye uwekezaji kwenye maeneo yote katika nchi yetu. Maziwa yapo zaidi ya hayo mawili yaliyowekezwa lakini upande mwingine hakuendi. Keki hii ni ya kwetu sisi sote Watanzania, igawiwe sawa kwa sawa na maeneo mengine ambayo wanapewa fursa hii haipendezi na wala haitavumilika. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nipo kwenye eneo hilo hilo la lishe suala la ulaji wa samaki katika nchi yetu ya Tanzania imekuwa ni anasa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msongozi, kuna taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** …Mheshimiwa Sanga nakuomba sana nina mambo ya msingi sana ya kuchangia tafadhali sana usinitafunie muda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msongozi, kuna Taarifa. Tafadhali.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Leta Taarifa ya maana tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpa taarifa dada yangu Mheshimiwa Msongozi, anachokizungumza kwenye Ziwa Nyasa ni kweli wavuvi wa ukanda ule wanapata shida. Serikali ya upande wa pili ya nchi jirani wana bajeti kwenye Wizara yao inayomwaga chakula pembezoni mwa Ziwa. Kiasi kwamba, samaki wote wamekimbia kutoka Tanzania wameenda kwenye nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge ni sahihi kabisa hawatendei haki hasahasa kwenye suala la maendeleo ya eneo lile pale. *(Makofi)*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msongozi, umepokea Taarifa?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, una akili, ninaipokea Taarifa yako, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kama ifuatavyo: suala la ulaji wa samaki katika nchi yetu imekuwa ni anasa yaani Mtanzania kwenda kununua samaki kwa kweli samaki ni bei mbaya sana, lakini kulingana na uwekezaji huu sasa unaoenda kuwekezwa ninaamini kabisa utaongeza tija. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani kwamba tungeongeza sasa kwenye uwekezaji wa eneo hilo turuhusu hata samaki wengine kutoka nje ya nchi waweze kuingizwa. Samaki watakapokuwa wanaingizwa kwa wingi katika nchi yetu basi suala la lishe… kwa sababu samaki ana virutubisho vingi lakini imekuwa ni anasa kumpata samaki huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, familia nyingine hawawezi kula samaki kwa sababu hawana uwezo wa kumpata huyo samaki. Kwa hiyo, samaki hawa wakiruhusiwa kuingizwa kwanza tutaongeza Pato la Taifa lakini pia wananchi wataweza kunufaika kwa kupata lishe iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula cha mifugo, mimi naona kabisa kwenye eneo la chakula cha mifugo tumefeli. Niwaambie wazi kwamba tumefeli kwa sababu unaangalia kwenye suala la wafugaji wanapata shida sana kwenye kupata chakula na wakipata hicho chakula unakuta chakula ni bei kubwa mno. Kwa mfano, wafugaji wa samaki na wawekezaji wa mabwawa unakuta chakula kilichokuwa kizuri kwa wao wanavyozungumza kinapatikana nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini chakula hicho kinapoingia nchini kinakuwa na tozo nyingi nyingi kiasi ambacho kikishaingia maana yake kinaendelea kuongeza bei kubwa kwa mlaji wa mwisho. Kiasi ambacho sasa uwekezaji ule unaokusudiwa kwenye ufugaji wa samaki haufikiwi. Mimi nadhani ni vizuri basi kuondoa zile tozo zisizokuwa za lazima ili wawekezaji hawa waweze kufanya vizuri kwenye uzalishaji wa samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Sukari; huu sasa ni uchangiaji wangu namba mbili ambao unahusisha suala la usalama wa chakula. Nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru Serikali kuona umuhimu wa kuleta Sheria ya Sukari, kwa maana ya mabadiliko. Sheria hii ni vizuri sasa ikabadilishwa na ikarekebishwa ili kwenye eneo hili tuweze kupunguza urasimu ambao unaendelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *gap sugar* ni jukumu la Serikali kusimamia na kuhakikisha kwamba inalinda hali ya walaji katika nchi yetu lakini pia kusiwe na upungufu wowote na hata kusababisha ongezeko la bei kubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, ukiwasha washa taa hiyo unanichanganya, labda ungeizima kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msongozi, muda umeisha. Tuna changamoto ya muda tafadhali. Naomba hitimisha tafadhali.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, nahitimisha. Sheria ya Usalama wa Chakula ni kama hivyo nilivyoeleza. Kuna vitu ambavyo vinasikitisha sana wawekezaji wa sukari katika nchi yetu wapo saba ambao ndio wenye viwanda. Wamekuwa wakilindwa katika nchi hii kwamba wazalishe wauze na kama inatokea *gap sugar* wao ndio wawe waagizaji, lakini wamekuwa wana-*delay* kwenye kuagiza sukari kwa wakati kwa

sababu ambazo wao wanazijua ili sukari hii iadimike na waweze kufanya biashara kubwa kwenye suala la sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halikubali, halikubali kabisa kwa sababu inavyooneka sasa hivi ni suala la masikio kuzidi kichwa hatuwezi kuendeshwa katika nchi hii na watu saba ambao wao ni matajiri wawekezaji wa sukari kwenye eneo hilo… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, naomba hitimisha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** …kiasi ambacho sasa wanaweza ku-*drive* nchi hii na wa wakatupangia bei kwenye eneo hili. Suala hili halikubaliki na kwa sababu umeninyima muda nafikiria kama niunge mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa nashukuru.

Waheshimiwa Wabunge, tuna changamoto cha muda, naelewa sana tuna hoja nyingi naomba niwashauri zile hoja ambazo mnadhani ni muhimu sana Serikali izichukue, nashauri sana muanze nazo ili tuweze kuachiana dakika kumi kumi. Tukizidisha dakika moja mpaka mbili kuna Waheshimiwa Wabunge wengine watakosa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, nitaomba sana muivumilie Meza kwenye jambo hili, wale ambao watazidisha tutazima *microphone*. Ahsante sana, Mheshimiwa Msongozi tunakushukuru kwa mchango wako mzuri.

Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Geoffrey Mwambe na Mheshimiwa Maimuna Pathan, ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kuendelea kuwepo katika Bunge hili kuwatumikia Wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa Watanzania. Tumeshuhudia miradi mingi mikubwa sana lakini pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais, hatuwezi kuacha kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na Wasaidizi wako mnafanya kazi nzuri na ndiyo maana tunaona miradi inakwenda vizuri kila kona na imegusa kila sekta mambo yanakwenda vizuri lakini pamoja na kukupongeza wewe pia ninampongeza Waziri wetu wa Mipango kwa mipango mizuri ambayo ameileta ninaamini Tanzania tunaendelea kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sana suala la kulipa kodi hasa kudai na kutoa risiti. Mheshimiwa Waziri uliongelea hili jambo kwa ukali sana na kwa uchungu kuonesha namna unavyoipenda nchi yako na uzalendo kwa Taifa lako. Kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha Watanzania walio wengi hatuna tabia ya kulipa kodi au kudai risiti. Hili jambo mimi nilikuwa nasema ni kukosa uzalendo, kwa sababu hii nchi ni ya kwetu sisi wenyewe na ninaamini tutaijenga sisi wenyewe kwa kulipa kodi na tunapokwenda kununua na kuuza tukatoa na kudai risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa najiuliza tuanze sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge hivi sisi kweli ni wazalendo katika jambo hili? Tunalipa kodi? Tunadai risiti na kutoa risiti pale tunapouza na kununua? Mimi niwape mfano, tena wa hapa hapa ndani ya Bunge, ni mara ngapi mmenda pale *canteen* umenunua chakula, umedai risiti? Unapewa chakula unaondoka, hiyo ni kukosa uzalendo lazima tuambizane ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge tuwe namba moja tunapoenda kufanya mikutano tuwahimize Watanzania, kwa nini tunahitaji walipe kodi? Kwa nini tunahitaji wadai risiti? Hii ndiyo itakayosaidia miradi. Unakwenda kule unanunua kitu hujadai risiti au wewe unapofanya biashara hujatoa risiti. Unakuja hapa Bungeni unaomba mradi wa maji, unaomba mradi wa barabara hiyo ni kukosa uzalendo. Kile unachokifanya nje ndicho uje kukidai hapa. Kwa hiyo, mimi ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge sisi tuna nafasi kubwa, tuna maeneo mengi ya kusemea. Hebu

tutoke tushirikiane na Serikali twende kuwahimiza wananchi juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini kila Mtanzania akisimama vizuri katika jambo hili tukalipa kodi, tukatoa risiti na kudai risiti tutapata mapato mengi na ni sehemu ndogo sana ambako hatufanyi hili. Ninajua Wabunge wengi mnaweza msifurahie lakini sisi lazima tuwe mfano. Lazima tuwe mfano ili tumsaidie Mheshimiwa Waziri na tumsaidia Mheshimiwa Rais. Tunahitaji fedha nyingi kwa ajili ya miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana hili jambo Serikali ilichukue, tuanze kuwafundisha watoto wetu juu ya uzalendo, juu ya kulipa kodi, juu ya kutoa na kudai risiti. Hili jambo likianzia toka huko chini ninaamini mambo yatakwenda vizuri. Kwa hiyo, niombe sana hili tulisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilisemee, Serikali na nyinyi kuna sehemu ambapo hamfanyi vizuri. Wakati mwingine unaenda kwenye duka wanakuambia hapa tuna miezi miwili mashine ya *EFD* imeharibika. Jukumu lenu Serikali lipo wapi? Lazima turudi pande zote. Mimi nilikuwa najaribu kuangalia sisi tunahitaji Watanzania wakalipe kodi, hivi Serikali ikinunua hizi mashine ya *EFD* mkawapa wafanyabiashara wote, mimi ninaamini litaondoa huu usumbufu wa kutokuwa na mashine. Sehemu nyingine unakuta mashine imeharibika lakini haijategenezwa wanakuambia tumetoa taarifa Serikalini hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri hili nalo uliangalie, wanunulieni na kuwapa mashine wafanyabiashara ili sasa liwe jukumu la sisi kufuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nataka nikisemee, kuna hili suala la kukadiria hawa wafanyabiashara, lipa shilingi milioni 20, lipa kiasi fulani. Hili Mheshimiwa Waziri linatengeneza mazingira ya rushwa, kwa nini mfanyabiashara anapofanya biashara msiangalie biashara yake akalipa kwa mujibu wa Sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaanzia labda mfano shilingi milioni 80 lakini wanashuka wanashuka mwisho wa siku, hiyo shilingi milioni 80 hupati. Unapata shilingi milioni 10 halafu nyingine inaingia kwenye mfuko wa huyo mtu ambaye wanaenda ku-*negotiate*. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali hili nalo mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri umeongelea suala la kilimo kuendelea kuwekeza nguvu. Ni kweli kilimo ni uti wa mgongo mimi niombe sana Serikali mmeanza kuonesha kazi nzuri ya kuweka nguvu kubwa kwenye kilimo na mimi niwapongeze katika hili. Mmeweka nguvu kwa upande wa mazao yetu haya kimkakati tumeona mazao haya yameanza kupanda bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitoe mfano, mwaka 2022 nilikataa kuunga mkono hapa bajeti, nikitaka kahawa iuzwe kwenye mnada. Baada ya Serikali kulipokea kahawa imeuzwa kwenye mnada Waheshimiwa Wabunge imetoka shilingi 800 mpaka 1,100 sasa hivi tunaongelea shilingi 5,000 na kitu. Huu ni ushindi mkubwa na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Bashe kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** … na hili lisiishie hapa. Mimi naamini haya mazao yetu ya kimkakati tuki…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Muda wako umeisha tafadhali.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, ajiandae.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia machache kwenye hotuba mbili za Bajeti Kuu ya Serikali lakini pia na ile ya Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningependa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake hadi leo hii, lakini pia, nikishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi na Serikali yake chini ya Jemedari wetu Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli naomba tu nimhakikishie Mama kule Masasi sisi tumejipanga tupo vizuri na wala asiwe na wasiwasi mimi nipo kule. Niwashukuru pia Wananchi wangu wa Masasi Mjini kwa kuendelea kunivumilia lakini pia kunipa mwongozo na kunisimamia katika kutekeleza majukumu yangu kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo sasa naomba niingie kwenye mchango wangu. Ni bahati mbaya kwamba, muda ambao tunapewa kuchangia ni mdogo. Kimsingi hizi hotuba ni mbili ni Wizara mbili tofauti na tafsiri yake ni kwamba, tunapewa dakika tano tano kila Wizara. Pia, ni Wizara ambazo ndiyo Wizara *core* za kiuchumi kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, labda tunaweza tukafikiria hapo baadaye tuweze kuona upande wa Mipango iwe na siku yake iwe na mfumo wake wa kujadiliwa na Wizara ya Fedha iwe na siku yake ya kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu zamani ilikuwa ni Wizara ya Fedha na Mipango kwa hiyo, ilionekana kama vile ni Wizara moja tu lakini kwa sasa ni Wizara mbili tofauti. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kuleta hili kwenye meza yako ikiwezekana Kamati ya Uongozi muweze kulifikiria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ningetamani sana kushauri kwa wenzangu hapo Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo pamoja na Waziri wa Fedha, ikiwezekana tunayo Jumuiya ya Wachumi Tanzania, hebu bajeti kama hizi zinavyoandaliwa na taarifa kama hizi basi tuzipitishe kwenye vyombo vya fani zile ili tuweze kupata michango mizuri zaidi ikiwezekana tuweze kuboresha na kusaidia mchango wetu kwenye Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia baada ya kupitia taarifa hii ningetamani kupata ufafanuzi kidogo kabla sijachangia. Ukienda Ukurasa wa 29 wa Hotuba ya Mipango inaonesha pale mwenendo wa deni la Taifa. Sasa takwimu zake zilizopo pale kuna mkanganyiko kidogo. Kuna takwimu ambazo zinajirudia rudia kwa hiyo inaonekana kama vile kulikuwa na shida wakati wa uandaaji wa hii taarifa. Kwa hiyo, labda wanaweza wakanifafanulia kama ipo hivyo hivyo ili wakati wa kuchangia nijue nitachangia hivyo au kulikuwa na marekebisho kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano deni la ndani Machi, 2017 inaonesha ilikuwa ni trilioni 12.074, deni la nje mwaka huo huo ilikuwa ni kiasi hicho hicho na sasa deni kuu unajumlisha deni la nje na deni la ndani halafu kiasi ni kile kile trilioni 12 kitu ambacho haikiwezekani. Pia ukienda kwenye mwezi Machi mwaka 2021 deni la ndani ni trilioni 16.117, deni la nje trilioni 12.074 lile la 2017 halafu ukijumlisha zote mbili unapata ile ile 12.074. Kwa hiyo, inaonekana kama kuna mkanganyiko kidogo wakati wa uandaaji wa hii taarifa. Sijui kama utaruhusu nijibiwe kwanza hilo ndiyo nichangie au niendelee kuchangia tu kwa kujua kwamba hizo ndiyo takwimu halisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Geoffrey Mwambe taratibu inakutaka uoneshe kama kuna mapungufu, Serikali itapata muda wa kujibu wakati ambapo wataitwa na Kiti cha Spika. Kwa hiyo, unaweza tu ukatumia fursa hii kuonesha mapungufu uliyoyaona na ukachangia kwa upande ule unaodhani unafaa halafu Serikali itapata nafasi ya kutafakari na itakuja. Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa mwongozo wako, basi naomba nikimbie kwa

sababu muda wenyewe ni mdogo niainishe maeneo ambayo labda tungeweza kuyaimarisha kidogo ili bajeti zetu na hasa Mpango wetu uweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza nikubaliane sana na Mheshimiwa Askofu Gwajima, ni vizuri mpango wa bajeti uandaliwe na kujadiliwa kwa kina kabla ya Wizara za Kisekta, kwa sababu tunapojadili hapa tukibaini kwamba kwenye mpango, hiki na kile na kile kirekebishwe na utekelezaji ni Wizara za Kisekta tunafanyaje wakati tumeshapitisha bajeti zao? Kwa hiyo nilikuwa nafikiri hii ilitakiwa ije mapema itengenezwe mwongozo kama *framework* kwa ajili ya *Sectoral Ministries* kuweza ku-*adopt*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nilikuwa natamani sana …

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Geoffrey Mwambe samahani naomba uketi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Profesa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwa sababu linajirudia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mpango ambao tumeuawasilisha hapa ni mpango ambao mchakato wake unaanza mapema, mtakumbuka kwamba mwaka jana mwezi Novemba, Bunge hili lilijadili kwa siku saba mapendekezo ya mpango wa taifa wa maendeleo, baada ya hapo tarehe 13 mwezi wa kwanza mwaka huu tumekuja rasmi kwa ajili ya kupokea Mpango wa Taifa. Kwa hivyo, mchakato wake ni mrefu, ni mchakato wa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari hapa wanachojadili walishajadili mapendekezo yake kwa siku saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo Waziri wa Mipango na Uwekezaji. Mheshimiwa Mwambe unapokea taarifa?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea hiyo taarifa lakini labda tu kumshauri Mheshimiwa Kitila Mkumbo kwamba ule ulikuwa ni mchakato wa kupata maoni lakini alichowasilisha juzi ilikuwa ni hotuba rasmi sasa, ambayo tunasema ingetangulia ili Wizara za Kisekta ziweze kufanya *mapping,* zijielekeze kwenye kilichoandikwa kwenye mpango ili tusi-*miss point*. Kwa sababu kama sasa hivi hapa tukisema turekebishe kwenye mpango alichokisema sasa, Wizara ya Kilimo inaweza ikarudi ikarekebisha? Haiwezekani! Wizara ya Miundombinu inaweza ikaja kurekebisha? Haiwezekani! Kwa hiyo labda ni kuona namna tu yaku-*improve*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nidokeze maeneo machache ambayo nilitamani niyasikie. Kwa mfano, nilikuwa natamani sana kuona kwenye mpango wa bajeti tunaonesha juhudi na mkakati wa kukuza umri wa kuishi wa Mtanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe naomba uhitimishe muda wako unaisha.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Sawa. Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani sana wenzangu waweze kuonesha namna ambavyo tunaweza tukaimarisha umri wa kuishi lakini pia matumizi ya takwimu za sensa. Tumefanya sensa karibuni ni namna gani tunaweka juhudi za kupunguza kiwango cha umaskini kwenye nchi yetu lakini pia tunaongeza matumizi ya maeneo kama ya nishati kwa mfano *SNG,* kwa sababu tunataka sasa na hata Mheshimiwa Rais ana-*thrive* matumzi ya gesi kwa hivyo natamani mpango ujielekeze vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwambe, tafadhali ahsante nashukuru.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mchangiaji anayefuata lakini nadhani mchango wa Mheshimiwa Mwambe, nadhani utaratibu wa Kibunge uliopangwa ulitafakariwa kwa muda mrefu sana, nadhani kama tukitumia vizuri zile siku saba za kujadili mpango ambao unaelekeza kwenye Wizara za Kisekta kuandaa bajeti zao, tukitumia ile nafasi vizuri tunaweza kuziongoza Wizara za Kisekta kuweza kutengeneza bajeti, kwa sababu inakuwa kipindi ambacho Wizara za Kisekta hawajaleta bajeti hapa. Kwa hiyo nadhani Profesa ameeleza tuendelee kufanyia kazi Waheshimiwa Wabunge, ni jambo la kutafakari lakini naamini tukitumia zile siku za maandalizi za mwanzo zinaweza kusadia Wizara za Kisekta kuweka mipango yao vizuri na tunapojadili bajeti za kisekta tunaweza kuwa *more focused* kwenye maeneo hayo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwambe samahani muda wako ulituishia lakini nadhani yale ya msingi Serikali imeyachukua.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Maimuna Pathan atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve na Mheshimiwa Michael Costantine Mwakamo ajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia mpango wa maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024/2025. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya uhai na pia nampongeza Rais wetu kipenzi Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa kazi zake kubwa ambazo anaziendeleza na tunaziona na pia nimpongeza Waziri wetu Mwigulu na Waziri wa Mpango, mmeandaa kitu kizuri tumekiona, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchango wangu ni mdogo sana. Mchango wangu wa kwanza nataka nizungumzie Kada ya Ununuzi na Ugavi, sana sana Serikalini. Kada hii ya ununuzi na ugavi tunaona imeongezewa kazi, kuna kazi ambayo ilikuwa inafanyika kwenye kada ya uhasibu na ilikuwa inapatikana

kwenye *Finance Act,* kuna masuala ya vifaa *(assets)* kazi hii ikiwa inafanywa na uhasibu lakini sasa hivi kuna mabadiliko ya sheria kazi hii imerudi inatakiwa ifanyike kwenye kada ya ununuzi na ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali. Kwanza naomba tuiandae kada hii kwa kazi rasmi ambayo inaingia kwenye kada yao. Tutaiandaaje kada hii? Kwenye Serikali yetu ninaona kada mbalimbali ambazo zipo, kwa mfano, kada ya uhasibu. Kuna Mhasibu Mkuu wa Serikali, kuna Mganga Mkuu wa Serikali, kuna Mfamasia Mkuu na kada nyingi zina Mkuu, mkuu mkuu wa Serikali lakini hii kada ya ununuzi ni kama vile imetengwa fulani kama vile siyo kada rasmi au siyo kada ambayo inafanya mambo ya muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke ndugu zangu, pesa kubwa ya Serikali, hela nyingi zaidi ya 80% inaingia kwenye ununuzi. Sasa kwa kuwa pesa nyingi ya Serikali inatumika kwenye ununuzi hii kada ninaomba tuiboreshe apatikane Afisa Ununuzi Mkuu wa Serikali. Kada inapokuwa haina mkuu kule juu inakuwa inalega lega, kwa sababu kuna mambo mengi yanashindwa kwenda sawa, kada hii inatumia pesa nyingi sana za nchi hii. Ninaomba sana kada hii iandaliwe, iwekewe Mnunuzi Mkuu wa Serikali, waweke malengo vizuri na kuwawekea kupokea kwenye kazi hii ya vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia kunapokuwa na Mkurugenzi wa Ununuzi awe na wasaidizi wake wawili. Mmoja awe anaenda kwenye ununuzi, mmoja awe anaenda kwenye vifaa kwa sababu, kada hii imeongezewa vitu ambavyo vilikuwa vipo kwenye uhasibu. Kada hii ya ununuzi naomba ku-*declare interest,* mimi mwenyewe ni mnunuzi, ninaifahamu. Kada hii huwa inapigwa vita na kupewa mizigo ambayo wakati mwingine siyo ya kwake. Mara nyingi malalamiko yakitokea kwenye ununuzi wa Serikali kwenye miradi mbalimbali ya Serikali wanatupiwa mizigo kada ya ununuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie leo, mara nyingi kesi mbalimbali zinazotokea, barabara mbovu, majengo

mabovu, ununuzi wakati mwingine labda vitu vimefanyika visivyo, wakati mwingine siyo wanunuzi wanaofanya hayo mambo. Mnunuzi anafanya sehemu yake anayotakiwa afanye lakini yeye ni mtaalam wa ununuzi. Tukumbuke kwamba kwenye barabara kuna wataalam ma-*engineer,* kwenye majengo kuna wataalamu ma-*engineer,* wale ndiyo wanakuwa wasimamizi wakuu wa yale mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana, mara nyingi sana wanapata lawama lakini baadae wanapokuja kufuatilia utakuta kada hii hawana kosa jamani, kuna watu pale nyuma yake ndiyo wanakuwa na makosa hayo. Kwa hiyo niombe kada hii tuimarishe, tuwatafutie semina vizuri, wapokee kazi ambayo imeingia iliyokuwa upande wa pili na tuwaimarishe jamani, kwa kweli tuwaimarishe, wanatumia pesa nyingi ya nchi yetu, wanatakiwa wapewe kazi na muongozo ulio imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wetu wa Maendeleo ya Taifa 2024/2025 tunaona kwamba kuna vipengele hapa, kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, kukuza biashara na uwekezaji, kuchochea maendeleo ya watu, kuendeleza rasilimali watu na vitu kama hivyo. Kipengele hiki cha nne kuchochea maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wangu wa Lindi asilimia kubwa kuna kazi mbili zinazofanyika, wananchi wengi ni wakulima, wananchi waliobaki asilimia kubwa ni wavuvi. Nikija kwenye suala la wakulima hiki kipengele cha nne kinachosema kuchochea maendeleo ya watu, kule Mkoa wa Lindi mpaka majirani zake mwaka huu itakuwa ni shida sana. Kuna huyu mnyama tulishapiga kelele mara nyingi sana kwenye Bunge lako, huyu mnyama anaitwa tembo, kiukweli wananchi wa kule wanakufa, wanauawa na huyu mnyama, wakienda mashambani kulima mazao yanaliwa, watoto wengi wanashindwa kwenda shule, hata hao waliolima ni wachache, wengi wameshindwa kulima, hata hao waliobarikiwa wakaweza kulima mazao yote yanaliwa na tembo. *(Makofi)*

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chinguile, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge anazungumza vizuri, hata kule kwenye Jimbo la Nachingwea mwananchi ameuawa mara ya mwisho tarehe 17 Juni, mwaka huu kwa hiyo hali siyo nzuri sana. Naomba kuunga mkono anachokizungumza.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chinguile, Mheshimiwa Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa. Sasa hali iliyoko ni njaa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha ahsante.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja sijaongea kabisa. Hali ni mbaya na sheria zilizopo sasa hivi Maliasili kifutajasho heka moja mtu unamlipa laki moja, halafu pamoja na kwamba kifutajasho wanalipwa laki moja bado hata vifutajasho vya mwaka jana wananchi hawajapata. Hali ni mbaya sana, tuwakumbuke wananchi wetu, hali siyo nzuri jamani. Huyu mnyama tumewashauri kutengeneza *solar electric fence* hata kwenye sehemu chache, tunaomba Serikali itusaidie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve atafuata Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu na ninaomba anisimamie katika mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa imara na mwanamke ambaye hajatikisika kuhakikisha anaendelea kuliongoza Taifa hili. Vilevile nikupongeze Mheshimiwa Mwigulu, kaka yangu na Mheshimiwa Mkumbo kwa namna ambavyo mnaendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ndiyo tunakwenda kuhitimisha Bajeti Kuu na kwa bahati nzuri kwa utaratibu mzuri ambao tumejiwekea ni kuwa, hata kama bajeti za kisekta tumeshazipitisha, mchakato huu unapata kutuongoza pale tunapoona kuna mapungufu na maboresho tunaweza kwenda kushauri kuhakikisha sasa bajeti yetu inakuwa na tija kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha bajeti yake hapa aliongea kwa masikitiko makubwa sana, aliongea kwa uchungu mkubwa sana na aligusa mioyo na mimi alinigusa sana pale ambapo alionekana akisema tunapoteza Watanzania wengi kwa vitu ambavyo tunaweza kuvi-*control*, vipo ndani ya uwezo wetu. Nami naungana na wewe Mheshimiwa Waziri, na mimi nasikitishwa sana, pale kama taifa tunakuwa na uwezo wa kuzuia vifo vya Watanzania na hatufanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunapoteza zaidi ya Watanzania 1,500 ndani ya miaka mitano tumepoteza Watanzania zaidi ya 6,000 hadi 7,000. Naomba nitumie fursa hii kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo iliona jambo hili na walisikitishwa na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 mpaka 2015 walichukua juhudi za maksudi wakatenga milioni zaidi ya 48 za Kimarekani, pesa za walipa kodi, pesa za watu maskini wakajenga kiwanda pale Kibaha, Kiwanda cha Viuadudu kuhakikisha tutazalisha dawa na kuzipeleka kwenye maeneo yetu kuhakikisha tunatokomeza malaria nchini. Kiwanda hiki ni cha kipekee, tuna viwanda kama hivi vitatu tu duniani, Japan, Tanzania na Cuba, kiwanda hiki kinatumia *bio technology*

ambayo bidhaa hii haina madhara kwa binadamu, haina madhara kwa wanyama, haina madhara kwa mimea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema nasikitishwa na *NIMR* walitoa hati kuwa dawa inayozalishwa pale Kibaha ni salama na safi kwa matumizi ya binadamu. Kitu cha kushangaza kwa taarifa iliyokuja hapa wiki iliyopita, toka mwaka 2017 mpaka 2024 tumenunua lita laki moja na tisini tu ndani ya miaka sita! Uwezo wa kiwanda hiki ni kuzalisha lita milioni sita, wakati tunajiwekea mikakati tulisema ndani ya miaka mitano maana yake lita milioni 30 tungezalisha pale na kutokomeza malaria kwenye Taifa hili. Tungeokoa maisha ya watoto, tungeokoa maisha ya akinamama na nguvu kazi ambayo ingekuja kufanya kazi kupandisha Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naungana na wewe, hatuna sababu ya kuona Watanzania wakiendelea kuteketea, tume-*invest* zaidi ya dola bilioni 48, *this ball is in your hands* Mheshimiwa Waziri. Kama ambavyo umekasirishwa na vifo vinavyotokana na ajali ndivyo hivyo tukahakikishe kupambana kuhakikisha tunaokoa maisha ya Watanzania yanayopotea kwa sababu tu hatujatekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kwa unyenyekevu mkubwa sana. Kila mwaka tunatumia zaidi ya shilingi bilioni 100 kwenye kununua *net,* kufanya makongamano na kufanya semina. Sasa najiuliza kwa nini pesa hizi... *(Makofi)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rose, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Chumi. Mheshimiwa Chumi, tafadhali.

**TAARIFA**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri wa dada yangu Mheshimiwa Rose, napenda pia kumuongezea taarifa kwamba dawa zinazotengenezwa na

kiwanda kile moja wapo wa wateja wakubwa ni Nchi ya Angola. Kwa hiyo, pamoja na sisi dawa ile pia ingeweza kutuongezea kuwa chanzo cha mapato ya fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Angola wameamini dawa hiyo na mimi nilishiriki wakati wa uzinduzi wa kile kiwanda, alikuja Makamu wa Rais wa Cuba. Kwa hiyo kama Angola wameamini kwa nini sisi kama Taifa tunashindwa kuamini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimuongezee taarifa Mheshimiwa Dada Rose. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rose Tweve, unapokea taarifa?

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa ya Mheshimiwa kaka yangu Chumi na yeye amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha tunatokomeza malaria kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na mchango wangu. Nilikuwa nahoji na ninajiuliza na nimejaribu kuuliza watu wengi; *if we are spending* shilingi bilioni 100 kwenye semina, ununuzi wa *net* na kufanya makongamano, kwa nini nguvu hiyo hiyo tusitumie kwenda kununua dawa ya viuadudu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnakuja hapa mnatuambia ndani ya miaka mitano hadi sita tumenunua tu lita 200,000 na nchi zingine wanakuja kununua dawa kwenye kutokomeza malaria kwenye nchi yao. Mheshimiwa Waziri, ndiyo maana nimesema mazungumzo tuliyonayo hapa bado tuna *room*. Naiomba Serikali twende tukakae Kamati ya Bajeti, Wizara ya Afya na TAMISEMI; twende kuokoa maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Bajeti ya Afya, wametaja malaria mara 57 lakini hakuna kifungu kinachosema tutaenda kununua dawa na kwenda kutokomeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza hivi kwa nini tunatumia hata neno “mapambano dhidi ya malaria,” tunapambana na nini Mheshimiwa Waziri? Kiwanda kipo pale ni kununua dawa na kunyunyizia, hayo mapambano tuyapeleke huko kwingine tukapambane na magonjwa ambayo yanashindwa kutibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili tutafanya historia. Mheshimiwa Waziri utaleta historia kwa nchi hii kuwa ndani ya miaka mitano ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeweza kutokomeza malaria kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *as long as...*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuwa kwenye Bunge hili, asubuhi, mchana na jioni nitaimba malaria kuhakikisha tuna...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rose...

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ooh, *thank you*. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Stella, samahani muda umeisha. *(Makofi/Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na kwamba muda umeisha nilipenda kumpongeza kiongozi wa mbio za mwenge kwa kuungana na haya maneno aliyoongea Mheshimiwa Rose sasa hivi, kwamba

Serikali za mitaa halmashauri zote zinapaswa kwenda kununua dawa zile ikiwemo Halmashauri yangu ya Nyasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za Bunge sawa sawa Mheshimiwa Rose Tweve unapokea taarifa ya Mheshimiwa Mbunge?

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa. Pia naomba unilindie muda wangu nina *point* za kumalizia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rose, muda wako umeisha, ahsante sana.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja.

**MWENYEKITI:** Naomba hitimisha, ninakupa dakika moja.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini nisipopata majibu ya kuridhisha, Mheshimiwa Kaka nyangu Dkt. Mwigulu anajua *how much I am proud of him,* nitashika shilingi kuhakikisha Tanzania sasa inakuwa *malaria free country*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tweve, ahsante sana, ninakushukuru. Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, atafuata Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi lakini kabla sijaendelea kwa kweli nampongeza sana mchangiaji mwenzangu aliyemaliza kuchangia sasa. Kiwanda ambacho ameendelea kukizungumza kikitoa hiyo malighafi muhimu katika Taifa hili kinapatikana katika

Wilaya ya Kibaha ambapo lilipo Jimbo la Kibaha Vijijini. Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anaendelea kutekeleza majukumu ya kulitoa Taifa liliko na kulipeleka maeneo mengine. Hii ni sambamba na wasaidizi wake Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa namna ambavyo wameleta hotuba zinazoweza kutusaidia kuchangia na kutaka kuwapa mawazo ni namna gani tunaweza tukaongeza uchumi wa Taifa hili kwenye kuendelea kuyatatua matatizo ambayo Mheshimiwa Rais anapambana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu leo utajielekeza sana sana kwenye kushauri Wizara hizo na hasa hasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali kwa ujumla ni kwa namna gani ambavyo Watanzania wana matumaini na namna Mheshimiwa Rais anavyofanya shughuli zake. Pia, Watanzania wanafahamu na Bunge tunafahamu, ili tuweze kufikisha malengo ya mipango tunayoipanga ni lazima tuwe na mikakati ya kuongeza uchumi wa Taifa hili kwa maana ya mfuko wa Taifa kupata pesa za kutosha na kutengeneza matumizi bora ya fedha hizo ili ziweze kutimiza malengo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi leo nitajielekeza kwenye kuishauri Serikali kwamba, tunafahamu chanzo kikubwa cha makusanyo ya pesa ya Serikali ni kodi. Huwezi kupata kodi ya kutosha kwa Watanzania kama mzunguko wa matumizi ya Watanzania ni mdogo. Pia huwezi kupata pesa ya kutosha na kuingiza katika uchumi wa Taifa hili kama uzalishaji au miundombinu ya uzalishaji itakuwa ni michache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitatoa mfano mmoja na nitaomba Serikali ielekeze nguvu kwenye uwekezaji wa hivyo na kuwasaidia wawekezaji hao kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kutokana na uhamasishaji Mheshimiwa Rais anaofanya na kufanya ziara

mbalimbali, wawekezaji wengi wameendelea kuliamini Taifa letu kama sehemu nzuri ya uwekezaji. Wanakuja Tanzania kutafuta maeneo ya uwekezaji na hakika maeneo ya uwekezaji kwa maana ya ardhi tunayo ya kutosha. Kwa sababu tunao wawekezaji wanaokuja wanakwenda kwenye maeneo ambayo yametengwa mfano mzuri ni kwenye maeneo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu tunalo kongani la viwanda pale Kibaha - Kwala. Pia tunayo kongani moja ya viwanda nyingine iko pale pale Kwala ambayo inaitwa *Modern Industrial Park*. Watu hawa wamewekeza mabilioni ya fedha pale; kwa mfano, hawa *Modern Industrial Park* wamewekeza shilingi trilioni 3.5 na wameshapima viwanja katika eneo lile. Wawekezaji wanakuja wanakutana na changamoto mbalimbali za kushindwa kufanya uwekezaji kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naiomba Serikali iende ikaungane na wawekezaji hawa walioko kwenye maeneo mbalimbali nchini wakiwemo hawa ninaowataja ili waweze kuwasilikiza na kuwatatulia changamoto zao ili watakapofanikiwa kuwaingiza wawekezaji wengi na kujenga viwanda maana yake Taifa hili litakwenda kupata pesa za kutosha. Zinavyopatikana fedha za kutosha ndiyo tutakavyokuza Pato la Taifa, tunakuza pato la mtu mmoja mmoja lakini pia tunafanya Watanzania wawe na mzunguko mkubwa wa umiliki wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mfano kwenye maeneo haya yote ya uwekezaji ninayoyazungumza likiwemo hili kongani la viwanda; wana shida kubwa sana ya upatikanaji wa maji. Wawekezaji wanakwenda kwenye yale maeneo lakini kuna shida ya maji. Nashukuru tu siku mbili zilizopita hapa Mheshimiwa Waziri tulipokuwa tunawasiliana na Wizara ya Maji amepanga kwenda kutembelea maeneo yale ya viwanda na ninamuombea kwa Mungu arudi salama kwenye mizunguko yake ya kitaifa ili tuambatane kwenda kuwasiliza watu wale na kutatua changamoto ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wawekezaji hawa wana shida kubwa sana ya uingizaji wa vifaa vya ujenzi. Wanakutana

na gharama kubwa sana ya kodi. Naiomba Serikali hasa Mheshimiwa Waziri ambaye nina hakika kabisa anaamini wawekezaji wakiwa wengi ndiyo uchumi wa Taifa unaongezeka; akawasikilize aone namna atakavyowapatia misamaha ya kodi ya baadhi ya vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana shida sana ya kupeleka pale vifaa vya ujenzi lakini vina kodi kubwa. Pia wana mambo mengine ambayo wameyaandaa kuyafanya kwenye maeneo yale kama ununuzi wa magari ya zimamoto kwa ajili ya kuweka usalama wa wawekezaji wanaokwenda pale lakini wanapata changamoto ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana Wizara na hasa Serikali ikawasikilize. Wawe wanawatembelea sana wawekezaji wetu hawa wawasikilize kwa ukaribu ili waweze kuwaondolea changamoto ambazo zitaendelea kutuongezea, kwa sababu hawa wawekezaji wanapokuwa wengi kwenye nchi yetu maana yake tunaongeza idadi kubwa ya wafanyakazi na hakuna kodi inayopatikana kirahisi katika nchi hii kama kodi zinazokatwa kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba wawasikilize wawekezaji, wawarahisishie kuwekeza katika nchi hii ili waweze kupata wafanyakazi wengi ambao watalipa kodi kwenye nchi hii. Watakavyolipa kodi kwenye nchi hii maana yake Taifa linakwenda kuongeza uchumi wake. Kwa hiyo, nawaomba sana na ninaiomba Serikali ifanye hivyo kwa ajili ya kuwasikiliza wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunafahamu mamlaka nyingine ya ukusanyaji wa mapato ni hizi halmashauri zetu. Yapo mapato ambayo yanakusanywa na halmashauri zetu nayo ni sehemu ya pesa zinazoingia kwenye Taifa hili. Naomba sana, tuna tatizo kubwa la pesa kwenye halmashauri kutumika zikiitwa pesa mbichi. Kwa hiyo, Serikali itafute mfumo mzuri utakaosababisha ukusanyaji wa pesa za halmashauri zisitumike kabla hazijaingia kwenye mifumo ya kimatumizi ili iweze kusaidia kutumia pesa hizi vizuri na kuikamilisha miradi na kuendelea

kufanya shughuli zingine za kimaendeleo ambazo zinakwenda kusaidia kuondoa changamoto zinazowakabili Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashauri na ninaiomba Serikali sasa isaidie kuondoa vikwazo ambavyo vinawafanya wawekezaji kuingia kwenye nchi hii vinavyoweza kuwarahisishia kutamani kuja kuwekeza ili wakifika kwenye yale maeneo ambayo yametengwa basi waweze kuwekeza kwa kadri ambavyo Mungu amewajalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi baada ya maneno haya, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakamo, nakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wageni wengine ambao hawakutangazwa muda uliopita. Kwanza tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni wapigakura wake kutoka Babati Vijijini Mkoa wa Manyara, karibuni sana. Popote mlipo simameni, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, ambao ni wapigakura wake kutoka Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mbunge, ambaye ni mchezaji wa zamani wa *Taifa Stars* kutoka Jijini Mwanza, Ndugu Amir Maftah, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge, ambao ni viongozi wa Taasisi ya *Bongo Net* kutoka Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, karibuni sana kama mpo. *(Makofi)*

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge, ambao ni umoja wa mabinti wajasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoa wa Geita. Karibuni sana kama mpo simameni. *Yes,* karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge, ambao ni marafiki zake kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge, ambao ni viongozi wa dini wa Jimbo Katoliki kutoka Mbulu Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge, ambao ni familia yake kutoka Hanang, Singida, Dar es Salaam na Mpanda, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 33 wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge, ambao ni Umoja wa Wanamakete Mtandaoni (*Makete Online Platform*) kutoka mikoa mbalimbali Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine waliotembelea Mbunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao viongozi 60 toka Taasisi ya *Young CEO Round Table Africa* kutoka Mikoa mbalimbali Tanzania wakiongozwa na Ndugu Zakayo Shushu, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 kutoka Taasisi ya *East African Youth Panel* inayojihusisha na vijana wajasiriamali na wafanyabiashara mbalimbali kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana na ahsanteni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage na Mheshimiwa Vuma Augustine, ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango. Mimi hawa kwangu mmoja ni mwalimu wangu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *mentor* na mwingine ndiyo *lifetime teacher* wangu wa maisha yangu yote hadi leo niko hapa; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo machache ya kuzungumza. Jambo la kwanza ninaunga mkono hoja. Ninaunga mkono hoja kwa sababu kama Wanamakete tuna kila sababu ya kuunga mkono hoja kwa takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumza kwamba ninaunga mkono hoja? Serikali hii imetufanyia mambo mengi sana Wanamakete. Jambo la kwanza kwenye Sekta ya Maji kwa sasa Makete tunaongoza kitaifa. Tunatoa maji kwa wananchi kwa zaidi ya 92% kwenye sekta ya *RUWASA*. Ukienda kwenye vituo vya afya, hadi mwaka 2020 tulikuwa na vituo vitatu vya afya, Kituo cha Matamba, Kituo cha Lupila na Kituo cha Ipelele. Ninavyozungumza leo tumejenga vituo vya afya vingine saba ndani ya miaka minne. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuona Serikali imetusaidia na imetuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ninamuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, namuomba sana sisi Makete tuna barabara ya kiuchumi ya kutoka Makete kuelekea Mbeya. Barabara hii ina mkandarasi tayari anajenga kwa kiwango cha lami. Tunakuomba malipo yaende kwa wakati ili mkandarasi aongeze *speed* ya ujenzi wa barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imebakiza *lots* mbili; *lot* ya kutoka Kikondo kuelekea Mbeya – Isyonje na *lot* ya kutoka Ipelele – Inio kuja maeneo ya Makete. Ni *lot* mbili zimebakia, kilometa 96 tu. Ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, mkandarasi yuko *site*, tunaomba alipwe ili ujenzi wa barabara hii uweze kuanza kwa ukamilifu wake na hatimaye Wanamakete waweze kuitumia barabara hii kwa sababu kwetu sisi hii ni oksijeni ya uchumi wa Wilaya ya Makate. Wanamakete wengi wanatumia sana barabara hii kwenda Mbeya kwa ajili ya shughuli za kibiashara.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunakutegemea sana kwamba, mtamlipa mkandarasi ili *speed* ya kujenga barabara iweze kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ni kwenye Barabara za *TARURA*. Makete ndiyo Wilaya ambayo katika Mkoa wa Njombe ina bajeti ndogo sana ya *TARURA* lakini sisi ndiyo wazalishaji wakubwa wa mazao mengi ambayo watu wa Dodoma na Dar es Salaam wanayatumia. Kuna barabara za kutoka Matamba kuelekea Itundu, barabara ya kimkakati kabisa na kiuchumi lakini hatuna fedha. Barabara ya kutoka Mang'oto kuelekea Ibaga, hatuna fedha na barabara nyingi za *TARURA* za Makete zina changamoto ya kutokuwa na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutokana na changamoto ya kutokuwa na fedha, wakandarasi hata wale wanaopatikana wamekuwa wakijenga kwa kilometa chache sana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msongozi, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mchangiaji anayechangia sasa hivi anachangia vizuri sana tena kimkakati. Hasa anapolenga suala zima la kuongeza uchumi katika Nchi yetu lakini nataka nimwambie changamoto ambayo anaiona Makete, changamoto hiyo hiyo ndiyo ambayo iko Songea Mjini kwenye barabara ya *TARURA* inayotoka Mshangano kwenda Mletele. Sasa na hii barabara ikienda ikajengwa kwa kiwango cha lami itachochea uchumi vizuri sana pamoja na Barabara ya kutoka Majengo kwenda Subira yenye urefu wa kilometa 18. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itakaa vizuri sana, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Msongozi yupo ndani ya kanuni, hajazidisha dakika mbili. Mheshimiwa Sanga unapokea taarifa ya Mheshimiwa Msongozi?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea taarifa yake na ninamuunga mkono kwa sababu anatetea Wananchi wa Ruvuma. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Barabara ya Makete ni kubwa na ni mtambuka. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ambalo ninasimama nalo leo hapa, Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sana tusikilizane. Ni suala la mabadiliko ya Sheria ya sukari ambalo Mheshimiwa Waziri amelizungumza hapa. Sheria ya Sukari Na. 6 katika mabadiliko yake kwenye kipengele namba mbili anasema "Kufanya marekebisho kwenye Kanuni ya *NFRA* kujumuisha sukari kuwa sehemu ya usalama wa chakula." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia *food security;* kwenye sheria yetu *food security* ina tafsiri hii, "*all people at all time have physical, social and economic access to sufficient and safe food to meet their nutrition needs for an active and heathy life*." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sukari, wananchi wanatusikiliza huko nje *in a very sensitive way*. Kwa nini nazungumza hili? Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Waziri wa Mipango nawapongeza sana kwa kuja na huu mkakati. hapa hesabu ni ndogo sana. Watanzania mnaotusikiliza, mlioko nje na mlioko hapa, hesabu ni ndogo sana. Hawa watu kwenye suala la sukari Serikali iliona ni tija iwape wenye viwanda kuagiza sukari nje, *sugar gap* inapotokea, Serikali iliona inatija. Lakini hawa watu kutokana na imani waliyopewa na Serikali wanapewa vibali waagize sukari; wao wamegeuza mchezo vibali wanakaa navyo na vingine

wanaviuza. Wakiviuza vibali hivi sukari inachelewa kutoka nje ili kujaza lile *gap* na hatimaye sukari ya ndani inapanda bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuomba, wasije wakaja na hoja kwamba Serikali hailindi viwanda, hakuna wakati ambapo viwanda vya sukari vimejengwa kama kipindi hiki cha Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan. Lakini katika kipindi hiki hiki Serikali tayari ina maeneo, maeneo ya Busega na Iringa ambayo inayaandaa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya sukari. Hoja ya kulinda viwanda vya ndani siyo msingi; hoja ni maisha ya Watanzania walioko kule nje ambao sukari ilifika shilingi 7,000, shilingi 11,000. Hatuwezi kuwa na hoja ya kulinda viwanda vya ndani na watu ambao wanaifanyia *sabotage* Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu tunajua wana nguvu na kuna maneno yamezungumzwa hapa na mwandishi mmoja anasema hivi; "*older men declare a war but it is the youth that must fight.*" Vijana wa Wizara ya Kilimo wanajitahidi kupambana na jambo la sukari na bahati mbaya sana nimesoma *political science,* wanasema "*The most peripheral countries zinakuwa driven by events.*" Watanzania ni wasahaurifu, juzi tu hapa walikuwa wanapiga kelele ya sukari lakini hakuna Mbunge alikuwa anaenda kufanya mkutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mabadiliko ya sheria...

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya sheria haya yana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga naomba uketi.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilinde... maslahi ya nchi.

**MWENYEKITI:** Naomba uketi.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Taarifa mzungumzaji.

**MWENYEKITI:** Hii ni Taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Sanga zisizidi mbili.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Taarifa mzungumzaji, ni katika Bunge hili hili Serikali imeongeza bajeti katika Wizara ya Kilimo hususani katika *component* ya umwagiliaji. Sasa nataka nimpe Taarifa kwamba tunavyoongelea umwagiliaji tunaongelea kupanua mashamba makubwa ya miwa ili tuweze kuzalisha sukari za kutosha ili tuwe na malighafi na tuzalishe hapa nchini. Tutengeneze ajira, tunavyoongelea kununua sukari nje tunaongelea kutengeneza ajira Brazil na maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga unapokea, Mheshimiwa Sanga naomba uwe na uvumilivu.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajui anachokizungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga sijakuruhusu.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajui anachokizungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga uketi tafadhali. Zima *microphone*, Mheshimiwa Sanga unapokea Taarifa ya Mheshimiwa Anatropia?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei, kwanini sipokei sisi sukari yetu kwenye hivi viwanda Mheshimiwa Rais analinda kabisa ajira na viwanda vya Watanzania. Nataka nikwambie kinachofanyika *simple* tu, Kilombero inafanya

*expansion* sasa hivi ni Serikali hii imeruhusu, Kagera imefanya *expansion* ni Serikali hii inaruhusu na Watanzania wako huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokizungumzia viwanda tulivyonavyo havina utoshelevu wa uzalishaji wa sukari, kwa hiyo, Serikali hii kwenye kupambana huwa inakuwepo na hilo *gap sugar* inawaruhusu waagize sukari ya nje. Kuwapa kibali waagize sukari nje wale watu wanavificha vibali mfukoni mwisho wa siku bei ya ndani inapanda. Watu kama hao unawaruhusuje waonewe huruma kwenye suala kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe jambo moja suala la sukari ni *sensitive*, ni usalama wa nchi, naipongeza Serikali kuleta mabadiliko ya Sheria lazima tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa hiki anachoenda kukifanya. Hatuwezi kuruhusu *monopolization* ya soko, hatuwezi kuruhusu *monopolization* ya soko ya watu saba ambao wanakaa mkakati. Nakupa tu mfano mmoja watu wanaotetea hawa watu walipewa tani 15,000 waagize sukari wameleta tani 2,300 ndani ya miezi sita sukari haipo nchini ili bei ya ndani ipande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wapo Tunduma wanaona sukari kutoka Zambia inatoka inakuja kwa bei nafuu wapo Kyela wanaona sukari kutoka Malawi inakuja kwa bei nafuu Tanzania tunaumiza watu wetu unaenda kuwatetea kwamba hawa watu wafanye nini? Hii tunaita sukari ilikuwa jela sasa tunataka kuiokoa sukari yetu iweze kwenda kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali na ninalishawishi Bunge yoyote anayepinga mabadiliko ya Sheria maana yake anasema nini? Maana yake anasema sukari iendelee kupanda bei kwa sababu hawa watu tunawaruhusu waendelee kuagiza sukari kidogo ili sukari bei ya ndani iweze kupanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliombe Bunge, iungeni mkono Serikali kwenye ajenda ya sukari, Mheshimiwa Rais amenuia kuishusha bei ya sukari kwenye Taifa letu. Hatuwezi kukubali watu wachache wa-*monopolize*.... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** ...soko na hizi nguvu wanazozitumia huko nje kwenye *media*, hizo nguvu wanazotumia kushawishi tuzikatae tutetee maslahi ya Taifa letu,...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:**....tuwatetee Watanzania, ninawatetea wana Makete waliopo Bulongwa waliopo Ipelele waliopo Lupila wanaopambania nchi yao na siyo kitu kingine kile.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nampongeza Mheshimiwa Waziri, nakupongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango songeni mbele tupo tayari kuwakingia kifua na Mheshimiwa Rais amekuwa aki-*intervein*...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikula dakika zangu dakika ya mwisho.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika ya mwisho, hakuna cha Taarifa hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga ahsante, Mheshimiwa Sanga nimekupa muda wa kutosha tafadhali, tafadhali, tafadhali.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na changamoto ya mbolea...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga nimekupa muda tafadhali naomba tuwatendee haki Waheshimiwa Wabunge wengine, ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Sanga.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tutambue pia uwepo wa wageni wengine ambao hawakutangazwa.

Tunao wageni 13 ambao ni watumishi wa Kituo cha Afya Engusero wakiongozwa na Katibu Mwenezi wa Wilaya ya Kiteto wageni hawa ni wa Mheshimiwa Olelekaita Kisau, kama wapo tutapenda tuwatambue, karibuni sana.

Tunao wageni wengine wawili, tunae Ashery Ayubu Majanja *Managing Director wa E-Gas Limited* na Catherine ambaye ni *Marketing* na *business manager* wote ni wa *E-Gas*. Wageni hawa ni wa Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa Sanga tunakushukuru kwa mchango wako. Tulikukatishia muda wako kwa sababu ya kutenda haki kwa Waheshimiwa Wabunge wengine ambao tumefanya hivyo pia.

Naomba nimkaribishe Dkt. Alice Kaijage na Mheshimiwa Vuma Augustine atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho asubuhi ya leo.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa uhai na pia Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umakini na umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mpango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Waziri wetu Mheshimiwa

Profesa Mkumbo, kwa kazi kubwa mnayofanya, hakika mmeleta bajeti ambayo imegusa maeneo muhimu sana kwa maendeleo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuendelea kuipa kipaumbele sekta au suala zima la rasilimali watu. Ukiangalia vipaumbele vya mpango huu na bajeti hii mojawapo ya kipaumbele chao ni kuimarisha na kuendeleza rasilimali watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, bajeti imeeleza pia kwamba maeneo muhimu ya utekelezaji wake ni pamoja na kugharamia mishahara ya watumishi wa umma. Huo ndiyo moyo wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, eneo la watumishi wa Tanzania. Toka ameingia madarakani kipindi cha miaka mitatu hakika ameendelea kujali maslahi ya watumishi *regardless* amepata kiasi gani cha pesa huko anapozunguka anatoa katika sekta zote, lakini hajawahi kuacha eneo la utumishi wa Watanzania, ameendelea kufanya na kujali maslahi yote pamoja na kuongeza ajira, sisi ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kabisa kwenye bajeti yetu pia kuna suala zima la kuongeza mafao ya mkupuo kutoka 33% mpaka 40% na kutoka 33% mpaka 35%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite sehemu ya mifuko ya hifadhi, uwekezaji katika mifuko ya hifadhi ya jamii imekuwa katika kiwango kisichoridhisha sana na tulimsikia Mheshimiwa Rais akisema wakati anasikiliza taarifa za mifuko. Uwekezaji katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii eneo la hati fungani Serikali imeendelea kufanya vizuri, inapokea faida ya 15% lakini uwekezaji katika maeneo mengine ikiwapo katika hisa za majengo na kadhalika bado uwekezaji wake siyo wa kubeza. Pia bado faida yake imekuwa ni ndogo, hivyo ninaomba nitoe ushauri kwa sababu kwenye mifuko yetu faida kuwa ndogo mifuko inashindwa kustahimili ongezeko kubwa la gharama za pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kitu kimoja, vitatu au viwili, Wizara ya Mipango mnayo kazi kubwa sana kwenye kuhakikisha tunaweka mipango stahimilivu na ya uhakika yenye tija kwenye kuwezesha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Tuisaidie Serikali, tushirikiane, hapajakaa sawasawa. Ukiona Mkuu wa Nchi anasema tunayo kazi ya kufanya Wizara ya Mipango kushirikiana na Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Bodi wanaokwenda kushauri kwenye mifuko hii zina bodi zake za ushauri. Ifikie mahala wasichaguliwe au kwenda kule kwa *position* zao kwa maana ya vyeo vyao kama ni kanuni au sheria zinasema. Tuchague watu ambao *upstairs* wapo tayari na wapo vizuri, tunao wataalamu wamesoma vizuri waingie kwenye bodi hizi. Hata kama kuna sekta au kuna taasisi inatakiwa ipeleke mjumbe mtizame kwenye taasisi nani yupo vizuri anaweza kwenda kushauri vizuri eneo la uwekezaji kwenye Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la uwekezaji kwenye mifuko yetu, tuna wawekezaji wa muda mrefu, wawekezaji wa kati na wawekezaji wa muda mfupi. Tumeona Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imewekeza kwenye uwekezaji wa muda mrefu kuna ubaya gani Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikaifanya biashara. Uwekezaji wa muda mfupi ni pamoja na *trade* ifanye biashara iuze mafuta, tuna shida kuna pesa kwenye mifuko ya hifadhi huo uwekezaji wa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna uwekezaji mkubwa ambao Mwalimu Nyerere kule, sasa hivi tuna kazi ya kusambaza huu umeme kwenye nchi yetu miundombiu ya kisasa inahitajika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikafanye biashara tunahitaji fedha. Watanzania watumishi wanahitaji mafao yao yawe yenye tija na kama uwekezaji wetu katika maeneo mengine haujafikia 15% kama uwekezaji faida kwenye hisa za Serikali kuna haja ya kuongeza nguvu na kuangalia maeneo mengi ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kumwamia Mheshimiwa Rais mifuko imefilisika yeye afanye nini? Ametuweka pale tuweze

kumsaidia. Tuwe wabunifu tutafute fedha tumesha-*mess up* huko nyuma, lakini tunayo nafasi ya kutengeneza. Hivyo nashauri Mheshimiwa Waziri wa Mipango unayo kazi kubwa ya kufanya eneo hili la uwekezaji kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili ile taswira nzuri ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameanza nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa Tanzania nimebahatika kwenda kwenye halmashauri za pembezoni za mikoa kadhaa wanampenda Mheshimiwa Rais, wanamshukuru sana ila wanalalamika kwenye mafao na mafao haya hatuwezi kutoka kama hatutawekeza vizuri tukapata faida ambayo itasaidia mifuko kuwa stahimilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice, ahsante sana tunakushukuru. Mheshimiwa Vuma Augustine.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kupata nafasi hii na mimi ya kuchangia kama mchangiaji wa mwisho kwa *session* ya asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza niseme wazi kwamba naunga mkono hoja kwa sababu ya kazi kubwa ambayo imefanyika Jimboni Kasulu Vijijini. Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli mkono wake tunauona mpaka chini hela zinashuka mpaka vijijini na miradi inaonekana inavyotekelezwa wananchi wanaona na sisi viongozi tunaona, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hongera sana sana kaka yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda moja kwa moja kwenye mchango yangu na mchango wa kwanza nataka nigusie kidogo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu namna ya ukusanyaji wa *VAT* kutoka kwa wafanyabiashara ambao kimsingi ndiyo mawakala wa kukusanya hizo fedha kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo utaratibu ambapo wafanyabiashara wengi hasa ni *suppliers* wanavyokuwa wame-*suppliers* vitu hasa Serikalini kwenye taasisi mbalimbali za Serikali ili waweze kupeleka madai yao lazima watoe *invoice,* lakini pia watoe *EFD receipt,* waambatanishe kwa ajili ya kwenda ku-*claim* madai yao waweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shida inatokeaje, mfanyabiashara akishatoa risiti ya *EFD, TRA* anarekodi kwamba amefanya mauzo, kwa hiyo mwezi ujao tu anaenda kudai hela kwa mfanyabiashara. Wakati mwingine hata hamjawasiliana anapeleka *demand notice* benki ili wakamate hela ambayo umekusanya *VAT* wakati kule ambapo Serikalini ame-*supply* vitu hata hela yenyewe hawajamlipa. Ninyi ni mashahidi na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni shahidi, malipo kwa *suppliers* wa ndani inaenda mpaka miezi sita, mengine mpaka mwaka mzima lakini *TRA* ukishatoa tu risiti mwezi ujao wanaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wengi wanafanya *general supplying* kwa mikopo, mtu amepata kazi, ana-*supply* kwenye taasisi moja ya Serikali labda *tender* ya bilioni tano anaenda benki anaomba mkopo, anapewa *facility,* ana-*supply* vitu kwa mkopo anategemea umlipe kwa wakati aweze kulipa benki abaki na faida kidogo. Unakuta *VAT* labda ni bilioni moja, wewe unaenda kukamata bilioni moja ambayo hata kwenye *account* wengine haipo ana milioni 200 yake au milioni 300 unakamata, hii Hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utaratibu tuweke vizuri kuwepo na *communication.* Mimi nadai Serikali halafu Serikali inakuja kunidai tena kupitia *TRA* hela ambayo sijalipwa yaani sijai-*collect,* hiyo *VAT* sijalipwa na Serikali, lakini *TRA* wanataka *that money 18%.* Kwa hiyo, naomba hilo jambo kidogo kuwepo na mawasiliano tutaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza sana mchango wa mashirika ya umma kwenye pato la Serikali bado haujawa mkubwa, ipo namna ambavyo tunaweza tukafanya, lakini hasa mwarobaini mkubwa ni kurejesha ule Muswada wa Sheria ya

Uwekezaji ambao ulitakiwa uje Bunge lililopita, haukuja. Lazima tuweke utaratibu wa kuwajibisha Bodi na Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali ili waweze kuwa *serious* kwenye kufanya majukumu yao, tuwapangie *KPIs,* tuwawekee malengo waweze kufanya kazi vizuri. Nakuhakikishia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kama ule muswada ukirudi tukaupitisha maana yake ulipita katika Kamati yetu na tukaujadili vizuri, unaenda kuwa mwarobaini wa kuongeza mapato ya Serikali kupitia mashirika ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeshauri pia mambo ya Kitaifa tukitaka kuyazungumza tuyape kipaumbele, nataka niguse kidogo kwenye suala la sukari, sukari tatizo lake ni nini hasa kwenye nchi yetu? Moja ni upatikanaji wake, lakini mbili bei kubwa maana wakati mwingine inauzwa kama bei ni kubwa, lakini inapatikana yaani upatikanaji wa sukari Tanzania hautabiriki kila mwaka utasikia sukari hakuna, sukari haitoshi mpaka wakati mwingine mwenye duka hawezi kukuuzia kilo mbili atakwambia chukua kilo moja mwingine achukue kilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni bei, sukari inaenda mpaka shilingi 7,000, shilingi 10,000 kwa kilo. Sasa ukiangalia haya yote ni *so artificial* yaani ni *cartel* tu fulani hivi, ni watu wachache wanakaa wanakubaliana tuweze kufanya sukari isipatikane moja, lakini mbili tuweze kufanya sukari ipande bei, *why?* Hii *scarcity* ni *artificial* kwa sababu haiwezekani, sukari unaambiwa Tanzania haipo, lakini Kenya ipo, Uganda ipo, Malawi ipo unaambiwa Tanzania haipatikani, tena watu wanapanga foleni. Unajiuliza sisi tupo kisiwani, halafu ukihoji utaambiwa unajua hili jambo ni zito, sukari kuipata duniani ni kazi, haiwezekani kuipata kwa kila mtu, Kenya wameipata wapi, Uganda wanaipata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *they are doing it* makusudi kwa sababu wanajua kwenye *formula* za biashara *supply* ikiwa ni ndogo *price* inafanyaje, inakuwa kubwa, wanafanya makusudi. Tuliwahi kukutana nayo Bodi ya Sukari kwenye Kamati, tukahoji kwa nini sukari inakuwa ni ngumu kupatikana, wakatupitisha kwenye utaratibu mzima wa kuagiza sukari tukaona kuna tatizo. Lazima tufanye mabadiliko na sisi tukasema kama Kamati lazima tufanye mabadiliko ya uagizaji wa sukari ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wapo watu wanajenga hoja wanasema tusijikite kwenye kuagiza sukari kwa sababu eti tunavyo viwanda vya ndani, ni uongo mtupu. Kabla ya kufanya maamuzi ya Bodi ya Sukari itoe vibali kiasi gani sukari iagizwe, inakaa *technical team* ambayo inapiga hesabu inajua *gap sugar* yaani mahitaji ambayo viwanda haviwezi kuzalisha ni kiasi gani. Baada ya kujua hiyo *gap* wanashirikishwa wazalishaji, sisi tumeongea na Bodi ya Sukari kwenye Kamati yetu, halafu baadaye wanawapa vibali wale wazalishaji wenyewe waende na wao kwa sababu wanajua wakiagiza sukari siyo kwamba sukari yao itakosa soko yaani ile *market portion* yao haiguswi kama mahitaji ya sukari ni tani 550,000 nadhani kwa mwaka wao wanataka laki tatu, laki mbili lazima waagize nje. Kwa hiyo, ukileta tani 200,000 haiwezi ikaharibu ili soko la tani 300,000. Hakuna kiwanda kinachouawa hapa, ila ni *cartel* ambayo inatengenezwa tu ili sukari isipatikane Tanzania, halafu *then price* iweze kupanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hongereni sana, nimeona kwenye *Finance Bill* tunaenda kubadilisha utaratibu. Lazima tuweke utaratibu mzuri, hii ni nchi yetu sote, haiwezi nchi ikashindikana kwenye jambo hili. Sukari ni neno ambalo kwa Watanzania ni maumivu makubwa sana na ni kila mwaka miaka yote tangu tukiwa wadogo sukari *is a problem* kama vile magendo, magendo ni kama dawa za kulevya, *no thank you*, sukari inapatikana vizuri Brazil, inapatikana nchi mbalimbali, inapatikana Dubai na ndiyo maana *intervention* ambayo Serikali imefanya *last time* juzi hapo baada ya hawa wazalishaji kusema kwamba sukari haipatikani Serikali ikaagiza tani zaidi ya 50,000 imepatikana wapi? Maana walisema haipo imepatikana wapi? Na ndiyo ikatuokoa kutoka shilingi 10,000 mpaka sasa hivi imekuwa shilingi 2,800. Sasa anakuja mtu tena bahati mbaya wakati mwingine ameaminiwa na watu, amechaguliwa na wananchi, yaani wewe unataka Kasulu Vijijini wanunue sukari shilingi 10,000? Unataka Jimbo la Kisesa pale Mwanza wanunue sukari shilingi 10,000 kwa kilo? Unataka Mlale wanunue sukari kwa shilingi 10,000? *No thank you.*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vuma endelea. Mheshimiwa Musukuma ulishapata nafasi ya kuomba Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijatoa, mimi sijatoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vuma tafadhali.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, haya mabadiliko yatasababisha na yatatusaidia *availability* ya sukari katika nchi yetu iwe ya uhakika na Watanzania waondokane na hayo maumivu makubwa ambayo wameyapata miaka yote, lakini *affordability* ili iweze kununuliwa katika bei ambayo haiwaumizi Watanzania wa kawaida hasa ambao kila wakati wanagombanishwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo makundi mbalimbali ikija mwezi Mtukufu Waheshimiwa Mawaziri wote roho juu, Mheshimiwa Rais roho juu, sisi Wana-CCM roho juu sukari itakuwaje, sukari itakuwaje? Kumbe ni maslahi ya watu wachache, we *should say no to this and* hii lazima ifike mwisho. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hongereni Serikali kwa maamuzi mazuri ambayo mmefanya na tunaamini kwamba itaenda kufanya vizuri, *NFRA* watafanya kazi yao vizuri lakini pia huo ukiritimba yaani *bureaucracy* ikikoma, tunaamini Watanzania watakuwa wametuliwa mzigo mzito ambao wameubeba kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vuma ahsante sana kwa kuchangia ndani ya muda.

Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa shughuli zetu za leo asubuhi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili pamoja na Waheshimiwa Naibu Mawaziri ambao mmekuwa mkipokea hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa utulivu mkubwa.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana wote ambao tumepata nafasi ya kuchangia kwa niaba ya wananchi, lakini pia kwa niaba ya Wabunge wengine mmepata fursa ya kutoa mawazo na ushauri kwa Serikali na mmeitumia hiyo fursa vizuri. Niwaombe radhi wale ambao tumepata changamoto ya muda wakati wa kuchangia tutajitahidi kwa kadiri inavyowezekana kutoa muda wa kutosha, lakini niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge tujitahidi sana kuwa ndani ya zile dakika kumi ambazo tunapata tuelekeze hoja zetu zile za msingi mapema zaidi ili tuweze kuendana na muda.

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporejea tutakuwa na wachangiaji watano wa mwanzo nitawatamka, lakini na wengine ambao wapo kwenye orodha ambazo zimeletwa na vyama vyetu vya siasa.

Waheshimiwa Wabunge, mchana tutaanza na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, halafu atakuja Mheshimiwa...

Samahani tutaanza na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, atafuatia Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani wajitahidi kuwahi ili tuweze kwenda pamoja saa 11.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja za Serikali; tunayo Hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na Hoja ya Waziri wa Fedha. Nilishawatamka Waheshimiwa Wabunge watano ambao tutaanza nao mchana huu na kwa sasa nitawataja watatu, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ndiye atakayeanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza jioni ya leo niweze kuchangia hoja mbili zilizoko mbele yetu. Kwanza kabisa naanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyofanya kazi kwa kweli, sisi Watanzania tunasema mama anatutendea haki, zaidi tunamuombea mama aendelee kuchapa kazi na tunamtia moyo kwamba, kazi anaiweza na Watanzania tutaendelea kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango pamoja na wasaidizi wao

wote wa Wizara husika kwa namna walivyowasilisha hoja za Wizara hizo hapa mbele yetu. Kwa kweli, hotuba zao zilikuwa nzuri, zilizoshiba na mimi naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza moja kwa moja kuchangia kwamba, sisi Watanzania tunategemea kilimo kama uti wa mgongo. Watanzania wengi ni wakulima na tunategemea kilimo kwa kila kitu, unapozungumzia kilimo kwa Watanzania maeneo mengi, hasa wakulima wadogowadogo wanategemea kilimo kwa kila kitu. Mkulima anategemea kilimo, kwa ajili ya kusomesha, mkulima anategemea kilimo, kwa ajili ya mahitaji yake ya nyumbani na mkulima anategemea kilimo anapoumwa, ataenda hospitali kwa kutumia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki ndio wakulima wanavuna, lakini jambo la kusikitisha ni wakulima wanalia kwa sababu, bei ya mazao iko chini sana. Katika maeneo yetu leo gunia la kilo mia moja linauzwa shilingi 35,000 mpaka 50,000, kitu ambacho ni kilio kwa mkulima yeyote kwa sababu, gharama tunayotumia katika kilimo ni kubwa ukilinganisha na gharama ya kwenda kufanya mauzo. Kwa hiyo, mkulima anapata hasara badala ya kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilituahidi hapa wakati wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwamba, watakwenda kufungua vituo vyetu vya *NFRA*. Mimi naomba jambo hili liende kwa haraka sana kwa sababu, mwaka jana wakulima walipata faida kwa kuuza mazao yao kwa kuanzia shilingi elfu themanini na sita mpaka elfu tisini na nane kwa sababu, waliuza kwenye vituo vyetu vya *NFRA*, lakini kwa sasahivi hali ni mbaya. Mkulima anapoenda kuuza gunia shilingi elfu hamsini, hela haitoshi hata kwenda kulimia kwa jembe moja la kwanza. Kwa hiyo, unaona ni kwa namna gani wakulima wanaendelea kurudishwa nyuma. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali itupie jicho suala hili, hasa kwa wakulima wadogowadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilisoma Bajeti ya Wizara ya Fedha, ukurasa ule wa 126, Waziri amesema kwamba, watatoa

unafuu kwenye ushuru wa forodha katika zao la ngano. Ni jambo jema kwamba, ushuru unapungua kutoka 35% kwenda kwenye 10%, sio jambo baya, lakini tuangalie wakulima wetu wa ndani hali yao itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu, mwaka jana wakulima walipata hasara sana, hasa wakulima wa ngano. Wapo wakulima kama *Ngano Limited* aliteketeza tani elfu tano kwa kukosa soko, zao lile liliharibika. Sasa tukienda kwa *style* hii kwamba, wanaoleta zao kutoka nje *automatically* watauza kwa bei ya chini na huyu wa ndani amelima kwa gharama kubwa anapoenda kuuza kwa bei ile ya chini atapata hasara. Kwa hiyo, yeye atataka kuuza kwa bei ya juu ili apate faida, sasa zao lake litanunuliwa na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba kwa mpango huu wa Wizara mliokujanao waende kuwaangalia pia wakulima wetu wa ndani, ili na wenyewe waweze kujinyanyua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa makusanyo mazuri ya kodi, lakini pia, naweka angalizo, ukusanyaji wa kodi kwa sasa ulivyo hauna uwiano. Leo walipaji wazuri wa kodi ni watumishi, asilimia mia moja watumishi wanalipa kodi, hakuna namna wanaweza kukwepa, lakini wako wafanyabiashara hawalipi kodi na ukiangalia hakuna uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mtumishi wa Serikali ameajiriwa, analipwa shilingi 400,000 kwa mwezi analipa kodi vizuri, lakini wapo wafanyabiashara kwa siku ana uwezo wa kuingiza shilingi elfu ishirini, huyo kwa mwezi tunakadiria kwamba ana uwezo wa kupata shilingi laki tano, halipi kodi. Kwa hiyo, nasema tu kwamba, Wizara iangalie namna ambayo itaweza ku-*balance* kwamba kila Mtanzania anaweza kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kurahisisha ukusanyaji wa kodi. Sasahivi tunategemea ukusanyaji wa kodi kwamba, wale wafanyabiashara ambao wanatakiwa kukusanya kodi wanategemea mashine ya *EFD*, zile mashine, hata hapa Bungeni tukitaka tufanye utafiti, twende kwenye

maduka kumi, maduka saba utakuta wanakwambia mashine zimeharibika, maduka matatu ndio unakuta wanatoa risiti. Tunadai risiti, lakini mashine zimeharibika, mtandao uko chini, hao wote ni wakwepaji wa kodi. Wakati mwingine huwa tunaenda kuwaonea wafanyabiashara, mashine zinaharibika kweli. Je, wanapata *service* wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, ndani ya Mkoa wangu mimi, unatoka Wilaya ya Kiteto, Wilaya ya Babati, Wilaya ya Hanang mpaka Wilaya ya Karatu unaambiwa mashine ikiharibika *service* anaenda kufanyia Arusha. Huyu mfanyabiashara afunge duka atoke Kiteto aende mpaka Arusha akafanye *service,* ametumia shilingi ngapi kwenda? Amekula wapi? Amelala wapi? Kwa hiyo, naomba Wizara irahisishe upatikanaji wa huduma za mashine ya *EFD* kama kweli, tuko *serious* katika kukusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hilo halitoshi wafanyabiashara hawa wanapotumia zile mashine za *EFD* wakati mwingine wanapata changamoto, hata upatikanaji wa zile mashine ni wa shida kwa hiyo, mimi naomba Wizara ibuni namna nyingine. Aidha, hata kwa kutumia simu watu walipe kodi, watumie *printer* kulipa kodi. Sasahivi mambo ya kutoa risiti, ukienda *super market* kubwa hapa nchini hakuna namna unaweza kudai risiti, risiti wanatoa bila hata kudai, lakini kwenye maduka yetu hawatoi kwa sababu, utaratibu wa kulipa kodi haujawa uzalendo kwa kila Mtanzania. Kwamba, mtu anakupa risiti pale unapomdai, usipomdai hakupi, huo ni utamaduni ambao Watanzania bado hatujajijengea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iangalie namna ya kuharakisha kuona hizi mashine za *EFD* zinapatikana maeneo yote kwa urahisi. Hata zile kampuni ambazo zina-*supply* hizi mashine ziwafuate wafanyabishara kwenye maeneo yao, lakini gharama zile za utengenezaji na *service* ziondolewe, ili zinapoharibika zitengenezwe badala ya mfanyabiashara kuona uchungu kwamba, anaenda kutengeneza mashine kwa shilingi 80,000. Kwa hiyo, naomba sana Wizara iliangalie hili, ili walau ulipaji kodi uwe rahisi kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nilisoma kwamba, kuna faini imeongezeka kutoka shilingi milioni nne mpaka shilingi milioni 15. Mimi naomba hii Wizara iliangalie upya kwa sababu, kiuhalisia ni jambo gumu sana kulitekeleza. Mfano, leo unataka kuniambia mtu ambaye hajatoa risiti anatakiwa kulipa shilingi milioni kumi na tano kwa kosa la kutotoa risiti. Mfanyabiashara huyo unakuta duka lake lina thamani ya shilingi milioni 10 tu halafu wewe unamdai shilingi milioni 15 kama faini, hili jambo muliangalie kwa sababu, halina uhalisia. Tuweke faini ambayo kila Mtanzania anapofanya kosa anakuwa na uwezo wa kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishukuru Serikali yangu, naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitutengea shilingi bilioni 5.4, kwa ajili ya kujenga soko la kisasa la Tanzanite. Nasema masikitiko yangu mpaka sasa ni ujenzi wa lile soko unasuasua kwa sababu fedha hazijapelekwa mpaka sasa, tumepewa shilingi bilioni 3.3, kwa ajili ya kujenga lile soko. Kwa hiyo, naomba Serikali itupelekee fedha ili kukamilisha huu ujenzi wa soko kwa sababu wafanyabiashara wetu wa *Tanzanite* wamekosa imani, wamepata hofu, hawana amani tena kwa sababu wanajua soko lile haliendi kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* ya mwisho ni suala la umeme. Sisi kule Mkoa wa Manyara umeme umekuwa na tatizo kubwa, hasa kwa Wilaya ya Hanang ambao wanatumia *line* moja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua dakika zimeisha kwa hiyo, naiomba sana Serikali itupelekee *substation* pale Hanang kwa sababu, umeme ukikatika *Babati line* unakatika mpaka Hanang, vijiji vyote vinakuwa havina umeme mpaka Mbulu. Kwa hiyo, naomba sana *substation* ikajengwe pale, ili Watanzania na wananchi wote wa Hanang waendelee kupata huduma za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza kabisa napenda kuanza kwa kuishukuru sana Serikali yetu, Serikali ya Awamu ya Sita, iliyo chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anayafanyia kazi maoni yetu sisi, kama Wabunge. Hiyo inatupa ari ya kuendelea kuishauri Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, wakati tunajadili Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 nilisimama hapa Bungeni nikaishauri Serikali ianze kutoza kodi ya huduma za kidigitali, yaani *Digital Service Tax* na Serikali iliichukua agenda hiyo. Sisi hapa Bungeni tulilipitisha jambo hilo na kati ya mwezi Julai, 2023 mpaka Aprili, 2024 Tanzania tumeweza kukusanya kodi kiasi cha shilingi bilioni 12.6 kodi ambayo awali ilikuwa haikusanywi. Kwa hiyo, naendelea kuipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo tumeona hata katika bajeti hii ambayo tunaijadili hivi sasa inakwenda kujielekeza zaidi katika namna ya kuboresha malipo na uchumi wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo napenda nianze kwa kuishauri Serikali, kama kweli nia ni hiyo na tayari tumeshaanza kuona matunda, naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha/Benki Kuu, iweze kuruhusu malipo ya *paypal.* Maana haiingii akilini kwa nini, malipo ya *paypal* yamezuiliwa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti Kuu hii ya Serikali ya mwaka 2024/2025 na kwa kuzingatia muda, mimi napenda nijikite katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea kukuza uchumi wa Taifa letu ni lazima tuone ni namna gani tutatanua wigo wa walipa kodi. Nimeshasema mara kadhaa hapa ndani ni lazima Serikali ije na jitihadi za makusudi kabisa za kurasimisha sekta isiyo

rasmi. Katika kila shilingi kumi ambayo inazunguka katika uchumi wetu shilingi sita mpaka saba ipo katika sekta isiyo rasmi. Wakati umefika sasa kama ambavyo tunaisikia Serikali, kama ambavyo tunasikia Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Fedha waweke mazingira wezeshi kwa ajili ya wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa Serikali iweke jitihada za makusudi kabisa kuweka mazingira wezeshi, kwa ajili ya biashara ndogo kuweza kufanyika hapa nchini. Bila ya kufanya hivyo tutaendelea kuzunguka bila kupata jawabu kamili kwa sababu, ni lazima turasimishe sekta isiyo rasmi, lakini ili kufanya hivyo ni lazima tuwavutie wale ambao wako kwenye sekta isiyo rasmi, waone umuhimu wa kurasimisha biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi hapa nawasilisha ombi maalum kwenda kwenye Shirika letu hili la *BRELA*. *BRELA* ianzishe dirisha maalum, kwa ajili ya kusajili biashara zisizo rasmi bila ya gharama. Iwe kama ni moja ya kichocheo, kwa ajili ya hizi biashara ziweze kurasimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba, ni lazima tuje na mfumo ambao utaweza kupima utekelezaji wa hii mipango na bajeti yetu. Ni lazima tuwe na mfumo ambao utaimarisha nidhamu ya utekelezaji kama ambavyo awali tulikuwa tuna *Big Result Now,* si lazima tuchukue hiyohiyo, lakini tunaweza tukajifunza kutoka pale tukachukua baadhi ya mambo yaliyoko pale tukaborsha mfumo, ili tuwe na mfumo ambao utaimarisha nidhamu ya utekelezaji katika bajeti zetu pamoja na mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurejea, wakati tunajadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka 2024/2025 nilisimama hapa Bungeni nikaiomba sana Serikali tunapokuwa tunatawanya fursa za uwekezaji na maendeleo katika Taifa letu la Tanzania tuhakikishe maeneo yote tunayafikia, tukiwemo sisi wa mikoa ya pembezoni. Niliongelea kwa upekee Mkoa wangu wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kuwasilisha ombi maalum, ombi la kipekee. Sisi pale Bukoba Mjini tuna machinjio ambayo imechoka, tuna machinjio ambayo haiendani na usalama wa chakula, kwa maana ya *food safety*, hili jambo limeongelewa kwa muda mrefu. Kwa hiyo, mimi ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri atafute fedha, na hawezi kukosa kupata fedha, ili tujengewe machinjio ya kisasa pale kwetu Bukoba Mjini kwa sababu, miundombinu ya machinjio ya Bukoba Mjini imechoka, imechakaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika Mheshimiwa Waziri wa Afya, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu akifika kwenye machinjio ya Buoba sio ajabu akasema isiendelee kutumika kutokana na hali iliyonayo. Kwa upekee na umuhimu huo na unyeti wake naomba sana na sisi tukumbukwe, kama ambavyo maeneo mengine yamekumbukwa na kujengewa machinjio ya kisasa. Sisi Bukoba Mjini pamoja na Mkoa wa Kagera sio kisiwa, sisi ni sehemu ya Tanzania kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itutendee haki. Tunaomba sana na sisi Serikali itukumbuke, tunaomba sana Serikali itekeleze maombi yetu, tunaomba machinjio ya kisasa pale Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoelekea kuhitimisha pia, napenda kuishukuru sana Serikali. Moja ya agenda ambazo nimekuwa nikizisemea hapa Bungeni ni zao la vanila. Naishukuru sana Serikali kwa sababu, mwaka huu, mwezi huu, tarehe 18, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeita wakulima na wadau wote wa zao la vanila hapa Dodoma, kwa ajili ya kujadili upatikanaji wa soko na changamoto zake, lakini natumia fursa hii nikirejea pale kwenye umuhimu wa nidhamu ya utekelezaji. Basi naomba sana maazimio ya kikao hicho yatekelezwe, ili na sisi Mkoa wa Kagera, wakulima wetu wa vanila waweze kuneemeka na zao hili la vanila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha. Wengi tumeguswa na kifo cha mtoto Asimwe, mtoto mdogo mwenye miaka miwili mwenye ualbino. Tumesikia kauli ya Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, Serikali inakwenda kufanya nini. Natumia fursa hii, naiomba sana Serikali kwamba,

sasa wakati umefika tupate Sheria mahsusi ambayo inahusiana na ukatili wa kijinsia kwa maana ya *Gender Base Violence Act*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili Tanzania ilisharidhia kupitia *SADC,* ninakumbuka hata ukirejea *Hansard* utaiona. Wakati tunajadili Sheria za Uchaguzi na Sheria za Vyama vya Siasa Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama aliahidi hapa ndani ya Bunge kwamba, Sheria ya Ukatili wa Kijinsia italetwa Bungeni. Ni kwa kuwa na Sheria mahsusi namna hii hata yale ambayo yamepangwa kutekelezwa kupitia MTAKUWWA yataweza kufanyika. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali ilete sheria mahususi ambayo itaweza kupinga na kupambana na vitendo vyote vya ukatili kwa wanawake, wanaume, watoto na hata wenzetu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha naipongeza sana Serikali kwa kuondoa *import duties* kwenye uzalishaji wa taulo za kike kwa maana ya pedi, lakini naiomba sana Serikali kwamba, hii haitoshi, watoto wa vijijini wanateseka sana. Kwa hiyo, naomba watafute namna ya kupunguza gharama, kwa ajili ya taulo za kike, hususan kwa watoto wa vijijini. Mwaka jana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba alituambia kwamba, wataweka kwenye Mpango wa *TASAF* kwa wale wanafunzi ambao wako kwenye kaya za *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa nafasi hii na ninasisitiza kwamba sisi Wananchi wa Bukoba Mjini tunahitaji machinjio ya kisasa kwa sababu sisi siyo kisiwa na sisi tunataka tujione kwamba na sisi ni sehemu ya Tanzania. Kwa hiyo, niombe sana Bukoba Mjini tupate machinjio ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana na naunga Mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema, tunakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, wajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Bajeti hii ya Mpango. Vilevile nimpongeze Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango kwa kutuletea bajeti moja ambayo inaweza ikakidhi mahitaji ya wananchi. Vilevile nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii nataka niseme kidogo, tunakwenda kwenye uchaguzi mwakani na Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Rais pekee atakayetoa matokeo makubwa ya kura ndani ya chama cha CCM. Kwa hiyo, tuwambie tu wale jamaa ambao wanapigapiga kelele kule nje kwamba Mheshimiwa Rais hana mpinzani ndani ya nchi hii. Kwa kazi ambazo amezifanya na anatufanyia inabidi na ni lazima tumpe *salute* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia uchumi, lakini tunapozungumzia uchumi inawezekana ikawa kwenye mipango yetu tunakuwa na mipango mizuri sana, lakini kwenye utekelezaji kunakuwa na tatizo. Leo ukiangalia Kusini mwa Tanzania, tunazungumzia kule Mtwara na Lindi, sisi tuna Mto Ruvuma. Tunazungumza kilimo ndiyo uti wa mgongo, kilimo ndiyo Wizara ambayo inapata bajeti kubwa kwa sababu Rais ameamua sasa kuwabeba wakulima ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kwenye mpango sijaona jinsi gani hii mito ambayo ni kubwa, Mto Ruvuma sasa hivi maji yote yanaingia baharini lakini tukiwa na *scheme* za umwagiliaji mimi nadhani hata vijana wetu ambao wako kule *idle* hawana kazi za kufanya tukawatengenezea mazingira, tayari tutakuwa na nguvu kazi ambazo zinaweza kujiajiri. Kwa hiyo niombe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hili nalo mlizingatie na mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kuhusu suala la sukari na kwenye kipengele hiki nataka nizungumze kwa uchungu sana. Mimi nilishawahi kutoa *document* na kumpa mkubwa mmoja, nikamweleza jinsi gani tunavyodhulumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hizi na viwanda vyetu hivi vinavyotengeneza sukari, leo wanatoa sukari na *delivery note* lori zaidi ya nne, tano na kwa siku wanatoa lori zaidi ya 30 kwenda kwa mawakala. Zinavyofika kule kwa mawakala zinaingia *godown*. Wakala anauza sukari kupitia *godown* kwa *delivery note* na ina kwenda moja kwa moja kwenye duka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu tuangalie hapa ndipo tunapopoteza fedha za kutosha lakini klule kwenye kiwanda kuna watu wa *TRA* wako mule ndani. Leo nimshauri tu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, katika viwanda vyetu ambavyo vinazalisha sukari inawezekana siyo lazima sisi Wabunge tupige kelele hapa lakini inawezekana *TRA* wakajua kuanzia Januari mpaka Desemba gari ngapi za sukari zimetoka kwenye kiwanda "A" na zimekwenda wapi? Leo mkitoka moja kwa moja mkaenda Dar es Salaam mkasema wakala ni fulani amepokea gari 100, hebu tuangalie kodi yetu sasa ya gari 100 ambayo amechukua Mtibwa iko wapi? Hapo ndipo tunapoibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaibiwa fedha nyingi sana. Sasa hao wakubwa, ukiuliza unatafuta mapambano. Leo ukiangali huku *Dodoma Hotel* kuna watu wenye viwanda huko wako huku wanawashawishishawishi Wabunge hapa. Baadhi ya Wabunge wanawaita wanawashawishi lakini nashukuru sana kwamba, Wabunge sasa hivi wamekuwa ni Wabunge wa kuwatetea wananchi na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza dhana ya uchumi, sisi Mtwara mmetujengea *airport* kubwa sana. Tunamshukuru Rais kwa kutoa fedha nyingi sana kwa ajili ya *airport,* lakini Mtwara hatuna ndege na kama Mtwara hatuna ndege, juzi yametokea mafuriko tumeomba ndege *Air Tanzania* wametupatia ndani ya mwezi mmoja, inasikitisha. Ndege hizi mnazoziona za *ATCL* ni fedha za korosho. Kwa nini wana Mtwara wasifaidike? Mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana katika mfuko wetu ambao tuliuweka wa fedha za korosho zikachukuliwa na Serikali kwenda kununua zile ndege sisi tunasema ni jambo zuri sana, lakini kwenye keki ya Taifa inatakiwa kila Mtanzania apate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tiketi ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara ni zaidi ya shilingi 600,000 siyo *go and return,* unakwenda mara moja shilingi 600,000 *Precision*. Sasa mimi nataka niseme, tufike mahali kama tuna mipango ya nchi basi tusiangalie kwenye eneo moja na haya nimekuwa nazungumza sana. Sisi Mtwara tuna shida ya umeme lakini tumshukuru sana Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, alivyoingia amepambana kweli kweli mpaka sasa hivi tumetoka kwenye ile shida ya umeme. Bado umeme ule hauna *guarantee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna gesi, gesi ile imetoka Mtwara imekuja Dar es Salaam Kinyerezi inatengeneza umeme ambao umeingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Kwa masikitiko makubwa sana tunatakiwa na sisi Wana-Mtwara tuingizwe kwenye Gridi ya Taifa tufaidike na ile gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana tukazungumza na mipango hapa lakini hakuna mpango ambao tusiojadili fedha. Siku zote nilikuwa nazungumza kwenye Bunge hili nikawa nawashauri Mawaziri wenye dhamana kwamba, twendeni sasa tukajenge Daraja la *Mozambique* – Mtwara ambalo litachukua *distance* ya kilometa 100, tunaingia sasa *Mozambique*. Hili halihitaji Profesa wala mtu mwenye *degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Dangote anauza *cement* Mbeya, Katavi, anashindwaje kwenda kuuza *cement* Msimbo na Playa? Kwa hiyo, kama tutafika tukafungua mpaka wa Mtwara, tukazungumza na watu wa *Mozambique* na kwa bahati nzuri wenzetu wa *Mozambique* wameanza kutengeneza barabara ya lami kilometa 15 kutoka Msimbo na Playa wanakuja Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka nishauri, Waziri Fedha, Waziri wa Mambo ya Nje na Waziri wa Ujenzi kaeni mzungumze haya. Mimi namshukuru Waziri aliyepita aliweka *token* ya kutafutia fedha. Hata hivyo, *token* imewekwa toka mwaka 2022/2023 hakuna kinachoendelea. Sasa tusizungumze mipango bila kuwa na mipango ya kutafuta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka nizungumze tena, tunapozungumza suala la sukari kwa kweli linasikitisha sana. Sisi tuna viwanda hapa lakini katika Nchi za Kiafrika, wananchi wanaonunua sukari kwa bei kubwa katika eneo lao ni Watanzania. Sisi tunapakana na *Mozambique*, tunapata sukari ya magendo ya Mozambique kwa shilingi 2,200. Sasa sikatai kama tunataka tuvi-*handle* viwanda vya kwetu lakini je, hivi viwanda vya kwetu Tanzania pamoja na kuwa vinalipa kodi vina masilahi gani kwa Watanzania? Vilevile, tuwanaangalie wananchi wetu kwa sababu leo ukisema sukari imepanda bei, kesho utasema unga umepanda bei. Maudhi ya vitu hivi kupanda bei yanakuja kwa Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuombe nimshukuru Mheshimiwa Bashe, hiyo sheria inayotaka kuletwa sisi tunaisubiri tuipitishe ili tuendele sasa na mambo mengine ili wananchi wetu wapate unafuu wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa ni hayo naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtenga, tunakushukuru kwa mchango wako. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, atafuatia Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na mwenzake katika kuhakikisha kwamba wametuwasilishia Taarifa ya Bajeti na Taarifa ya Mpango ambayo imesheheni mambo mazuri na sasa inakwenda kuwa mkombozi kwa wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikoa ambayo imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na mvua ambazo zimeendelea ni Mkoa wa Lindi. Mkoa wa Lindi mvua imenyesha zaidi ya miezi mitano mfululizo. Kwa hiyo, hali ya miundombinu katika Mkoa wetu wa Lindi ni mbaya sana. Madaraja yamekatika, hakuna mawasiliano

kati ya kijiji na kijiji, hakuna mawasiliano mazuri kutoka wilaya moja kwenda nyingine ni shida tupu katika barabara zetu za Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Waziri wa Fedha azingatie. Ninajua kwamba Mheshimiwa Rais ana mapenzi makubwa na ametenga fedha nyingi ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kuboresha barabara zetu ili sisi Watanzania tuendelee na maisha mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana fedha hizi zitakapopatikana mara moja zije Lindi kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba tunarejesha miundombinu yetu ya barabara ili Wananchi wa Mkoa wa Lindi waendelee kufanya kazi zao kwa amani lakini waendelee kufanya kazi zao za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri Bashungwa kwa sababu alikuja kwa haraka kuja kusaidia ili walau kuwafanya Wana-Lindi waendelee kupata huduma mbalimbali. Sisi Wana-Lindi hatuna bandari, hatuna ndege ambayo tunaona tukishindwa kusafiri kwenye barabara yetu tutasafiri kwa njia nyingine. Kwa hiyo, njia tunayoitegemea ni barabara peke yake. Kwa hiyo, barabara ina umuhimu mkubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi. Kwa hiyo, ujumbe huu Mheshimiwa Waziri wangu wa Fedha aupokee kwa sababu Mheshimiwa Bashungwa hana neno, yeye akipelekewa fedha mambo yanakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Fedha, mmesimama vizuri katika kuhakikisha kwamba mnaendelea kusimamia mapato ya nchi yetu. Tunajua kwamba tunajimwambafai (kujitutumua/kujisifu) humu ndani kuelezea mafanikio, lakini kwa sababu ya fedha ambazo nyie mmezisimamia kuzitafuta. Tunawashukuru sana Mungu awabariki. Hata hivyo, nitumie nafasi hii kuwapongeza ndugu zetu wa *TRA* kwa kazi kubwa wanayofanya, lakini bado wanatakiwa kuongeza jitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ambayo yanayoendelea ambayo siyo mazuri sana. Tunajua kwamba nchi yetu tuna wakulima, wafanyabiashara na wafanyakazi lakini niseme tu kwamba wananchi wengi wamewekeza katika biashara ndogondogo. Vilevile, zipo changamoto ambazo zinaendelea katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulipa kodi siyo vita bali kulipa kodi ni uzalendo. Pia kila Mtanzania anayeshiriki katika kufanya shughuli za kiuchumi na shughuli za kiuzalishaji ni muhimu sana na ni wajibu wake kulipa kodi. Niseme tu kwamba, mambo ambayo ndugu zetu *TRA* wanaendelea kuyafanya wanataka kuturudisha nyuma. Sisi tunasonga mbele wao wanataka turudi nyuma na ndiyo maana nasema kwamba kulipa kodi siyo vita, ni suala la watumishi wa *TRA* kukaa na kutoa elimu kwa wafanyabiashara ya namna ya kuweza kushiriki kulipa kodi bila kutozwa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba zipo mashine za *EFD* ambazo zinatumika lakini wakati mwingine zinaharibika na maeneo ya kwenda kutengeneza kwa haraka hakuna. Kwa hiyo, huduma hiyo inawezekana ikakosekana kwa wiki moja au wiki mbili. Sasa kodi inayokuja ambayo anakadiriwa mfanyabiashara yawezekana anakadiriwa kiwango kikubwa tofauti na mauzo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yanayoendelea siyo mazuri sana kwa sababu wafanyabiashara wengi wamekuwa na malalamiko. Hakuna mahusiano mazuri kati ya watumishi wa *TRA* na wafanyabiashara. Nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa sababu alifanya kikao na wafanyabiashara pale Dar es Salaam na anajua changamoto mbalimbali ambazo wamemwelekeza na sasa wanasubiri kuelekea kwenye utekelezaji wa kupunguza zile changamoto za wafanyabiashara ili wafanyabiashara wa Tanzania waweze kufanya biashara zao kwa amani na waweze kulipa kodi bila kushurutishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kuna suala la uwekezaji wa Mradi wa *LNG*. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa mradi huu, kwa sababu

Mradi huu umekuwa wa muda mrefu lakini Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira ya dhati katika kuhakikisha kwamba anatamani mradi huu utekelezwe. Ninajua kwamba Serikali iko katika hatua mbalimbali ya utekelezaji wa mradi huu lakini Serikali nayo kupitia Wizara ya Nishati mmekaa muda mrefu hamjasema chochote kinachoendelea. Wananchi wa Tanzania na Wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara wanatamani kusikia juu ya utekelezaji huu wa *LNG*. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapo-*windup* atueleze ni kwa namna gani tunakwenda katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendelee kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu amewekeza fedha nyingi katika Mkoa wetu wa Lindi na amewekeza fedha nyingi katika eneo langu la Lindi Mjini. Miradi mingi imetekelezwa, leo tuna shule za sekondari za kutosha, vituo vya afya na hospitali za wilaya. Sasa niiombe tu Serikali kwamba kwa sababu mpango huu tumetoka nao katika mwaka huu wa 2023/2024, miradi ambayo haijatekelezwa niiombe Serikali sasa ni wakati wa kutoa fedha ili wananchi wetu wa Lindi waweze kupata huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu tunayo changamoto katika miradi ya maji. Miradi mingi ya maji haijakamilika na sasa tunakwenda kwenye robo ya mwisho ya mwaka. Niliomba kupitia Wizara ya Maji mtuletee fedha tukamilishe miradi ya maji ili wananchi wetu waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mji wetu wa Lindi uliathiriwa sana mvua nyingi, ninapoongea hapa leo kuna mgonjwa mmoja ana shida ya kipindupindu pale Lindi Mjini kwa sababu ya kukosa maji safi na salama. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba fedha za miradi ya maji zinakuja Lindi Mjini kwa ajili ya kutekeleza miradi ili wananchi wetu waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niwatakie kila la kheri Wizara ya Fedha katika kuhakikisha kwamba tunaendelea kufanikisha ukusanyaji wa mapato kwa

changamoto ni nyingi na mahitaji ya Watanzania ni mengi. Nikushukuru sana, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ahsante sana kwa mchango wako. Sasa nimwite Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii ya Serikali tunapohitimisha Bajeti Kuu ya mwaka huu wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze pia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa wasilisho zuri na bajeti nzuri ambayo Wabunge wenzangu waliochangia kabla yangu wameonesha sehemu nyingi ambazo wameridhishwa nazo. Vilevile, niipongeze sana Serikali kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri ya utekelezaji wa Bajeti iliyopita. Tunapokwenda kuhitimisha bajeti hii kwa utekelezaji wake mwezi huu wa sita na kuanza bajeti mpya, tunaamini kasi ile ile itaendelea na tutaendelea kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kulikumbusha Bunge lako Tukufu juu ya mchango ambao niliwahi kuutoa na nitaurudia tena juu ya kufananisha au kutoa mfano wa familia ya Kisukuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baba yangu Mheshimiwa Kiswaga na Mheshimiwa Njalu watanielewa ninaposema, ukiwa na watoto wengi kwenye familia ya Kisukuma ndiyo unaonekana tajiri zaidi. Hii ni kwa sababu watu ni mali. Ukiwa na watoto wengi maana yake ng'ombe wako watajaliwa kwa wakati, utalima eneo kubwa zaidi kwa wakati, utavuna kwa haraka na kwa wakati. Kwa maana yake wingi wa watu ni *asset*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii takwimu za mwaka 2022 za sensa zinaonyesha kwamba Taifa hili bado ninaweza nikasema ni Taifa kijana kwa sababu zaidi ya 70% ya Watanzania kwa maana

ya wananchi wa nchi hii ni vijana, kwa hiyo Taifa letu bado ni changa kwa hiyo tuna uwezo wa kutumia uwingi huu kama *asset* kuipeleka mbele nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Itakushangaza wewe na Bunge hili Tukufu kwamba bado tunajadili changamoto ya ajira wakati duniani wanapomaliza kujadili changamoto ya *climate change*, mabadiliko ya tabia nchi changamoto ya pili wanayoijadili ni *global labor shortage*. Kuna changamoto ya ukosefu wa watumishi duniani, lakini Tanzania tunaongelea ukosefu wa ajira, tena changamoto hii ni kubwa kiasi cha kwamba tayari mataifa yanakutana kuanza kujadili namna gani tunakwenda kuongeza zaidi matumizi ya Sayansi na Teknolojia ili kupunguza changamoto hii, lakini sisi tuna watu tumekaa huku tunawaelimisha, tena niipongeze sana Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi katika juhudi zake za kufuta ujinga, ujinga umefutika watu wana elimu na wana ujuzi lakini lazima tuangalie kwenye mipango yetu, tunapangaje kutumia changamoto iliko duniani ya *global labor shortage* kama fursa kwetu sisi kupunguza changamoto yetu ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano mdogo, *USA* imeanza kuwa na changamoto hii ya *global labor shortage* kuanzia miaka ya *early* 2000 na kila mwaka wana-*register* pungufu ya asilimia tatu kwenye watu wake wanaondoka kazini. *As we speak,* kwa mfano kwenye sekta ya afya, wana upungufu wa zaidi ya manesi milioni kumi lakini wamesha-*register* manesi zaidi ya laki sita ambao wanategemewa kuacha kazi ifikapo 2027, hiyo ni kwenye *healthcare peke* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *manufacturing globally* kuna upungufu wa watu zaidi ya milioni nane wanaohitajika na hizo ni sekta mbili tu nilizozitolea mfano. Sisi huku tuna *workforce* ya kutosha, vijana wenye nguvu, wana ari na uwezo wa kufanya kazi, Balozi zetu zinatumia vipi Diplomasia ya Uchumi anayoijenda Dkt. Samia Suluhu Hassan kila siku duniani kuhakikisha tunaondoa changamoto hii? Nadhani kuna jambo la kufanya *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza mzungumzaji aliye….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sijakukaribisha. Mheshimiwa Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampongeza mzungumzaji anaongea vizuri lakini pia naomba na mimi nitoe tu kwa mchango wake kwamba sasa hivi Dunia ajenda kuu kama siyo kuu lakini ya kati ni ajira Ulaya, ni ajira Afrika. Kwa hiyo, watumishi upungufu wa ajira katika dunia ni mkubwa na upungufu wa ajira Afrika ni mkubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kamani umemsikia au nimruhusu arejee tena?

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia.

**MWENYEKITI:** Unapokea Taarifa ya Mheshimiwa Boniphace Getere?

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana siipokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozunguza taarifa ninazozitoa hapa ni za kitakwimu na ni takwimu ambazo zimethibitishwa na nchi husika kila mwaka zinatoa ripoti za kuonesha ni namna gani zina upungufu mkubwa sana wa watumishi kwenye maeneo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitumia fursa hii hatutapunguza tu changamoto ya ajira kwa vijana kwenye nchi yetu lakini tutaongeza mapato kwa njia ya *remittance*. Profesa Kitila utanielewa kwamba kuna nchi sasa hivi Afrika hii ya kwetu zinaingiza zaidi ya dola bilioni 20 za mapato kwa mwaka kama *remittance*, kama fedha zinazotumwa na watu wake walioko nje kuwatumia familia zao na watu wao walioko kwenye nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tutaongeza fedha za kigeni kwenye nchi zetu, tutapunguza utegemezi na mzigo mkubwa kwa Serikali kuhudumia watu ambao hawa-*produce* chochote. Hili mimi naomba sana Profesa Kitila anapokuwa kwenye utaratibu wake wa kutengeneza sasa mpango wa mpaka 2050 tuangalie namna gani tunatumia diplomasia ya kiuchumi. Mtaji mkubwa sana ambao ametutengenezea Dkt. Samia Suluhu Hassan kupunguza changamoto hii lakini kuongeza mapato na fedha za kigeni kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili nitauelekeza kwenye bajeti yetu ya Serikali ambayo tunayo hapa mezani. Pamoja na kuipongeza sana Serikali kwa makusanyo yake mazuri ambayo kwenye *graph* zake inaonekana inapanda kila mwaka, kwa namna ambavyo *TRA* inakusanya mapato kutoka kwa wafanyabiashara na watu mbalimbali lakini bado hatujafikia viwango ambavyo vinastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kwamba kwa *developing countries* kima cha chini au *average* ambayo mara nyingi tunakusanya kama mapato ya ndani kwa watu wetu ni 15%. Leo hii sisi japokuwa tumetoka mwaka uliopita tuna 12.6% na mwaka huu tunatazamia kukusanya 12.9% kama mapato ya ndani, lakini bado hatujafika hata ile *average* ambayo inaweza ikatusaidia sasa kutoa huduma Serikali kwa watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitakwimu ili Serikali iweze kuhudumia watu wake vizuri kwa kutumia fedha na mapato yake ya ndani kwa kujitegemea, lazima *TRA* ianze kukusanya kuanzia 40%. Sasa *research* zimeshafanyika hasa kwa nchi ambazo

zilikuwa na hali mbaya kabisa za *single digit* za makusanyo yake mpaka wamefika zaidi ya 40% wamechukua hatua kadhaa na mimi niishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni kupunguza wingi wa kodi. Tuangalie namna ya kupunguza wingi wa kodi na punguzo hili tutakwenda kuli *compensate* kwa kuongeza wingi wa walipakodi. Tunapopunguza wingi wa kodi tunaondoka kero kwa wananchi na kuongeza hamu yao ya kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine *World Bank* imeonesha kwamba ni muhimu Serikali ikajenga uaminifu kwa watu wake, sisi kwwenye nchi zetu zinazoendelea watu wengi wanafanya kazi za nguvu sana ili kupata vipato vyao. Watu hawana shida na kulipa kodi, shida ni kutaka kujua kwamba matumizi ya fedha wanazolipa kuingia Serikalini zinakwenda sehemu sahihi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitatoa tu *reference* ndogo kwa ripoti ya *CAG* ya mwaka jana ambayo amewasilisha Machi mwaka jana, ripoti inasema; "vyanzo vya mapato ambavyo havikukusanywa bilioni 61, ushuru wa huduma usiokusanywa bilioni 4.1 kutowasilishwa kwa makusanyo na mawakala waliokusanya bilioni 5.6 ushuru wa mazao usiokusanywa bilioni 5.2 lakini ukusanyaji usioridhisha katika vyanzo vikubwa bilioni 6.8." Hizi ni chache tu ambazo nimezinukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema nini? Tukipunguza upotevu au kutokukusanywa huku kwa fedha kunaongeza imani ya watu kulipa na hivyo kutaongeza makusanyo, suluhu pekee ni kuhakikisha tunaondokana na *cash economy*. Lazima tuondoe fedha za makaratasi kwenye mzunguko wetu, na ni lazima pia Serikali itoe elimu kwa watu kwamba kuwa na mashine ya kukusanyia haimaanishi kwamba ndio unakatwa kodi, kama wewe kisheria hustahili kukatwa kodi utaonesha *zero,* lakini kule Serikali itasoma kwamba kuna *transaction* fulani zimefanyika. Tujenge utamaduni wa kuondoa fedha za makaratasi kwenye mizunguko yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali imeweza na niipongeze kugawa pikipiki kwa Maafisa Ugani wote nchi nzima, tunatenga bajeti za kugawa fedha za magari kwa Halmashauri zetu na Mikoa yote nchi nzima, ninaiomba na kuishauri Serikali iangalie namna kila anayefungua biashara wapewe vile vifaa vya kukusanyia malipo yao kwa kadi, watoe vile vifaa bure, hiyo itakuwa ni *investment* ya kutusaidia sisi kutoka kwenye 12% tulizonazo leo kwenda kwenye 40% ikiwezekana 50%. Fedha ambazo zinalipwa leo hii na Serikali haijui zimelipwa ni nyingi kuliko kawaida zaidi ya 80% ya *transaction* kwenye nchi hii zinafanyika na Serikali haijui zimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya *transaction* zote ziwe zinapita kwenye mashine, mabenki yapunguze viwango vya makato ili kila mtu anayelipa alipe kutumia kadi. Kwenye nchi za wenzetu kadi ni kitu cha kawaida na mtu ukitoa fedha kulipia kitu unaonekana wa ajabu, kwamba huyu mtu anatoaje fedha? Kadi ni kitu cha kawaida na Serikali haipati shida kukusanya kodi zake kwa sababu inajua *transaction* zote zinazofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali iangalie hii kama *investment,* itafute hivyo vifaa kugawa kwa kila mtu benki zetu wawe wadau wakubwa wa maendeleo watoe kadi kwa kila mtu ili hata anayelipia hata kama ni 1,000 lipa kwa kadi kusiwepo na gharama za makato, Serikali itajikuta inakusanya kodi kadri inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia takwimu zinaonesha hata fedha zinazokuwa-*printed* na Serikali….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru dakika moja.

**MWENYEKITI:** Naomba hitimisha.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazokuwa *printed* na Serikali na ndiyo sababu pia na Serikali huwa inabadilisha fedha kila baada ya muda, kwa sababu inapo-*print* fedha baada ya muda fedha hazionekani kwenye mfumo, watu wanatunza fedha ndani lakini tukiondoa *cash economy* hakuna fedha itakayobaki ndani, Serikali itaona fedha zake zote 100% zilipo, tutakusanya mapato na nchi hii itaweza kuhudumia huduma zote bila kutegemea vyanzo vingine isipokuwa vyanzo vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, labda ku-*complement* tu kwenye hoja ya Mheshimiwa Ng'wasi Kamani na nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha umeonesha kwamba umeichukua hoja yake.

Waheshimiwa Mawaziri mnapata nafasi ya kusafiri pia inatupa *challenge* kama Watanzania yawezekana vijana wetu wako kwenye *comfort zone* sana, ukienda hata nchi tu za *U.A.E* utakuta madereva, wanaofanya kazi *Airport* na maeneo mengi ya huduma wanatoka nchi za jirani ikiwemo Kenya lakini wanatoka nchi zingine za India na Ufilipino lakini huwakuti Watanzania, labda sijui watanzania tupo *very comfortable* hapa ndani? Ni *challenge* kwetu lakini pia Serikali mtafute namna ya kuwaongezea ujuzi Watanzania na ujasiri wa kwenda kupambana nje.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Kamani. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatia Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na baada ya hapo atakuja Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Fedha pamoja na Mpango wa Taifa na mimi nigusie pale alipomalizia Kamani hapa kwenye *dollarization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeshauri najua Wizara ya Fedha imefanya kazi nzuri sana na inaendelea kupambana sana na *inflation* na inaonekana lakini ijitahidi zaidi ipambane na *black market*. Huku benki tunasema ni 2,690, elfu mbili mia sita na ngapi, wanakuambia hakuna chukua 500, 300 huko nje ni 2,800 mpaka 2,850 ili tu-*stabilize* zaidi, tunao uwezo huo kwa sababu ni kitu kidogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe kuwe na *special consideration* kwa watu ambao bidhaa zao zote wanazo-*deal* nazo zinatoka nje. Mathalani watu wanaochukua tenda Serikalini halafu wana-*order* vitu nje, halafu vinachukua muda kufika, vilevile Serikali inachukua tena muda kuwalipa, sasa waki-*deal* na hela ya ndani tu bado wataenda kupata shida. Kwa hiyo hayo maeneo mawili matatu yakiwekewa mkazo hapo kwenye dola tutakuwa tumekaa vizuri lakini nakubaliana kabisa na lile wazo la Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana Wizara zote mbili kwa ujumla kwa eneo la wakandarasi. Nimeona ule ukurasa wa 54 wameonesha nia ya kuhakikisha wakandarasi wazawa ambao wanapata *sub contract,* inapotoka *interest* na wale wazawa nao wanapata ile *interest*, hilo ni jambo zuri sana. Ameongeza *stake* ya wakandarasi wazawa kwenye kazi ni jambo zuri sana tumelipigia kelele mara nyingi niwapongeze sana, niombe tu sasa tuangalie pia namna ya kuweka *interest* hata kidogo kwa wakandarasi wazawa kwa malipo yanayochelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba maeneo mengi yamekaa vizuri yako maeneo ambayo ninashauri Serikali i-*consider* kuyarekebisha. Eneo la kwanza ni ile faini ya kutokutoa risiti ambayo iko ukurasa wa 100 pale ambayo ni ile Sheria Namba 86(1). Unajua jinsi unavyoweka ile kodi ya juu au faini ya juu unatoa mwanya wa wale wanapiga ile kodi ku-*negotiate* ili walipe ile ya chini halafu wapate hapo cha juu. Kwa hiyo, mwisho mzigo utaenda kumdondokea mfanyabiashara wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuliangalie milioni 15 ni nyingi sana kuna maduka ambayo yanatumia *EFD* na milioni 15 ni

*almost* mtaji wake hata kama *turn over* ni kubwa, sasa ukimwambia faini ni milioni 15, *TRA* wana mtindo wa kwenda kwenye ile ya juu ili mrudi mezani muongee na mkiongea pale unaona kabisa wana chochote ili warudi kwenye ile ya chini naomba tuliangalie sana hilo na ninaongea kama mtu ninayetoka kwenye jamii ya wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ninapowashauri Serikali waiangalie ni eneo la ile tozo kwa magari yanayotumia gesi. Haya magari bado ni machache, *motive* yetu ni kutia nguvu au kuwasaidia magari yawe mengi, haya magari wanafanya *modification* kule nyuma unakuta wameweka mtungi wa gesi hakuna hata sehemu ya kuweka begi, sasa ikiwekea tozo ya shilingi 382 kwa kilo tayari unaanza ku-*discourage,* kwa sababu menzake yeye ana nafasi huko nyuma na huu mzigo ukimwangukia hawataona ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa sababu Rais anataka *clean energy* kwenye kupika *definitely* tunaenda kwenye *clean energy* kwenye magari pia. Ni afadhali ihamishiwe kwa sababu kwa sasa hivi miaka mitano ijayo magari ya umeme yatakuwa mengi, ni heri tuihamishie kwenye magari ambayo tunayaagiza ya umeme na *hybrid* ili tuweze kulinda hawa wa gesi kwanza, watakapokuwa wengi hiki chanzo kitakuwa na tija, lakini kwa hawa wachache ambao wako Dar tu ukawarundikia shilingi 382 naona ni nyingi sana, tuangalie hata 150 ili na wao waweze kupambana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nirudi eneo la *road fund*, barabara ni siasa, barabara ni maisha, barabara ni maendeleo. Tumekuwa tunawalalamikia sisi hapa wote Wabunge Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi kwamba barabara hazijengwi na nini lakii tunajua kile kikapu chetu kikoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaushauri kwamba ni vizuri tuangalie namna ya kuimarisha mfuko ule, ndiyo sehemu ya kwanza ya kuanza, kwanza tuanze tuhakikishe ile hela yote inayokatwa kwenye maeneo yote iende yote kama ilivyo isiguswe. Wanasema sijui ni *ring fencing* kuna kiingereza chake,

sasa ni vizuri yaende kwa sababu barabara kwa kweli itatusaidia sana kuharakisha maendeleo na tu *aim* juu zaidi siyo *two trillion* ambayo wamependekeza twende mpaka 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo barabara za muhimu na zina maslahi kwa uchumi na zitapata watu. Tuende kwenye *PPP* na zile *road toll* kwa mfano ile barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro ya njia sita tukaweka *road toll* hatujamzuia mtu kutumia hii ya kawaida kama ana haraka lakini maana yake tunamsaidia yule mwenye haraka kama kenya walivyoweka ile barabara ya haraka kutoka Mlolongo kwenda mpaka *Westland,* inakusanya hela na ile hela inaendelea kuingia kwenye Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo ningeomba sana *toll roads* na *PPP* inaweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la kuangalia kwa hara, hela inayokatwa kwa ajili ya *REA* tumeshapiga hatua kiasi gani kwenye *REA*? Si karibu tunamaliza vijiji vyote? Hatuwezi kuipunguza pale kwenye *REA* tukaongezea hapo kile kipande kilekile bila kuongeza kwa wananchi kikaenda kusaidia kwenye mafuta? Kwa hiyo nadhani kitasaidia kwenye barabara *Road Fund* ikawa ina hela hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo ambalo ninapenda niishauri Wizara ya Ardhi na hii ishirikiane na Wizara ya Fedha. Watanzania wote hata mwenye kupata kipato cha shilingi laki moja wanajenga nyumba *cash* na kama wanajenga nyumba *cash* na nyumba ni *security* akiingia kazini akipata mwanya wa rushwa atakula, mwanya wa kuiba atakula kwa sababu *security* ya kwanza ni kupata nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusirejeshe ile *housing bank*? Mtu akiingia kazini asaini mkataba kama ana kiwanja apate mkopo wa miaka 20, 30 wa kujenga nyumba apate amani na aheshimu kazi yake kwa sababu akiacha hiyo kazi tayari nyumba itauzwa, tuingize pale ili hiyo hela inayobaki mkononi kwa mtu kama tuna *housing bank* itumike kwenye maeneo mengine, ifanye uchumi wetu uchangamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga nyumba *cash* kwa kweli ni gharama sana na hela nyingi inaenda karibu vitu vyote ambavyo vinatoka nje. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri sana tufikirie namna ya kuwa na Tanzania *housing bank* hasa kwa wale ambao wana maeneo yaliyopimwa na wana hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iachane na biashara haiwezi, iachane kabisa na biashara, iendelee kutoa huduma. Kuna kiwanda kimejengwa pale Moshi cha Karanga *Leather* imeingizwa bilioni zaidi ya 100 na ni hela hiyo hiyo ya wastaafu *NSSF* sijui *PPF* Serikali ilikuwa inaleta viatu hapa pea moja moja imeshashindwa hata ile pea moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hauwezi kuwekeza Kiwanda cha Ngozi cha namna ile uendeshe kwa mtu ambaye anateuliwa hajawahi kuona Ngozi inatengenezwaje zile mashine ni za kisasa kabisa. Tuuze share 51% tubaki na 49%, kama ilivyo *TBL* kama ilivyo *TPC* na mashirika mengine walete hela wafanye kazi na tena iwe ni *export* kwa sababu kiatu kitakachotengenezwa pale kwa sababu mashine zile ni za leo za Italy za dunia ya leo kile kiatu hakiwezi kuwa bei rahisi sawa na mtumba unaotoka pale Kiboriloni road.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutengeneze au kama tukiamua kama hatutaki kukitoa tena kwa watu ili kilete hela za kigeni basi tuanze kupitisha sheria ya kwamba majeshi yote ya ndani yatumie viatu kutoka pale ambao sasa tunavunja tena ile nia halisi ya kuwa na soko la ushindani na hii ni kwa viwanda vyote Serikali haiwezi kusimamia kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kiwanda ukiuliza matatizo waliyonayo sasa hivi wanataka bilioni 10 *working capital* kwa nini? Mshahara wao hautokani na kazi wanayoifanya, hela ya *NSSF* imekaa pale, Magereza wamekaa pale, tuwape watu wenye uwezo watengeneze viatu kama inavyotengenezwa pale *EPZ export* sisi tupate hela na tuweze kutoa soko la ngozi na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni hata kile kiwanda cha sukari cha Mkulazi hatuwezi mimi najua, kile kiwanda cha *TPC* kilikuwa

cha kwetu tukatengeneza wenyewe mwisho wa siku tukaanza kubadilisha kila kitu, tukashindwa! Tumerudisha mpaka sasa hivi kinatoa gawio kwa Serikali. Kwa hiyo, nashauri hata kile cha Mkulazi tutafute wadau tuwauzie *share,* tubaki na *share* zetu za maana, ajira itokee na ufanisi uwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la *SGR,* sijasikia kabisa *SGR* inakuja lini Kaskazini. Sasa *purchasing power* ya Kaskazini ni kubwa. *Purchasing power* ya Kaskazini hata hizo za *luxury* ni kubwa sana. Tuleteeni *SGR,* ianzie Dar es Salaam – Tanga – Kilimanjaro iende Arusha – Manyara mpaka Musoma iende itokee huko. Kule kuna *purchasing power* kubwa. Nina uhakika tutaweza kufanya marejesho kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo ambalo linahusu utumishi na nilishaliwasilisha mara kadhaa. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kwa kuboresha huduma za afya. Pale Moshi tuna KCMC ambayo ndiyo hospitali ya kanda, *super specialist.* Sasa hivi tuna *deal* na kansa, tutaenda kwenye kitengo cha moyo wameshakipatia fedha na tunaenda kwenye kufungua ubongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shida tunayopata, *salary scale* yake haifanani na Bugando na haifanani na Muhimbili. Maana yake ni nini? Mfanyakazi kuliko abaki pale, *super specialist,* anaona mazingira mazuri zaidi aende Bugando au aende wapi. Hilo ni suala la kurekebisha tu ili hizi huduma zitolewe kote kwa usawa na sisi tuendelee kuwahudumia wananchi wetu vizuri. Tayari uwekezaji ni mkubwa, naomba sana Serikali ifikirie namna ya kuweka *salary scale* ambayo inafanana kwa hizi *super specialist hospitals.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni vizuri Wizara hii ya Mipango ifanye kazi kwa uchungu kama mtu binafsi, kama mchaga au kama mpare kwa maana ya kwamba, haiwekzekani kuna mradi Serikali imepeleka shilingi bilioni saba ujenzi wa stendi ya Mfumuni. Halmashauri imeshindwa ku-*negotiate.* Shilingi bilioni saba imekaa pale chini na kile ni chanzo cha mapato kwa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa kuwafata *CRJE*. Hawa watu wakubwa walioko hapa, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa *Professor* Kitila wakienda *CRJE* ambao mnawalipa kwa miradi mingine mkawaambia, bwana tuna *interest* na hili eneo kwa sababu hela imekaa chini muda mrefu tunaihitaji ili iongeze mapato Moshi na iingie Serikalini warudi *site* wamalizie ile stendi imebaki kiasi kidogo sana. Tunatenga fedha, lakini tunashindwa kupata wakandarasi kurudi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante muda wako umeisha.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi kabisa naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi na Mheshimiwa Jackson Kiswaga ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nashukuru sana kwa kupata hii nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na siku ya leo hapa tupo tunajadili maendeleo ya Watanzania wenzetu kwa niaba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, natoa shukrani kwa Serikali. Nafikiri tulipokuwa katika Wizara mojamoja tuliishauri Serikali vitu vingi na Serikali imekubali na imepokea vitu vingi ambavyo sisi tunaviona. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali yetu hii sikivu. Tunampongeza na tunamshukuru sana Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutusikiliza Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyokuwa tunachangia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, tukasema kwamba hii Wizara imetengwa lakini sasa kwa kubadilika muundo kwamba tayari tunaona makundi maalum na masuala ya jinsia yanaenda kushughulikiwa na yatapata *solution*. Tulisema sana kuhusiana na maadili. Kwa hiyo, mama ameweka Naibu Makatibu Wakuu wawili. Kwa hiyo, hapa tunaishukuru Serikali hii inatusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulikuwa tunalia na pensheni za kiwango cha chini, kwamba ziko chini sana lakini Serikali imetusikiliza. Japo kwamba hawakusema watafanya nini au itakuwa ngapi lakini naamini kwamba Serikali inaweza ikafanya vizuri kwa kitu ambacho kinaweza kikaja kikawafanyia watu vizuri. Pia, tulisema kuhusiana na fedha za wamachinga; sasa hivi zimeshatoka ila tulikuwa tunaomba ziongezwe kwa sababu hili kundi ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo haya yanaonesha kwamba Mama Samia Suluhu Hassan ndiye mtu maarufu sana ndani ya CCM na nje ya CCM. Ndugu zangu niwaambie ndani ya CCM hatuwezi kuwa na mtu kama Mama Samia Suluhu Hassan na ndani ya CCM tunapimana kwa utekelezaji wa Ilani. Sasa ukijitokeza wewe mwana CCM ukasema labda kwamba unataka kupambana ina maana kwamba utekelezaji wa Ilani haujafana. Tumeona ametekeleza Ilani kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo twende tukatazame katika masuala ya skuli, masoko ya maendeleo, maji, umeme vijijini, barabara na katika maeneo ambayo yameigusa jamii. Wapinzani tuliokuwa nao katika Bunge la 11 walikuwa na msemo wao, "Ni kweli CCM inafanya maendeleo lakini wanafanya maendeleo ya vitu". Sasa hivi CCM inafanya inafanya maendeleo ya vitu na bado tunafanya na maendeleo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mishahara imeongezwa. Tunashukuru kwamba watu wamepanda vyeo na ajira zimetoka katika maeneo chungu nzima kama tulivyokuwa tunazipata takwimu. Kwa hiyo, hiyo inaonesha wazi kwamba ndani na nje ya CCM hakutakuwa na mtu mzuri wa kugombea Urais isipokuwa ni Mama Samia Suluhu Hassan na hapa naungana na Dkt. Nchimbi anayesema kwamba, "Mama mitano tena." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwa mwalimu. Unapotoa suala, halafu unaweka na *suggested solution* halafu unaweka na *marking scheme.* Sasa unampima mtu yale masuala yako ulitaka ajibu sababu tano yeye anakupa sababu kumi na wewe ulitaka tano. Hapo maana yake kwamba huyu mwanafunzi *right*

unayomtilia hutii kwa kinukta kimoja kimoja unapiga ile *right* moja kubwa kwa sababu amejibu zaidi ya majibu yaliyotakiwa Hivi ndivyo alivyofanya Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika *paragraph* ya 5.1 iliishauri Serikali kuwa na nidhamu ya upelekaji wa fedha ambazo *ring fence*. Mheshimiwa Tarimo amezungumza hapa, hizi *ring fence* kama hatujazipeleka kwa nidhamu nzuri ina maana kwamba moja kwa moja tunakwenda kufeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfuko wa barabara ambao ni *road fund*. Makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 906 lakini fedha zilizopelekwa ni shilingi bilioni 382, sawa na 40%. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu umekuja na mabadiliko ya sheria. Nimeona humu katika *finance bill* kwamba unataka kuweka *contingency fund* kwa ajili ya barabara wakati hizi fedha zipo na tunaweka makadirio madogo kuliko makusanyo. Kwa mfano Bajeti ya Mwaka 2021/2022 tuliweka bajeti ya shilingi bilioni 908 lakini tukapata takriban shilingi trilioni moja; hiki kiwango kilipelekwa. Mwaka 2022/2023 tuliweka bajeti ya shilingi bilioni 857 lakini tukakusanya shilingi trilioni moja, tukapeleka shilingi bilioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ina maana kwamba hizi fedha zinaenda wapi na wakati hapa tulipata matatizo na changamoto za barabara na wakati mfuko wa barabara fedha ya makusanyo makubwa ipo; hizi fedha zilienda wapi? Yale malalamiko na vilio tuliyokuwa tunalia kwa kukatika madaraja na barabara fedha si zilikuwepo? Kwa nini zisiende na hizi *ring fence?* Hili nilikuwa naomba kwamba Serikali tuwe na nidhamu. Hii imesemwa katika *page* ya 51 na Kamati, mpaka 57 wametaja mifuko yote. Kwa hiyo, hapa nilikuwa naomba tuwe na nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nazungumzia katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Juzi Mheshimiwa Dkt. Mwigulu alivyosoma hotuba yake hapa alisema kwamba katika Deni la Taifa kilichoongezeka miongoni mwao ni shilingi trilioni mbili ambazo ni hatifungani za Serikali ambazo walikubaliana na mifuko ya hifadhi lakini tumesahau kuli-*calculate* hili Deni la Taifa la Ndani, kwa sababu nyuma ya mwaka 2000 huko, kwa miaka 20 nyuma,

Serikali ikidaiwa na mifuko shilingi trilioni 5.9 na hawajaanza kuzilipa; walianza kuzilipa baada ya miaka 20. Tunaonaje zingelikuwa zimewekezwa na zikawa zinapata faida, zingekuwa ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini hatuwalipi na riba hizi fedha na kwa nini kwenye Deni la Taifa hatu-*account* hiki kitu? Kwa sababu hizi fedha ni za wananchi katika mifuko. Kwa hiyo, hili deni kama tutalitazama Deni la Taifa basi hebu tujaribu kuingiza na hiki na ndiyo maana tunaweza tukapata tabu kikokotoo kiwe kipi kwa sababu zile fedha zilizowekezwa kule nyuma hazikulipwa ndani ya miaka hiyo 20. Zingekuwepo kwamba zimewekwa na Serikali inatambua deni basi angalau lingekuwa limekaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tunazungumza kikokotoo; kusema ukweli Watanzania wengi hawajui kipi kipo katika kikokotoo. Watu walikuwa wakipokea 25%. Zaidi ya 81% ya wafanyakazi ilikuwa wanapata kikokotoo cha 25%, kikaja 33%. Kilipokuja 33% tunaishukuru Serikali kuja kupeleka kwenye 40% na wengine wakaenda kule kwenye 25%. Kinachotakiwa hebu haya mashirika yetu yatoe elimu; watakapotoa elimu watu watafahamu. Serikali inafanya jitihada na kwa upande wake imetusikiliza lakini watoe elimu. Naamini ni elimu ndiyo kilichokosekana. Kwa hiyo, hiki kama kitatolewa elimu kinaweza kikakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sasa imeamua katika *monetary policy* wamesema watatumia *interest rate base monetary policy*. Sasa wasiwasi wangu kwa mujibu wa *formula* na mataifa mengine wanavyotumia ni lazima kutakuwa kuna *changing of interest rate* katika kipindi kifupi kifupi. Serikali mara nyingi inakaa na madeni ya wakandarasi au ya watu ambao wamefanya zabuni zao kule Serikalini. Wale wameenda kukopa benki kwa kupitia fedha ambazo wameshatoa huduma Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, itakapokuwa kwamba ile *interest* ina *change* huyu atakapoanza kwenda kukopa hakutakuja kuwa na hasara na hawezi kuja kupata maumivu?

Serikali ikae ijaribu kuangalia au kama kuzielekeza hizi benki tuanze sasa mambo ya *hedging,* vinginevyo bila ya hivyo tunaweza tukaja tukaathiri uchumi wa wafanyabiashara wetu ambao fedha zao ziko Serikalini. Sasa hili napenda Serikali ijaribu kuliangalia na itakapoliangalia ije na majibu mazuri, ituambie nini kinaweza kikafanyika. Kuna athari nyingi sana, lakini moja kwa hawa watu ambao wametoa huduma Serikalini halafu wakawa wanadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze tena kutoa shukurani kwa Serikali; Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya vizuri na inajali watu. Hapa nitoe msemo mmoja; wasitokee wengine wakawa kurumbizi. Kurumbizi akitoka kwenye kichaka anaanza kusema kichaka hiki kichaka gani; kichaka hiki kichaka mavi. Usiku ukifika anarudi tena palepale anaanza kunyenyekea; Kichaka hiki kizuri; kichaka hiki kinanukia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha, ahsante sana.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, CCM kichaka kinachonukia anayeona kichaka mavi siyo CCM, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali King, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi atafuata Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Innocent Kalogeris ajiandae.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hizi nzuri tulizonazo mbele yetu. Nianze kwa kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Mheshimiwa Profesa Kitila na Naibu Mawaziri, kwa hotuba nzuri waliyotuletea; hotuba ya wananchi ambayo inaenda kumalizia pale palipobaki lakini na kuanza miradi ambayo inaenda kuchechemua uchumi wa wananchi wetu katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza watendaji wote wa Wizara hizi na makatibu wakuu kwa jinsi ambavyo wanaendelea kuwapa ushirikiano ili tuweze kufanikiwa katika nchi yetu kuweza kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kuwaletea wananchi maendeleo lakini kwa jinsi ambavyo anaendelea kuwa na maamuzi thabiti lakini kuwa na Serikali iliyo imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Neno la Mungu katika kitabu Mithali 14 linasema; "Pasipo mashauri Taifa huanguka." Ili Taifa liweze kusonga mbele lazima Serikali iwe na maamuzi na siyo sifa kuwa kwenye kiti umeaminiwa ukaogopa kufanya maamuzi kwa sababu utafanya makosa, siyo sifa. Sifa ni fanya maamuzi sahihi kwa ajili ya wananchi ili Serikali iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1975 nchi yetu ilipata uhaba wa mahindi. Mwalimu Julius Nyerere aliambiwa soko la mahindi liko kwa makaburu lakini kwa sababu wananchi wake walikuwa na... nam-*quote* Mheshimiwa Rais Nyerere alisema kwamba; "Niko tayari kwenda kununua mahindi kwa mashetani ili wananchi wangu wasife." Alificha hisia zake na alificha chuki yake ili wananchi wake wasife.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miezi miwili, mitatu tulikuwa hapa na sote tulikuwa tunapiga kelele kwa ajili ya wananchi wetu hawana sukari. Kule kwangu Muhambwe sukari ilifika shilingi 7,000. Serikali kwa kuona kwamba hawawezi kukaa kimya wananchi wao wakafa na kupiga kelele walifanya maamuzi. Nampongeza Mheshimiwa Bashe, Waziri wa Kilimo na nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa kuja na mpango na sheria ambayo itatusaidia kutoka kwenye hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari hii kwa wnanchi wetu ndiyo kila kitu. Asubuhi akipata chai yake na mihogo atakutana na mlo mwingine jioni baada ya kutoka shamba lakini muuza maandazi bila hii sukari hawezi kuuza maandazi ili aweze kupata uchumi.

Kwa hiyo, tukifanya masihara kwenye hii sukari kwa kweli hatuwatendei wananchi wetu waliotuleta humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimo humu ndani kwa sababu ya Wanamuhambwe walioniamini pamoja na changamoto kubwa ya mfumo dume lakini waliniamini wakasema nije niwatetee wananchi wangu wa Muhambwe. Leo nitawatetea wananchi wangu wa Muhambwe ili wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninavyokwambia sukari bado ni shilingi 3,500 mpaka 3,800. Kwa hiyo, kama tutakalia kimya suala hili ina maana wananchi wetu wataendelea kuumia. Nawapongeza Serikali kwa kuja na maamuzi sahihi kwa sababu maamuzi haya yatakwenda kuwakomboa wananchi wetu. Hatuna haja ya *tuition.* Kila mtu anafahamu *supply and demand* ndiyo ina *control* kila kitu...

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naungana kumpongeza mjumbe anayezungumza kwamba Serikali lazima iwe na maamuzi kwa maana kwamba haina sababu ya kuwaacha wananchi wake wanaumia. Kama hivyo ndivyo, sasa ni vizuri zaidi maadamu Waziri mwenyewe anasema kwamba wale wafanyabiashara wanaficha sukari na wanasababisha uhaba uwepo na kutokana na hali hiyo ni kwamba suala hilo limemshinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini suala hilo sasa lije Bungeni, ili tujadili na tuone namna ya kulishughulikia. Kuliko pale tunapofika maamuzi ya kusema njia pekee ya kushughulika na hao ni kuruhusu sukari ambayo haina ushuru iingie nchini wakati huo tunaendelea kupoteza mapato na tunaendelea kupoteza ajira, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Samizi unapokea Taarifa?

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa yake siipokei kwa sababu sasa hivi Serikali imeshakuja hapa na Muswada wa *Finance* tupitishe tusonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo viwanda vingi hapa nchini vinavyoleta bidhaa na viwanda hivi pamoja na kuwa vinatengeneza bidhaa hapa nchini bado tunaingiza vitu. Simenti na mabati yanaingia hapa nchini. Tuna viwanda vya vitenge na vitenge bado vinaingia hapa nchini. Sisi watu watu Kigoma tunavaa vitenge vya Congo na siku zote vitenge vinaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko njia pekee ya kuvilinda hivi viwanda. Hatuna sababu ya kutengeneza njia ya kulinda viwanda vya sukari tofauti. Kwanza ni *double standard;* kama ambavyo viwanda vingine vya nchi hii vinalindwa kwa bidhaa zinzoingizwa kuwekewa ushuru wa forodha *(import duty)* na viwanda vya sukari navyo vilindwe hivyohivyo ili kuwe na uhuru tusiwe na *monopoly* ya watu wachache ambao watakuwa wanatuamulia bei kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na naunga mkono hiyo *finance bill* ije mbele yetu tuweze kupitisha kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu lakini kwa sababu ya manufaa ya wananchi wa Muhambwe. Nimalizie kwa kusema...

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ambayo naomba kumpa mjumbe ambaye anaongea vizuri sana, si vibaya kama tutaenda kujifunza kwa majirani zetu ambao wamefanya vizuri. Nchi ya Uganda walikuwa na *shortage* ya sukari. Walichofanya ni kuhakikisha kwamba wanajitosheleza kwa

kuzalisha sukari ndani ya nchi yao na sasa hivi wa *export*. Kwa hiyo, kuna la kujifunza kwa jirani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Samizi unapokea Taarifa ya Mheshimiwa Kandege?

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa yake na naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa yote iliyopo pembezoni mipakani ndiyo mikoa inayofaidika na sukari ya bei rahisi kwa ajili ya sukari za magendo kutoka kwenye hizo nchi? Kwa nini isiwe Tanzania ambapo tuna viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuwaambia Mawaziri hawa, Joshua aliambiwa uwe hodari na moyo mkuu na muwe mashujaa. Muwe mashujaa kwa sababu leo hii tunapata nguvu ya kujadili *process* kwa sababu wananchi wetu wametulia na wana sukari. Ingekuwa leo wananchi hawana sukari kelele zile za mwezi wa pili na wa tatu hapa ndani tusingeweza kujadili. Ingekuwa ni taarifa zinaendelea humu ndani kwa sababu wote tunafahamu kelele za wananchi zilivyokuwa kubwa na wananchi ndiyo wametuamini, wametuleta hapa ndani. Tuna raha leo tunajadili kwa sababu wananchi wana sukari, muwe na moyo mkuu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, muwe mahodari Mheshimiwa Bashe, muwe mashujaa, tupo pamoja na ninyi katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata sukari ya bei nafuu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umeisha, hitimisha tu Mheshimiwa.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nihitimishe kwa kusema kwamba naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi nzuri na kwa jinsi ambavyo wanaendelea kutuletea maendeleo na sisi wananchi wa Muhambwe tuko pamoja kuunga mkono Serikali hii ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Samizi. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mjadala, lakini naomba nitoe tangazo la wageni.

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika, ni wageni 13 wa Mheshimiwa Spika kutoka Benki ya CRDB ambao ni Ndugu Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, karibu sana Mkurugenzi. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Bruce Mwile Mwasenga, Afisa Mkuu wa Uendeshaji; Ndugu Tully Esther Mwambapa, Mkurugenzi Mtendaji wa *CRDB Bank Foundation*; Ndugu Boniventura Paul Kiungo, Mkurugenzi wa Wateja wa Awali na wa Kati na Msimamizi wa Matawi; Ndugu Adimin Mwansasu, Mkurugenzi wa Uendeshaji; Ndugu Godfrey Bahati, Meneja Mwandamizi wa Uchambuzi wa Kina; Ndugu Chabu Mwishwaro, Meneja wa Kanda ya Kati, Ndugu Dennis Mwoleka, Meneja wa Kanda ya Kusini; Ndugu Jenipher Tondi, Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu; Ndugu Muhumuliza Buberwa, Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam; Ndugu Badru Iddi, Meneja wa Kanda ya Pwani na Zanzibar; Ndugu Cosmas Sadat, Meneja wa Kanda ya Kaskazini na Ndugu Jumanne Wagana, Meneja wa Kanda ya Magharibi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni wageni maalum ambao wamekuja kwa ajili ya bonanza kubwa linalotegemewa kufanyika kesho tarehe 22 Juni, 2024 katika uwanja wa Jamhuri, Jijini Dodoma. Tunawakaribisha sana wageni wetu kutoka CRDB kama ambavyo nimewatamka hapa na kesho tutakutana viwanjani. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 17 wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni kikundi cha Njombe Wanawake Madini Samia, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 86 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, ambao ni Watumishi wa Kanisa la *Church of God of Prophecy* kutoka sehemu mbalimbali nchini Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 13 wa Mheshimiwa Mavunde ambao Kikundi cha Sanaa cha Uchekeshaji cha Watubaki, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Jimbo la Mufindi Kaskazini, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati, ambao ni Wajumbe wa Baraza la Umoja wa Vijana kutoka Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge ambao ni Taasisi ya Bega kwa Bega kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Ali Hassan King, ambaye ni mtoto wake kutoka mjini Zanzibar, karibu sana kijana wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoa wa Kigoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 48 wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, ambao ni wanafunzi wa kozi ya sheria kutoka Chuo Kikuu cha Mt. Augustino cha Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kundi lingine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunaye Ndugu Rhoda Charles kutoka Capripoint Jijini Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wataalamu wawili wa maabara kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa wakiambatana na Ndugu Fahad Bagonza ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Tumbi, karibuni. *(Makofi)*

Pia katika wageni ambao tunao leo, tunaye mtoto Caren Kikoyo ambaye ni mtoto wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, karibu sana kama yupo, karibu sana Bungeni kijana wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia leo katika hoja hizi mbili zilizoko mezani. Nianze kwa kumshukuru sana Rais kwa kazi kubwa inayofanywa katika nchi hii katika kuimarisha miundombinu mbalimbali ikiwemo ya afya, barabara, maji na maeneo mengine yote katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru Mawaziri wawili ambao leo wana hoja zao mbele yetu; Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango, wameleta mipango mizuri ambayo tunaamini ikienda kutekelezwa kwa usahihi, nchi hii itapiga hatua kimaendeleo na itakuwa mahali pazuri sana pa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze kuzungumzia suala la kodi; tunazungumzia Bajeti Kuu ya Serikali na tunazungumzia upungufu wa makusanyo ya kodi katika maeneo mbalimbali. Ningependa nianze kwa kushauri katika vyanzo vingine ambavyo Serikali hii inaweza kuviangalia, kwa mfano, kuna biashara kubwa sana ambazo zinafanyika kwenye mitandao na biashara hizi ambazo

zinafanyika kwenye mitandao hazijaweza kuangaliwa vizuri. Kwa hiyo, tuwe na teknolojia au maarifa ambayo yatatuwezesha kutambua biashara mbalimbali zinazofanyika kwenye mitandao na namna gani tunaweza kupata kodi kutoka kwenye hizo biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine ambayo pia tunapoteza kodi, kwa mfano, iko miradi mikubwa unakuta inafanyika na hawa mafundi wadogo wadogo. Anaweza akachukua mradi wa shilingi milioni 100, shilingi milioni 200, shilingi milioni 300 ukafanywa na mafundi tunawaita *local* fundi, lakini Serikali haipati kodi, unaweza ukaona fundi anachukua karibu 30% katika mradi ule, lakini haziingii kwenye Serikali, sasa tufanyeje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuwe na kusajili hii miradi, mradi ukiwa pengine unaanzia shilingi milioni 30, Serikali iweke mpango wa kusajili hii miradi ili iwe na sababu ya kulipa kodi na Serikali iweze kupata mapato yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nichangie kwenye mipango ni kwenye upande wa elimu, tunafahamu kwamba elimu ni msingi na ndiyo uti wa mgongo. Nilikuwa najaribu kuangalia, tunaweza tukaweka mipango ya muda mrefu; kwa mfano, tunajua katika nchi hii tuna *reserve* pengine za madini ambazo tunaweza tukavuna kwa miaka 50 ijayo, *reserve* za gesi, mafuta na vitu vingine. Ni muhimu sana sasa tunavyoangalia vipaumbele vyetu vya elimu kwamba tupeleke watoto katika maeneo haya, twende tukawasomeshe katika maeneo haya ili sasa wakirudi watatusaidia kama nchi kufanya *exploration,* lakini tukawa na wataalamu wetu wa ndani ambao wanaweza kusaidia kuinua uchumi katika maeneo haya ambayo ni nyeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunavyoweka mipango ya muda mrefu, tuangalie kusomesha watoto katika haya maeneo kwamba katika miaka 50 ijayo tutasomesha watoto wangapi ambao baadaye watakuja kulisaidia Taifa, ni mataifa mengi yamefanya hivyo, China wamefanya hivyo, walipeleka

watoto kusoma Marekani. Japan wamefanya hivyo na sasa wamerudi kujenga nchi zao, utaona *trend* ndivyo ilivyo, kwa hiyo, hilo tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu sasa hivi imeanza kukua sana katika eneo la utalii, je, ni aina gani ya elimu ambayo tunatoa hasa katika eneo la kuhudumia wageni wetu. Sehemu hii tuko chini sana, ukiangalia katika nchi za Afrika Mashariki kwenye eneo la huduma kwenye hoteli, sisi tuko chini sana. Tatizo ni kwamba aina ya vyuo ambavyo vinatoa elimu hizi, walimu wake tunawatoa wapi? Hilo ni eneo ambalo pia lazima tuliangalie, kama tunataka kuboresha utalii ni lazima pia tuboreshe huduma kwa wale watalii wanaokuja katika nchii hii, kwa sababu mtu akija mara moja hajapata huduma nzuri ataipenda nchi, lakini ile kero tu ya huduma kesho harudi na ndiyo maana Tanzania inakuwa na wageni wengi ambao hawarudi kwa sababu ya huduma ambazo tunazitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni upande wa viwanda, tumesema kwamba tunataka kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Ni mikakati gani ambao tumefanya kutoa *incentives* kwa watu wanaojenga viwanda hasa ukiangalia kwenye maeneo ya kilimo, eneo hilo tunasema, lakini hakuna uwekezaji mkubwa na punguzo la kodi ambalo tumetoa kwa watu wanaowekeza hata kwenye viwanda vidogo vidogo. Tulikuwa na mipango ya kujenga viwanda, kwa mfano kule Mafinga kuna eneo lilitengwa Nyororo kwa ajili ya kujenga viwanda vya parachichi na *packaging*, tumeishia wapi katika hiyo mikakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta kwamba tunakuwa na mipango mingi mizuri, lakini sasa utekelezaji wake, kama tunaweza kuweka vivutio vya kodi kwenye eneo la viwanda vidogo vidogo hasa katika eneo la kilimo tutaweza kuwa na viwanda na kuweza kuvutia ajira. Sasa suala la kununua bidhaa za ndani ni lazima liwekewe msisitizo maalumu. Tunavyo viwanda katika nchi hii, kwa mfano, katika mabomba ya maji, lakini tumezungumzia hapa katika viwanda vya sukari pia. Mwenzangu amezungumzia ni namna gani Uganda wameweza

kujitegemea kwenye sukari, ni lazima wakati mwingine tupitie maumivu, tunavyotaka kutengeneza huu mchakato wa kuwa na viwanda vyetu tujitegemee, ni lazima tukubali kupitia maumivu wakati fulani ili sasa tufike kule tunakokwenda. Tukiwa na maamuzi rahisi kila wakati hatuwezi kufika, mambo mengine lazima tukubali kupitia katika mchakato mgumu ili tufike tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwenye matumizi ya fedha za Serikali, ni muhimu sana tukawa na nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Kama tunaweza kuweka fedha nyingi kwenye *OC*, kwa mfano sasa hivi unakuta kwamba mtu anaweza akafanya kongamano la shilingi milioni 300, *for what?* Kwa sababu gani katika nchi hii maskini? Mnaelewa? Kwamba ni vizuri kufanya makongamano na semina, lakini ni kwa kiasi gani tunatumia fedha kwenye haya makongamano na ni tija ipi ambayo tunaipata kwenye Taifa kama hili maskini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali ni muhimu sana ili Taifa liweze kuendelea, vinginevyo, tutakuwa tunapiga *mark time*. Hapa alizungumza asubuhi dada yangu Mheshimiwa Rose Tweve, namna tunavyotumia fedha nyingi kwenye makongamano na warsha kwenye kuelimisha malaria wakati tuna kiwanda kikubwa na kizuri pale Kibaha ambacho kinaweza kutokomeza malaria, hatuna habari, tunazungumzia habari ya kuleta chanjo za malaria wakati tuna kiwanda hapa nchini. Wakati fulani sisi kama viongozi ndiyo tunaweza kutoa dira namna gani Taifa letu linavyokwenda na linaweza kustawi kwa michango yetu na maamuzi tunayofanya, ni muhimu sana hilo tukaweza kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la kuwa na *indicators* katika kutenda kazi, *key performance areas* ni muhimu sana. Huu mtindo wa kusema kwamba mfanyakazi akikaa kazini miaka miwili, mitatu, ndiyo apande daraja siyo mtindo ambao uko kwenye *corporate world*. Mimi nimefanya kazi huko kwenye mitandao, hupandi wewe mpaka umeonesha mchango wako kwenye hiyo kampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai watumishi kupanda, lakini kila mtumishi afahamu kwamba ana mchango wake katika nchi hii. Mchango wa kuboresha uchumi na huduma za jamii, siyo tu nimekaa kwenye dawati sichangii chochote baada ya miaka miwili naanza kudai kupandishwa, hapana, ni lazima tuanze kuangalia uwajibikaji katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia habari ya uwekezaji kwenye mifuko, kwamba siyo suala geni, lakini ni wapi tunawekeza. Ukiangalia *South Africa* wanasema; "*the social security corporation is the major investor in the tourism sector.*" Kwa hiyo, uwekezaji kwenye mifuko ya jamii ni jambo la kawaida, lakini tuhakikishe tu kwamba watu wanaostaafu wanapata mafao yao, kwa hiyo, uwekezaji ni jambo la kawaida na tuwekeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naona unavyoendelea kufunga naomba tu kwamba *NEMC* kwa maana ya Baraza la Mazingira, sisi kama Kamati tumetaka iwe mamlaka kwa sababu tunataka mazingira yasimamiwe, hakuna uchumi pasipo mazingira. Kwa hiyo, jambo hili wenzetu ambao wataliangalia katika hatua inayofuata ni lazima waliangalie jambo hili ili mazingira ya nchi hii yaweze kusimamiwa na uchumi wetu uweze kuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiswaga nakushukuru. Mheshimiwa Innocent Kalogeris atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Ikupa na Mheshimiwa Emmanuel Cherehani ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu ya Wizara ya Mipango na Wizara ya Fedha. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi yetu ya Tanzania, katika kuimarisha uchumi katika sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa anayoifanya yeye na msaidizi wake, ndugu yangu Mheshimiwa Chande na Mheshimiwa Waziri wa Mipango ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila na msaidizi wake, ndugu yangu Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na watendaji wenu wote kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais ili ndoto yake na azma yake katika kuwatumikia Watanzania iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja na sababu kubwa ya kwanza ya kuunga mkono hoja, wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kulikuwa kuna suala la ujenzi wa Barabara ya Bigwa – Kisaki, kilometa 78 kutoka Morogoro – Mvuha, lakini vilevile kulikuwa kuna ujenzi wa Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere, kilometa 11 tukiwa tunakwenda Mvuha – *Matemele Junction*, kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere na Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Februari Barabara ya Bigwa – Kisaki iliwekwa saini ya shilingi bilioni 132 na *point,* lakini tarehe 7 Februari tuliweka saini na mkandarasi kujenga Barabara ya Ngerengere – Ubena Zomozi, kilometa 11. Kwa hiyo, yote haya kwa sasa hivi ninachojua wakandarasi wameshakamilisha *document,* kinachosubiriwa ni *advance payment* ili kazi ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wana-Morogoro kwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kila kitu tushakamilisha kilichobaki ni barabara tu. Sasa kusema kwamba unataka kupinga bajeti itakuwa ni kitu ambacho hakiwezekani, maana yake nakwenda kusema kwamba barabara hizi hazijengwi. Kwa hiyo, nikuombe tu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, nikupongeze kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. Kwanza, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, nianze na suala la kusikia kilio cha Kamati wakati tunazungumzia suala la fedha ya *wharfage* iendelee kubaki *TPA* na itoke kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia bandari ndiyo lango la uchumi wa nchi yetu hii na katika misingi ya kuweza kupata fedha lazima tuwe na magati mengi ambayo yataweza kusaidia kukusanya fedha. Tuliambiwa kwenye Kamati, gati moja linajengwa kwa thamani ya kati ya shilingi milioni 150 mpaka shilingi milioni 180, lakini gati moja kwa mwaka lina uwezo wa kukusanya kodi kwenda *TRA* na *TPA* karibu shilingi trilioni moja kila mwaka kwenye *wharfage* zinazokusanywa tunaweza hata kujenga magati matano mpaka sita. Ni nini maana yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa na uwezo wa magati mengi ambayo yataingiza fedha nyingi na kuweza kutusaidia kwenye bajeti ya Taifa. Ninajua kabisa, ndugu yangu Mheshimiwa Mtenga hapa, kule Mtwara kuna suala la ujenzi wa Gati la Mwigalo, gati ambalo linakwenda kusaidia kupokea makaa ya mawe na kuondokana na uchafu kwenye Mji wa Mtwara. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwa *TPA* kukaa na fedha hii wao wenyewe wataweza kufanya mambo makubwa katika bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tu kwa Mheshimiwa Mwigulu, hebu tuangalie, maana tumesema fedha hizi zitakwenda kwenye Benki Kuu na kutakuwa na utaratibu maalum wa kuzichukua. Hebu tuangalie kusiwe na urasimu kwenye kuchukua fedha hizi, ili *TPA* iruhusiwe ikafanye kazi ambayo, sisi kama kamati tumeomba, lakini Watanzania wanaomba fedha ipatikane na iingie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Sasahivi tunakwenda kwenye 90% naa, lakini katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, mimi nitaendelea kuwa mtetezi wa Wanamorogoro na Wanapwani, mpaka tunafikia dakika hii hakuna *CSR* ambayo imetoka kwenye mikoa hii miwili.

Mheshimiwa mwenyekiti, ombi langu wakati tunakuja kwenye ku-*wind-up*, hebu tuambiwe Wana-Morogoro na

Wanapwani haki yetu tutaipata vipi? Tulichoambiwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwamba, kinachotakiwa ni watu wa Morogoro na watu wa Pwani wakae na *TANESCO* na wakae na Wizara, ili kuona ni jinsi gani ambavyo fedha hii itapatikana na ni kitu gani kifanyike kwa maendeleo ya wananchi wa mikoa hii miwili? Naomba, tunapokwenda kwenye ku-*wind-up* kwenye bajeti, najua Waheshimiwa Mawaziri wengi watasema, basi tuambiwe Wanamorogoro na Wanapwani haki yetu ya *CSR* ya Bwawa la Mwalimu Nyerere tunaipata lini?

Mheshimiwa mwenyekiti, mimi nachelea, kama tutakuwa hatuna majibu yaliyokuwa sahihi basi, Bunge lijalo, sisi Wanamorogoro na Wanapwani tutaleta hoja binafsi ya kudai *CSR* yetu. Naomba tusifike huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ninapongeza, mimi ni mkandarasi naomba ni-*declare interest.* Nampongeza Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kwenda kwenye suala la kuwajali wakandarasi wazawa. Nakupongeza Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Bashungwa, Waziri wa Ujenzi, kwa kutimiza maono ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenu ni kiuhalisia kuna mambo ambayo sisi Umoja wa Wakandarasi na Watoa Zabuni tumetoa kwenye Serikali tunaomba yafanyiwe kazi. Kuna suala la *withholding tax* wanayokatwa wakandarasi na watoa huduma, ni kubwa, tunakatwa asilimia tano ya *contract,* ndani ya nchi hii hakuna biashara yoyote unayoifanya ambayo utapata faida ya zaidi ya 10%. Ni nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapopewa mkataba wa shilingi 1,000,000,000 unakwenda kukatwa *withholding tax* ya shilingi 50,000,000 wakati wewe matarajio yako ya faida ni shilingi 100,000,000, kodi ni 30%, ni shilingi 30,000,000. Serikali inachukua shilingi 50,000,000, shilingi 20,000,000 zaidi. Hapa tunawaua wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye hilohilo kuna suala lingine la maboresho ambayo tumeyaleta sisi, kama wakandarasi. Kuna suala la malipo kwa haraka, wakandarasi wengi wamefilisiwa na benki kwa sababu, wanadai Serikalini muda mrefu. Asilimia ya riba inaongezeka, wanafika mahali mali zao zinauzwa na wanafilisika kwa hiyo, naiomba Serikali katika maboresho yake, hebu iangalie kipengele cha kuona tunafanyaje kuwalipa wakandarasi kwa haraka, ili waondokane na riba ya benki na kufilisika wanaposhindwa kulipa madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, kuna suala hili la *withholding tax*, badala ya kulipa asilimia tano tumependekeza asilimia mbili, lakini kama Serilkali inaona hapo ni padogo basi, twende kwenye asilimia tatu na tuachane na suala la wakandarasi. Wakishalipa kodi hiyo ya asilimia tatu ya *withholding tax* biashara iwe imekwisha, hakuna malipo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine, kuna suala mama yetu amezungumzia la kutokurejesha nyuma kufuatilia masuala ya kodi. Bado suala hili linaendelea, sisi kama wakandarasi tumelileta suala hilo. Naiomba Serikali, hebu liangalieni, mliafanyie kazi, ili tuweze kufikia pale Mama anapotaka. Badala ya fedha kwenda nje, China au India, ibaki nyumbani, uchumi uendelee kukua na sisi tutengeneze mabilionea wengi Wakandarasi wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kwenye suala la utalii. Mimi natoka Morogoro Kusini, kule tuna hifadhi ya Mwalimu Nyerere, lakini ninachojua kwa sasa hivi ni utalii umeongezeka. Kwa ripoti ambayo tumepewa, tulikuwa na watalii 928,000 sasa hivi tumekwenda 1,800,000. Kiuhalisia sisi Tanzania tuna vivutio vingi, ukijaribu kuangalia katika dunia, Morocco wana watalii 10,000 kwa mwaka, lakini hawana vivutio vingi vya asili kama tulivyokuwa navyo Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa sasahivi tuendelee kutangaza mbuga zetu, hasa kwa ukanda wa Kusini

ambao kuna Morogoro – Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, kuna Mikumi, kuna Udzungwa, kuna Katavi, kuna Ruaha Mkuu, ili mapato yatakayopatikana upande wa utalii wa Kusini yaingie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kuongeza pesa za kigeni kwenye nchi ziweze kusaidia kuleta maendeleo katika Tanzania. Baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent. Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Cherehani. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. STELLA A. IKUPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa fursa ya kuweza kuchangia jioni hii ya leo. Awali ya yote ninaomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo ameendelea kutulinda mpaka tumefikia Mkutano huu wa Kumi na Tano na hatimaye Kikao cha 51 cha Bunge letu. Ni jambo la kumshukuru Mungu kwa sababu, wengi walitamani kufika, lakini hawajaweza kwa hiyo, tunaposimama ni lazima tumshukuru Mungu kwa sababu, ni neema tu wala siyo kama tunastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba kuunga mkono hoja ambazo ziko hapa mbele yetu, lakini pia, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa jinsi ambavyo wanasimamia Wizara zao na kwa jinsi ambavyo wanamshauri vizuri Mheshimiwa Rais wetu. Pia natumia fursa hii, kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Rais shupavu, ni Rais mahiri, ni Rais ambaye ana ubunifu ambao kwa kweli, ukikaa ukiutafakari, mpaka unashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubunifu huu na umahiri wa Mheshimiwa Rais wetu ndiyo ambao umesababisha uchumi wetu kuwa imara mpaka hivi tunavyozungumza. Dunia imetikiswa sana, lakini pamoja na kutikiswa kwa dunia uchumi wetu umeendelea kuwa imara. Kwa hiyo, ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kuendelea kumshukuru na kuendelea kumuombea kwamba, Mwenyezi Mungu aendelee kumpa maarifa na ubunifu wa kuendelea kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, uchumi wetu uko imara, lakini Serikali inapaswa iendelee kuchukua tahadhari dhidi ya vitu ambavyo vinaweza vikasababisha uchumi wetu kushuka, miongoni mwa vitu hivyo ni mabadiliko ya tabianchi. Tunaona jinsi ambavyo mabadiliko ya tabianchi yanaendelea kutikisa dunia kwa hiyo, iko haja ya Serikali kuweka mikakati ya kuona ni namna gani inakabiliana na mabadliko haya, ili yasiweze kuathiri uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Serikali iweze kuona ni kwa jinsi gani inapunguza uagizwaji wa bidhaa kutoka nje na badala yake kutoa kipaumbele kwa bidhaa ama mazao ambayo tunazalisha sisi wenyewe likiwemo zao la ngano. Yako mambo mengi, lakini kwa sababu ya muda, ninaomba niyataje hayo kwa uchache. Kwa hiyo Serikali iendelee kuangalia mambo ambayo wanashuku kwamba, yanaweza yakasabaisha uchumi wetu ukashuka, ili uchumi wetu uendelee kuwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaomba kuongelea suala la misamaha ya kodi. Kuna malengo ambayo yamewekwa kwamba, misamaha ya kodi isivuke asilimia moja ya Pato la Taifa, lakini mpaka hivi tunavyozungumza misamaha hii imekwishavuka, iko asilimia 1.3. Sasa, kwa staili hii ama kwa jinsi hii, iko haja ya Serikali kuweza kuipitia upya misamaha ambayo ilitolewa kuona kama ina tija kwa Taifa letu au kama inaendana na wakati tulionao hivyo, iweze kuipitia na kuona kwamba, ni kwa jinsi gani inaiondoa na kuweka ile misamaha ambayo itakuwa na tija kwa Taifa na itaendana na wakati tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba kuongelea suala la kulinda viwanda vyetu. Ninaishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo imekuwa imara katika kulinda viwanda vyetu, hasa tukiangalia hata kwenye hizi taarifa ambazo tuko nazo. Imeonesha wazi kwamba, inaenda kufanyia mabadiliko Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Kutoka Nje, Sura Na. 276 na kuanzisha Tozo ya Maendeleo ya Viwanda *(Industrial Development Levy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kupongezwa sana, lakini pia, Waswahili wanasema; "ukibebwa bebeka." Viwanda vyetu vya ndani iko haja ya kuona ni kwa jinsi gani bidhaa ambazo inazitengeneza zinakuwa shindani. Kwa maana ya kwamba, ziweze kuwa shindani ndani ya Taifa letu, lakini pia, na nje ya Taifa letu.

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba kutolea mfano mdogo wa kiwanda cha vitenge. Kiwanda hiki kinatengeneza vitenge ambavyo vinauzwa kwa bei ndogo, lakini pamoja na hilo, wanawake wa Kitanzania na Watanzania kwa nini wanashawishika kununua vitenge vya shilingi 30,000, vitenge vya shilingi 100,000, mpaka shilingi 300,000? Ni kwa sababu ya ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninasema ukibebwa bebeka. Viwanda vyetu vione ni kwa jinsi gani bidhaa ambazo vinazitengeneza zinakuwa shindani. Pale ambapo bidhaa zinakuwa shindani ama zinakuwa na ubora unaotakiwa ni faida ya Watanzania. Kwa mfano, unakuta kwamba, labda kiwanda kama kilianzishwa Pwani, kutokana na ubora wa bidhaa zake, kiwanda hiki kinaanza kujitanua, kinaanza kuwa na *branches*. Kupitia zile *branches* ama matawi unakuta kwamba, ajira zinaendelea kuongezeka kwa vijana wetu na hivyo pato letu pia linaendelea kuongezeka. Kwa hiyo, mimi nadhani, iko haja ya Serikali kuona viwanda ni watoto wetu na kuendelea kuvifuatilia. Kadiri ambavyo tunafuatilia tunatengeneza uchumi wetu, lakini pia, tunaongeza Pato la Taifa na tunatengeneza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba kuongelea suala zima la kuongeza wigo wa makusanyo. Ninaipongeza sana Serikali wigo wa makusanyo haya kadiri ambavyo miezi inaongezeka na miaka inaongezeka tunaona kwamba, yanaongezeka, lakini bado hatujafikia, yaani vile vyanzo vya mapato tulivyonavyo bado hatujavikusanya ipasavyo. Kama tungekuwa tumekusanya ipasavyo, yamkini tungepunguza hii kuumiza kichwa kwamba, tunapata wapi hiki? Tunapata wapi hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naiomba Serikali iweze kuona ni jinsi gani inarasimisha sekta isiyo rasmi. Pia iweze kuona ni kwa jinsi gani mifumo tuliyonayo na taasisi zote zinajiunga na hii mifumo, lakini pia mifumo hii iweze kusomana kwa sababu, ipo lakini haisomani, hivyo inasababisha kuvuja kwa mapato yetu, ninaomba sana Serikali iweze kuliona hili. Mifumo yetu isomane na taasisi zote ziunganishwe kwenye hii mifumo, ili tuweze kupata mapato ambayo yanastahili ama tuweze kukusanya kulingana na vyanzo tulivyonavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Serikali inaweza ikalifanya, limekwishazungumzwa, lakini na mimi naomba kuwekea mkazo. Kwa jinsi ambavyo tunazunguka kwenye nchi za wenzetu ni jambo ambalo linawezekana, kutumia kadi kwenye malipo yetu, linawezekana kabisa. Tuliweza Kwenda nchi jirani tu hapa, tunashukuru Bunge, kama kamati tulienda pale, tuliona ni kwa jinsi gani ambavyo makusanyo yanakusanywa kupitia kadi ama kupitia, tunaita *electronic payment*. Sasa kwa nchi yetu tunaona kabisa kwamba, tukiwa kama Watanzania yamkini tunaweza tukaona kwamba, ni jambo gumu, lakini hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kiasi kilekile ambacho ungetoa fedha taslimu, ndiyo hichohicho unakilipia kupitia kadi yako kwa hiyo, ni kitu ambacho kinawezekana kabisa. Naiomba Serikali iweze kuona ni kwa jinsi gani tunaelekea huko kwa sababu mbuyu nao ulianza kama mchicha, tusisubiri mpaka hiki na kile, lakini tunaweza tukaanza taratibu. Kwa mfano tunaweza tukaweka *amount* kwamba, labda kiwango kinachozidi kiasi fulani kilipiwe kwa kadi, ama kiwango kinachopungua kiasi fulani ndiyo kilipwe kwa fedha taslimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, unaweza ukahitimisha. Muda wako umeisha.

**MHE. STELLA A. IKUPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninaomba kuhitimisha kwa kusema kwamba, wakati sasa tunasubiri kuelekea huko kwenye huu ushauri ambao nimeutoa kuna zile namba ambazo zimetolewa, ambazo zipo, zile za *TRA* ambazo zinakuwa zinatumika labda kama kuna shida unaweza

ukaripoti. Naomba namba hizi ziingizwe kwenye mifumo, kama kwenye meseji labda kwamba, tuwe tunatumiwa mara kwa mara. Kwa sababu, unakuta mtu unakumbana na tatizo kwamba, haujapewa risiti, unadai risiti, huna mahali pa kuripoti na hujui unaripoti kwa namna gani. Kwa hiyo, mimi naomba hii namba iwe inazunguka kwenye *messages* zetu za kila siku, ili kila mwananchi aweze kufahamu kwamba, nisipopewa risiti, naripoti wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naishukuru Serikali kwa hatua kali ambazo inazichukua za kuweza kukabiliana na mauaji ya watu wenye ualbino ambayo yametokea hapa nchini. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stella Alex Ikupa. Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, atafuata Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Jumanne Kishimba ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, binafsi nakushukuru sana kwa jinsi unavyotuongoza, lakini mimi binafsi namshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kibali cha pekee ambacho ametuwezesha kuendelea kuwepo hapa na kuendelea kujadili Bajeti ya Serikali. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Daktari, mtu bingwa kabisa, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, pamoja na Profesa, kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya lakini pia kwa bajeti yenu nzuri sana iliyojaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo amewafanyia wananchi wa Jimbo la Ushetu, kwa miradi mikubwa aliyoileta kwa wananchi wa Ushetu. Nasema tu kwamba, kwa kweli, Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Rais, Wananchi wa Jimbo la Ushetu, juzi tu wakati tuko pale tunazindua na kusaini mkataba wa shilingi 44,000,000,000 wa Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu alikuwa mgeni rasmi pale, aliwashuhudia wananchi wanavyomshangilia Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambazo amezifanya. Ni tukio la historia kubwa sana kwa Wananchi wa

Ushetu kwa sababu ni miaka mingi sasa walikuwa wanalia na hicho ndicho kilikuwa kilio chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Bashungwa kwa kweli, amefanya kazi kubwa kwa wananchi wa Ushetu. Barabara nyingi ambazo zilikuwa zimeshindikana toka uhuru, Barabara ya Uyogo – Ulowa ambayo ina kilometa 30 ilikuwa imeshindikana, lakini leo wananchi pale wanapita wanamshangilia tu Mheshimiwa Rais. Ni kazi kubwa Mheshimiwa Bashungwa umeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, tuna Daraja la Ilangashiga ambalo mkandarasi yuko kazini nalo lilishindikana. Tuna Daraja la Ubagwe ambalo nalo lilishindikiana, lakini lina mkandarasi. Pia, tuna Daraja la *Igombe River*, nalo lilishindikana, lakini Mheshimiwa Bashungwa mifupa iliyoshindikana amekuja kuitafuna. Hongera sana, Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo inaifanya. Kwa kweli, ni kazi kubwa sana Mheshimiwa Rais anafanya. Hapa najikita kwenye mada zangu, mwaka 2021, Sheria ya *Withholding Tax* ililetwa hapa Bungeni ambapo wakulima walilazimika wakatwe asilimia mbili, lakini kabla ya utekelezaji Sheria ikapita Bungeni na bahati nzuri Mheshimiwa Rais akaisaini, lakini utekelezaji wake ulikuwa mgumu sana kwa wakulima, kelele zilikuwa kubwa sana. Tuliirudisha tena hapahapa Bungeni mwaka 2022, tukaijadili tukaiondoa kwa sababu, utekelezaji wake ni mgumu, lakini leo hii tena wakulima hawa tumewaletea suala la kodi asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa bado ni masikini sana. Wakulima hawa ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, mkulima huyu mdogo, ambaye anateseka na jembe la mkono kuanzia mwezi wa nane, mwezi wa tisa, mwezi wa 10, mwezi wa 11, mwezi wa 12, mwezi wa kwanza, mwezi wa pili mpaka mwezi wa sita mwaka unaofuata ndiyo anaanza kupokea pato lake ambapo mkulima mkubwa sana anaweza akawa na kipato cha shilingi milioni mbili, milioni tatu au milioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunampelekea tena makato ya asilimia mbili ambayo tuliyajadili sisi wenyewe humuhumu Mwaka 2021, Sheria ikatushinda tukaiondoa, tukairudisha mwaka 2022, leo tena tunaenda kuwakata hawa wakulima. Mimi naendelea kumuomba sana Mheshimiwa Waziri, hii kodi aiondoe kwa wakulima. Mazao yetu haya yote ya pamba, tumbaku, korosho, kahawa na mazao mengine, yote yamepitia katika wakati mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji ulipungua mwaka 2018, 2019, 2021, katika mazao haya, yote yalipitia katika mtikisiko mkubwa. Mheshimiwa Rais ameingia madarakani, kwa miaka mitatu ya Mheshimiwa Dtk. Samia Suluhu Hassan, sasa mazao yameenda kutengemaa. Kutengemaa kwa mazao haya, tunaenda kuyaingizia kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda tena kuwavuruga wakulima wetu. Hatuwezi kuwapelekea kodi wakulima hawa wanaoteseka na jembe la mkono, hatuwezi kuwapelekea asilimia mbili wakulima hawa wanaohangaika shambani kwa kipato kidogo kwa miezi 12. Hatuwezi kuwapelekea kodi hawa wakulima ambao ni wachache, wako chini huko wanateseka ambako hata gharama za uzalishaji hawazijui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunawapelekea kodi, tunaenda kutokuwatendea haki wakulima. Nikuombe mwaka 2019/2020 mfano tu kwenye zao la pamba hali ilikuwa ni ngumu sana, sasa leo ushindani umeongezeka, kabei kanachangamka, wanunuzi wanaendelea kuongeza bei, mkulima anaenda kufurahia tunanyanyuka tena kumwambia sasa atozwe asilimia mbili, hii bado haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa tumbaku hawa waliokuwa wameteseka na tozo nyingi 2018, 2019, 2020 uzalishaji ulitoka tani 200,000 mpaka ukaja tani 34,000 na Pato la Taifa lilipungua mpaka dola 148,000. Mheshimiwa Rais ameingia madarakani ameondoa baadhi ya kodi, amesamehe baadhi ya madeni, leo tena tunaibuka uzalishaji wa tumbaku umetoka tani 34,000. Leo kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

tumeenda tani 200,000. Pato la Taifa limetoka 148,000 limeenda kuwa dola 484,000 Pato la Taifa limeongezeka. Sasa tunaenda kuwanyang'anya hata kile kidogo ambacho wanakipata waweze kuendesha uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii naendelea kuisisitiza kwamba tukubaliane hii tuiondoe, tuiondoe kabisa kwa sababu tunaenda kuwaumiza wakulima wetu. Mimi niendelee kuwaomba Mheshimiwa Daktari na Profesa wako hapa sifa kubwa ya mtaalamu ni kutengeneza uchumi na kodi ambayo ni rafiki kwa wananchi wetu siyo kuwa na maumivu kwa wananchi. Ng'ombe lazima umchunge, umnenepeshe, umpe dawa, siyo kabla haujamlisha unaanza kumkamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukuomba suala hili tuweze kuliondoa kwa sababu leo utakapo mwekea kodi mkulima, mnunuzi anachokifanya ni kupunguza bei kwa mkulima. Wakulima hawa hawa ni wachangiaji wazuri mbona kwenye mapato? Leo hii asilimia tatu ya halmashauri si inaenda kwa mkulima? Mnunuzi unapomwekea tu yeye ataenda kupunguza bei kwa mkulima wala hahangaiki na kitu kingine. Kwa hiyo, niendelee kukuomba hili suala bado ni changamoto sana kwa wakulima wetu, tunaomba suala hili hata kwenye bajeti ya fedha tumelijadili sana kwamba vyama vya msingi navyo viwe na mashine ya *EFD,* hatuwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa wanajiunga kwenye *AMCOS* ili waweze kupata soko, ni wale wakulima wadogo wadogo wanajadiliana wanajiunga kutengeneza chama chao cha msingi. Vyama vya msingi havina fedha, fedha hii ni ya wakulima hawa waliojiunga na inapoingia kwenye akaunti, ukiingia kwenye *schedule* unaweza ukaona ni bilioni mbili ziko kwenye *AMCOS A,* kumbe fedha hizi zinaenda kwa wakulima wadogo wadogo wote chama kinaachwa bila hela yoyote, kinaachiwa ushuru tu kidogo kwa ajili ya kujiendesha. Sasa unaenda kuwakata asilimia mbili, halafu unabeba tena unawaambia chukueni mashine ya *EFD* kwenye *AMCOS* zao, wakulima watakachofanya ni kusambaratika na kuvikimbia vyama, tunaenda kuua ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukuomba kupitia Bunge lako Tukufu, tuondoeni kodi kwa wakulima, waende kulima watengeneze fedha. Hakuna mkulima ambaye anazalisha zaidi ya shilingi 10,000,000 kwa mwaka, hayupo ni wakulima wachache mno hata tukifanya sensa hapa. Mimi nina *declare interest* mimi ni sehemu ya wakulima wale wadogo ambao wanateseka kule shambani. Tuondolee kodi wakulima kwa sababu tunapowaondolea kodi wanaenda kuzalisha, wanapozalisha kwa wingi ni Pato kwa Taifa, wanapozalisha kwa wingi ni utulivu kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa pamba tu, ni Mikoa zaidi ya kumi na mbili inalima pamba, ni zaidi wilaya 29 zinalima pamba ni wakulima wangapi wako kule vijijini ambao wanasubiria kwamba je, tunaenda kuwekewa kodi asilimia mbili? Waheshimiwa Wabunge kelele yake tunapoenda tutaenda kui-*solve* kwa wananchi wetu? Mimi niendelee kwa usikivu huu Mheshimiwa Waziri, tuondoleeni hii kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimeiongelea kwa uchungu sana, kwa sababu kelele tunazozipata kule kwa wakulima wetu ni kubwa sana, leo wakulima wa tumbaku bei ilishuka kuwa dola 1.5 kwa kilo. Kipindi cha Mheshimiwa Rais na tunavyoongea leo wastani wa bei na soko linavyoenda ni dola 2.5 ni Mheshimiwa Rais ametengeneza soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendelee kuomba tulindeni wakulima wetu wanaojenga uchumi wetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uhitimishe…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** …tunao watetea zaidi ya 70% ni wakulima wetu wa Tanzania na Mheshimiwa Rais amewatengenezea soko linazidi kupanda kila wiki, kila mwaka linaenda kuongeza, uzalishaji umepanda sana. Kwa huu utulivu ulipo kwa wakulima wetu ni mkubwa sana, tuendelee kuulinda, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani, ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatia Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Almas Maige ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha jioni hii ya leo. Napenda kuipongeza Serikali, Mheshimiwa Rais na Wasaidizi wake wote kwa bajeti hii nzuri na mipango mikakati ya maendeleo ya nchi yetu. Nawapongeza Mawaziri wote wawili Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango na Manaibu wao pamoja na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwanza kwenye mpango; kwenye mpango kuna mipango mikakati ya kuhakikisha kilimo kina tija kwa maana ya mikakati ya kwamba tija katika kupata mbegu bora, kupata uwekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji, kuongeza maafisa ugani na mambo mengine, naipongeza kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Kilimo kwa maana ya kwenda kuhakikisha sasa kilimo kweli kinaleta tija kwa wananchi, wakulima na Taifa. Hapo hapo napenda kushauri, kuna mpango mkakati wa kuongeza viwanda vya mbolea nchini, nashauri viwanda vya mbolea viendelee kuongezeka kwa maana ya viwanda vikubwa, vya kati na vidogo na kwa maana ya kwamba tuweke pia mkakati kwenye mbolea zetu za asili ambazo hazitumii kemikali yoyote kwa maana ya kupata vyakula ambavyo vinahitajika duniani. Kwa sababu vyakula hivyo vina soko zaidi (hayo mazao ambayo hayatumii kemikali) na pia wananchi wa humu ndani sasa hivi hayo mazao wanayatafuta kwa sababu ya kulinda afya zao. Kilimo kile kiendelee, lakini na kilimo hiki kingine kiendelee kikiwemo kilimo hai na kilimo hifadhi. Tutenge kabisa bajeti ya kuendeleza kilimo hai na kilimo hifadhi kwa faida yetu yetu, wananchi na ardhi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye kilimo twende tuongeze uzalishaji wa humu ndani kwa viuatilifu vya mazao mbalimbali kuepusha wananchi wetu na wakulima wetu kuletewa

viuatilifu feki au ambavyo havina ubora au vimezidi viwango ambavyo vinahatarisha maisha ya mwananchi katika hayo mazao yanayozalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijielekeze sasa hivi kwenye sekta ya uvuvi. Naipongeza Serikali kuingia kwenye uvuvi wa bahari kuu, tunajenga gati yetu kule Kilwa ya bandari ya uvuvi lakini Serikali iendelee na ule mchakato wa kununua meli za uvuvi pamoja na kuhakikishika Shirika la *TAFICO* linaanza kazi, kwa sababu hili Shirika litakapopewa fedha za kutosha tukakamilisha miundombinu yote likaanza kazi pale pesa zipo, pesa zipo sana kwenye uvuvi. Shirika hili lisipewe pesa kwa awamu awamu, tutafute fedha za kutosha tuachane na hili Shirika liendelee kufanya kazi tupate mapato tuwekeze kwenye miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya mifugo napenda kuvipongeza viwanda vya ndani na hasa kiwanda kilichoanzisha utengenezaji wa maziwa ya unga. Hapa tutaokoa fedha nyingi za kigeni kuagiza maziwa ya unga. Kumbe maziwa ya unga ni uwekezaji mkubwa, imetumika karibu shilingi bilioni 22 kwenye kuweka mitambo tu ya uzalishaji wa maziwa ya unga. Tukilinde kiwanda hiki na tuhamasishe na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie hizi kodi mbalimbali ambazo zitakuja kurejesha nyuma uwekezaji huu. Nawashauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Uwekezaji mwende kule kwenye kiwanda msipite nje mkaone ndani hali ilivyo mtashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maziwa tumesamehewa yaani wafugaji wamesamehewa mambo mengi yanayohusu mifugo na maziwa. Tunaishukuru Serikali kwa kuondosha baadhi ya tozo na baadhi ya kodi. Hata hivyo naishauri Serikali kwenye hii sekta ya maziwa basi yasamehewe maziwa yote kwa maana ya maziwa ya unga na *cheese*, kwa sababu maziwa ya unga siyo anasa tunataka kuepukana na lishe duni na utapia mlo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, tukiweza kutoa kodi kule, maziwa ya unga yatanunuliwa kwa wingi kwa sababu kuna

baadhi ya wananchi wetu hawana hayo majokofu ya kuhifadhia haya maziwa ya kawaida kwa hivyo watakaponunua maziwa ya unga atajenga afya yake na watoto wake lakini ikiwa bei iko juu yatashindikana kununuliwa. Nashauri iangaliwe sana hapo kwenye kodi hizo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nataka nijielekeze kwenye mpango, nimeona ukurasa wa 59 kuna kipengele kinasema tutaimarisha, kukuza na kubidhaisha Kiswahili Kitaifa, kikanda na kimataifa. Mwenyezi Mungu katupa neema, sasa hivi wenzetu wanahangaika kuhakikisha hili soko wanalikamata, sasa sisi Tanzania wenye hii mali tutakuja kunyang'anywa na kwa sabbu kuna nchi wenzetu tayari sasa hivi wanafunzi wao wamewalazimisha lazima wawe na *dictionary* ya Kiswahili na lugha yao nyingine kama Kifaransa au Kingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye hii mipango tuseme sasa ndani ya mwaka mmoja tutawawezesha na kuwaandaa wakalimani wangapi? kama ni mia tatu kama ni mia mbili. Tuna mpango gani wa kuongeza walimu wa Kiswahili kama ni mia nane kama ni mia tisa, tuwe na takwimu kwa sababu tusipokuwa na uhakika wa kuwekeza kwenye hili soko, soko hili tutanyang'anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu kuna nchi moja ya mbali ya Asia tayari wao wamejitangaza wana walimu wa Kiswahili na tayari wameshapata soko na wanasomesha huko duniani. Sisi tumekaa Kiswahili cha kwetu, Kiswahili cha kwetu. Wanachapisha vitabu, wanachapisha *dictionary*, wakienda kuchapisha nchi jirani ikawepo ile ilama wanaona ndiyo kule Kiswahili.kilikotoka *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe tunawekeza mitambo ya kutosha hapa nchini tuchapishe machapisho yetu, *dictionaries* zetu na vitabu vyetu hapa ndani ya nchi ili kutangaza jina letu kama hii ni mali ya Tanzania. Pia tutafute, hivi Kiswahili ni hatimiliki ni ya nchi gani? Kwa sababu tusipojua hatimiliki ni ya nchi gani tutakuja kunyang'anywa. Nimeshasema hili tayari watu wameanza kusema Kiswahili ni cha nchi fulani kwa sababu

anaona yale machapisho, wanaona vile vitabu, wanaona vimechapishwa nchi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupambanie, hii ni rasilimali, hizi ni ajira. Ndani ya Tanzania tunafanya mikutano yetu ya kimataifa lakini ukiweka kusikiliza mkalimani anatoka nchi jirani. Ile lafudhi na yale matamshi ni ya nchi jirani. Kweli tumeshindwa hapa kukidhi vigezo vya kuwa na wakalimani wa kutosheleza ndani ya mikutano yetu hata ya ndani ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo sisi tunaliona ni jepesi lakini wenzetu wanalichukulia kwa uzito mkubwa na wanakuja Tanzania sasa hivi kwa wingi kuja kuona utamaduni wa Mswahili na hiyo Lugha ya Kiswahili. Tusiipoteze hii fursa, ukalimani ni muhimu duniani, ualimu ni muhimu duniani. Tutengeneze mazingira ya vijana wetu na kwanza, mfano vijana wetu wenye ulemavu hii ni nafasi nzuri kwao kwa ajira kwa sababu haitumii nguvu kubwa ni kuwaelemisha tukawaongezea uwezo wa lugha mbalimbali na tukawapa mafunzo ya ukalimani, watafanya hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo msisitizo wangu kwenye lugha ya Taifa ya Kiswahili. Tuipigie debe lakini kwa kuiwekea mikakati maalumu na mizito ili kuhakikisha lugha hii na utajiri huu hatuporwi na mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namalizia kwa kuipongeza Serikali kwa kuiweka nchi yetu kuwa salama na yenye utulivu amani ya nchi inaendelea nawapongeza viongozi wote kwa kazi kubwa wanayoifanya kutuletea wananchi maendeleo. Nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, ahsante sana, nakusukuru sana. Mheshimiwa Jumanne Kishimba atafuatia Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar ajindae, karibu.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye huu Mpango

wa Bajeti ya mwaka 2024/2025. Kwanza nimpongeze Waziri wa Fedha na Timu yake, Waziri wa Mipango na wasaidizi wake kwa bajeti hii ambayo nafikiri tunakwendanayo vizuri. Kikubwa zaidi nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutuongoza wakati huu wa matatizo makubwa ya uchumi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye hoja. Mimi Jimbo langu au Mji wangu wa Kahama ndiyo umeongoza Tanzania kwa Mapato lakini pia ndiyo unaongoza kwa barabara mbovu. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango hebu nipangie vizuri kama unaweza kunipa mkoa wa kibarabara utakuwa umenisaidia sana. Kwa sababu wewe unakusanya pesa nyingi unafurahia unanipa zawadi ya ushindi wa mapato lakini unanichonganisha na wananchi wangu, kwa sababu wewe umekusanya pesa kwa njia ya mtandao hupiti barabarani kwa sababu mtandao haupiti barabarani, mtandao unaruka juu, ungekuwa unapita barabarani na wewe ungeona lakini sasa hivi mtandao haupiti barabarani. Naomba, naomba sana sana unisaidie sana kwenye suala la barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu vya Mungu, Biblia, *Quran* hata mila za wenyeji ni vitabu vimetengenezwa ili binadamu waishi na vimetengenezwa kwa kuzingatia vitu vingi sana, lakini sisi hapa tunaleta sheria ya kumwadhibu mtu ambaye hakutenda kosa kulipa faini ya shilingi milioni 15 au kwenda gerezani au vyote viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayekaa kwenye biashara siyo tajiri anayekaa kwenye biashara ni mfanyakazi. Sasa mfanyakazi hakutoa risiti unasema utamfunga tajiri, si matajiri wote utawamalizia gerezani? Lakini huyu mnunuzi anachukuaje mali ambayo haina risiti, kwa nini na yeye asikamatwe? Kwa sababu mali haina risiti, wewe umetoa hela hukupewa risiti unatokaje dukani? Maana yake ukikutwa na ile mali basi ni mali ya wizi, kama mali haina risiti ni mali ya wizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo matajiri wana-*branch* ngapi Tanzania? Haya kina Azam, kina Bakheresa kina nani wote

mtawamalizia gerezani, kwa sababu analewa na gari yake iko Ngara nyingine iko Tabora, mfanyakazi hakurudi maana yake shilingi milioni 15 itamu-*encourage* kila mtu kwenda kumshambulia huyu tajiri. Sasa mimi naweza kuwa gerezani kwa kosa hili, shughuli zangu za biashara zinaendelea kwa hiyo mashtaka yatakuwa yananifuata gerezani. Nitakuwa naongezewa tu miaka tu kule kule gerezani, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake Serikali ni kama mchungaji wa mifugo, haiwezekani mchunga mifugo akawa na hasira dhidi ya mifugo yake. Mwananchi ni kama mifugo ya Serikali, sasa mfugaji gani huwa ana hasira? Mchungaji hanaga hasira. Huwezi ukawa na hasira ukifikia kiasi cha kusema kwamba mimi sasa nataka niwauwe hawa ng'ombe sasa utachunga nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya biashara, ndiyo maana wewe unasema hakuna mapato ni kweli hakuna pesa. Leo maduka yote yamejaa plastiki, wachina wamechukua zile hela zimeishaenda. Nyumbani wote humu ndani Waheshimiwa Wabunge ukipata shida unaweza kuuza nini ndani? Wote tunamiliki plastiki hatumiliki chochote, hela zimeenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya bei ya mahindi leo shilingi 30,000 utauza gunia ngapi ili wewe Serikali upate hela? Kwa hiyo, hali ya biashara ni ngumu, fikiria sana hili suala. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu wewe mwenyewe una timu ya mpira je, mtu akichenga pale bila kutoa tiketi kwenye mpira ukamatwe wewe? Maana yake huyu ni mwizi kakuchenga wewe, haiwezekani. Mheshimiwa Bashe ana bucha, ana mabucha mawili, bucha yake sasa hivi Dar es Salaam mtu katoka kuchukua nyama bila risiti, kweli utakuja umkamate Mheshimiwa Bashe humu Bungeni... *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Na Nzega.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, itawezekani kweli? Na Nzega anayo. Sasa itawezekana kweli? Lazima tufikirie kwamba huyu anayechukua ile nyama bila risiti

ndiyo mwenye kosa. Huyu tajiri anashirikije kwenye huo wizi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuliangalie kwa mapana sana. Kila siku mimi nasema humu matajiri wachache mno ndio wazima, wengi wanashinda na vidonge wanameza vidonge kutwa nzima kwa matatizo makubwa mno. Alikuwepo hapo Meneja wa CRDB, mngemuuliza aeleze *statement* ya matatizo waliyonayo wafanyabiasha wa mikopo ni makubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niliseme kwa sababu umesema naongoza lakini simu ninazopata kule kwa wafanyabiashara wangu kwamba tumeongoza mapato. Halafu tarehe moja mnaanza tukukamata kwa risiti maana yake watu hawa watafanyiwa uhuni na *collaboration* itakuwa kubwa mno ya utapeli. Hali ya utapeli ni mbaya sana sasa hivi, itakuwa ni tatizo…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa faini ya trafiki…

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, faini ya trafiki ni shilingi 30,000 watu hawalipi, wanampa trafiki shilingi 3,000 wanaendelea hawalipi. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha lifikirie sana kwa mapana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya, mara mara najaribu kuliongelea sana, najua nikiwambia dawa hautakubali kuwapa wananchi bure lakini tuna sheria nyingi sana za kikoloni kwenye suala la afya. Leo tuna madaktari zaidi ya 7,000, 8,000 waliomaliza hawana ajira. Waliostaafu wapo zaidi ya 7,000, 8,000 *medical assistant* wapo, wafamasia wapo kwa nini watu hawa wasipatiwe na wao leseni kama za mganga wa kienyeji kwa shilingi 30,000 kufanya shughuli zao? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanye shughuli zao, wengine wamebakiza miaka nane kustaafu na kazi hawajapata na ninyi mnawadai je, mtawadai wakiwa wamestaafu? Waruhusuni

watibu watu. Hali ya hospitali Waheshimiwa Wabunge tunaifahamu ilivyo, tuna zahanati zetu zinatibu watu mpaka sasa tano asubuhi, kuanzia ile asubuhi mpaka jioni si ziko tupu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, daktari aweke bango pale kwamba mimi natibu kwa bei hii, ukija hata na mbuzi nitapokea au kama huna hela ukipona utakuja ufanye kibarua kwangu, tatizo litakuwa nini? Wananchi watasubiri huyu saa tano, wataacha hii ya kwenu, bwana ninyi malizeni ya kwenu ya Serikali mimi nasubiri ya huyu ili nikipona nitaenda kufanya kibarua. Kwani mimi nikifanya kibarua kwa matibabu kuna kosa gani? Kwa vile Serikali hatoi dawa bure, waruhusu hawa madaktari maana yake wewe ndiye uliyewapa digrii waje pale hospitali, waweke mabango kwamba, mimi natibu kwa gharama hii nafanya hivi, wafanyie kwenye zahanati zetu tumezijenga wenyewe, lakini baada ya saa nne au tano hazina watu ule muda wote. Wafanyie hapo kama wanaweza kutulipa sisi vijijini, si ndiyo tulijenga sisi, watulipe hiyo hela kama ni kodi ili kupunguza msongamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuliongea kwa mapana sana, maeneo ya kwetu yale ambayo yana watu wengi watu, hali yao ya umaskini ni mbaya sana. Hatu-*control* bei ya dawa na matibabu, watafanya nini hawa watu? Ondoeni sheria hizi mbaya za kikoloni. Tuna dawa nyingi sana zipo Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *chloroquine* nitatoa mfano, Kenya na Uganda wanatumia *chloroquine* lakini Tanzania imekataliwa, sasa mimi najiuliza ina maana wale mbu wa Uganda walijua hapa ni Mtukura waka-*stop* hapo wakakataa kuja huku? Walijuaje kwamba hapa ni Uganda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini basi wasingekuja *chloroquine* ikafanya kazi ikafika mpaka Nzega au Kahama ndiyo tukasema sasa imekataa, kweli inawezekana? Wote tunaamini kabisa chakula salama duniani ni cha *buffet* kwa sababu watu wote mnaona. Sasa kama wanatumia wakenya na waganda wewe unakataaje *chloroquine* isifanye kazi? Kwenye *corona* imetujsaidia, jaribuni kufikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tunatoka hapa kwenda India kutibiwa, je, huwa tunaenda na dawa zetu? si tunatumia dawa za India? Kuna ubaya gani tukanunua dawa za bei rahisi kutoka India hawa maskini wakatumia, matajiri wakatumia za bei ghali, nilitaka tu kuliongelea hilo kwa mapana sana ili kuwapunguzia maisha ni magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini lifikirie kwa makini sana suala la milioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Kishimba kwa mchango wako, tunakushukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Almas Maige, atafuatia Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar na Mchangiaji wetu wa mwisho leo atakuwa Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kuniruhusu na mimi nichangie bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2024/2025. Nianze kwanza kuwapogeza Ndugu yangu Mwigulu na Naibu Waziri wake, pia Profesa Mkumbo na Naibu Waziri wake, wamefanya kazi nzuri sana kuandaa bajeti hii. Matokeo yake bajeti hii imelenga katika kuendeleza miradi ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tuna mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo ndiyo uti wa mgongo wa umeme wa *REA* Vijijini, kama bwawa hili halijakamilika basi umeme vijijini itakuwa hadithi, hautawaka, utakuwa unawaka na kukatika. Vilevile, bajeti hii imelenga kumalizia mradi wa *SGR Lot 3, 4* na 5. Reli hii ikikamilka itafanya kazi ya kuongeza mapato na tuna mapango wa kupeleka mpaka Musongati kule Burundi ambako ingebeba mizigo mikubwa na kuingiza hela kwenye Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato cha Kimataifa ili ndege za kimataifa ziweze kutua hapa na Serikali ipate fedha. Pia ujenzi wa barabara na madaraja makubwa hasa lile la Kigongo – Busisi litasisimua uchumi katika maeneo hayo ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeongeza bajeti kwenye bajeti hii. Tumeongeza matumizi ya bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi milioni 710 mpaka shilingi milioni 825, hili si jambo dogo tuipongeze sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii ya bajeti Waziri Mwigulu ameeleza dhamira ya Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kukuza huduma za afya, maji, elimu na anaongelea nishati safi kwa akina mama hasa vijijini, jambo ambalo litaleta faida kubwa sana ya kiafya na nafuu kwa akina mama. Vilevile, kule kwangu Tabora tuna kazi mbili kubwa sana ya kukata miti, eneo la Mkoa wa Tabora tunakaribia kuwa jangwa kwa sababu tunalima sana tumbaku na hatuwezi kuacha kulima tumbaku, inaleta fedha Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakata miti kukaushia tumbaku na kwa ajili ya kupikia kuni na mkaa. Wazo hili la Mama Samia Suluhu Hassan la kuleta nishati safi ya kutumia gesi na nishati mbadala itaokoa miti ambayo itasaidia sana hapo baadaye ili wajukuu zetu waikute Tabora yenye miti badala ya jangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mizuri hii ya kuleta maendeleo na kukuza uchumi ina changamoto kwetu. Tumefurahia mambo mazuri lakini hela za mama katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini na maeneo mengine imezima zile changamoto kubwa zilizokuwepo. Naishauri Serikali ingezifanyia kazi changamoto hizi ambazo zipo, kwa mfano, uwekezaji mkubwa sana katika sekta ya elimu, madarasa na shule nyingi zimejengwa za sekondari na msingi, limetokea tatizo kubwa sana la upungufu wa nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyetu kwa mfano Wilaya ya Uyui na vijijini kote hatuna nyumba za kulala wageni za kukodisha, kila mtu na nyumba yake kwa hiyo walimu hawa, fikiria amechukuliwa amepangwa shuleni kijijini anapelekwa na gari la Halmashauri mpaka pale kijijini shuleni anateremshwa basi, mwalimu atalala wapi? Hali ni mbaya sana, watu hapa mjini walimu wanasema hawana nyumba lakini kuna nyumba za kupanga, kule kijijini hakuna nyumba ya kupanga hata moja. Walimu hawa wanalala nyumba moja iliyopo pale shuleni watu saba, nane, kumi na wana familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika Halmashauri yangu, mahitaji ya nyumba za shule za msingi za walimu ni 1,720 zipo 261 pungufu ni nyumba 1,459. Watoto wetu, wanafunzi wetu na walimu waliopangwa vijijini wanalala wapi? Sisi tumejengewa shule nyingi, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kuleta fedha za madarasa, shule mpya na kadhalika, walimu nyumba hakuna, kwa hiyo bajeti hii itibu suala la nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naliona napata taabu sana ninapoenda kutembea, mimi naenda vijijini sana. Ukiuliza mwalimu unakaa wapi anakuambia nyumba hii, mwalimu unakaa wapi, sina nyumba; unakaa wapi, nakaa na jirani. Hiki ni kitu kibaya sana naomba bajeti hii ifikirie sana suala la nyumba za walimu kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine la watoto wa mitaani. Serikali tumetunga sheria ya mimba za utotoni lakini tumelenga sehemu ya watoto wanaosoma shule. Hilo ni kundi moja. Wapo watoto wengi mimi nilikwenda Mwanza juzi hapa wanasema wamekusanya watoto wanawarudisha majumbani kwao, mimi naona uchungu sana. Badala ya kutatua tatizo watoto hawa wanapata mimba mitaani halafu wanaenda kuzaa wanarudi mitaani. Watoto wa shule wanapata mimba shuleni halafu wanarudi shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina *data* gani za watoto waliopata mimba za utotoni wapo mitaani, nini kinafanyika? Tulikaa Bungeni hapa tukapitisha sheria kwamba watoto wa shule

wakipata mimba, kwanza aliyemtia mimba miaka 30 lakini akimbaka ni maisha. Akipata mimba ajifungue mtoto arudi shuleni, lakini watoto wa mitaani wanapata mimba wanarudi mitaani. Tunazo Wizara mbili, Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na Wizara ya Wanawake, Jinsia na Wenye Mahitaji Maalum. Wizara hizi zina sheria za kibaguzi kwa watoto wa mitaani, watoto wa mitaani nani baba yao anawatunza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona uchungu kwa watoto wa shule tu? Hawa watoto dawa siyo kuwakamata na kuwapeleka majumbani kwao, watarudi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana bajeti hii iongezwe kwenye Wizara hizi mbili zipewe majukumu ya kuwachukua watoto wa mitaani na kupata utatuzi wake, siyo kuwatia kwenye malori na kuwarudisha majumbani kwao walikotoka. Wajawazito, wagonjwa wanaumwa, hili ni tatizo kubwa sana kitaifa pia hii ni nguvu kazi kubwa, mimi naomba Serikali hii inisikie na Mheshimiwa Mwigulu jaribuni kusaidia watoto hawa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuheshimu na kumpongeza mchangiaji Mheshimiwa Mbunge anachangia vizuri, lakini nataka kuweka kumbukumbu sahihi kwamba Wizara ya Kazi, Vijana na Ajira na Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwamba zinabagua mtoto wa mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika sheria na sera zetu tulizonazo tunayo Sera ya Masuala ya Haki za Watoto na tunayo Sheria ya Mtoto tumetunga katika nchi hii. Sambamba na hilo pia

tuna Katiba ya nchi ambayo inazuia kuhusiana na masuala ya ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahsusi kwa uzito Serikali iliamua kuandaa na kuwa na Wizara maalumu zitakazoshughulika na masuala ya watoto, ikiwemo Wizara ya Afya na hii ya Maendeleo ya Jamii. Katika kufanya hivyo zipo taratibu na sheria mbalimbali zinazoongoza namna gani ya kushughulika na masuala ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata hao watoto wa mtaani, mitaa haina watoto kwanza nataka tu kuweka tu kumbukumbu vizuri. Kwa hiyo, watoto wanazaliwa, isipokuwa kuna masuala ya makuzi na malezi ambayo inakuwa ni wajibu wa msingi kwa mujibu wa sheria ya mtoto kwamba, wazazi na walezi tunao wajibu kuweza kuhakikisha kwamba tunashughulikia masuala hayo. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na Serikali tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali kwanza kuweka bajeti kwa ajili ya masuala ya watoto na kuangalia masuala ya ustawi wao, makuzi yao na malezi yao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali tumeendelea kutekeleza hayo tofauti na jinsi alivyosema Mheshimiwa, nataka kurekebisha hapo tu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante na kabla sijamuuliza Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Naibu Waziri unachotaka kusema ni kwamba Serikali ina *mechanism* ya ku-*capture* makundi yote ya watoto waliopo kwenye mifumo rasmi ya malezi na wale ambao hawapo kwenye mifumo rasmi ya malezi, ndicho unataka kusema?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Almas Maige unapokea taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Naibu Waziri amesema mengi lakini Serikali haina *data* ya watoto waliozaa watoto wenzao (mimba za utotoni) huko vijijini, mitaani na mijini. Watoto wakazaa watoto wenzao ila tunajua watoto wa shule waliozaa watoto wenzao tunajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti basi naomba niseme hilo suala la watoto la ubaguzi sheria ya ubaguzi nimelitoa, lakini naona kama sheria zilizopo haziwasaidii watoto ambao wamefurika katika mitaa yetu na wanalala huko na kupata mimba za utotoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi Naibu Waziri ametumia muda wangu mrefu, naomba sasa nishukuru kwamba Serikali…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas Maige nakuongezea dakika moja uhitimishe.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsnate sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nyingi alizozifanya katika Jimbo langu. Kwa miaka mitatu hii ametuletea karibu shilingi 55,600,000,000 na hii imetupatia Hospitali ya Wilaya, sekondari mbili, shule ya msingi na Kituo cha *VETA* na mengine mengi. Pia barabara tumetengeneza na elimu tunasoma kama vile ada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, mwaka huu Serikali katika bajeti yake imepanga kujenga shule yenye ahadi ya Marais watatu pale Benjamin Mkapa, Kijiji cha Migugumalo, nashukuru sana Serikali. Pia, lipo tatizo dogo sana kwenye Wizara ya Nishati umeme unakatika kila mara kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui, ambapo sasa kuna mabenki na vituo vya mafuta lakini wafanyakazi na watumishi hawafanyi kazi vizuri. Tatizo kubwa tuliambiwa ni urefu wa njia inayotoka Tabora mpaka

Chaya hapa Manyoni, ikitokea shoti yoyote huku mpaka Isikizye kule Makao Makuu ya Wilaya. Tulisema dawa ni kuunga *circuit breakers* ama kujenga kituo cha kupoozea umeme. Naomba bajeti hii ifikirie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniongezea muda. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige kwa mchango wako. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar na atatuhitimishia Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, lakini nikupongeze kwa namna ambavyo unaendelea kutuongoza na kumsaidia Mheshimiwa Spika tangu asubuhi unaendelea kuongoza vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, ambaye ametupatia uhai na uzima hadi sasa hivi tupo tunaendelea na majukumu yetu. Sambamba na hilo nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea kuifanya ya kulitumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mama yetu anaendelea kuwa msikivu sana. Amekuwa msikivu kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi mbalimbali. Bajeti hii ambayo tunaijadili hapa na mpango ambao tunaujadili leo ni matokeo ya maoni ya Wabunge waliochangia kwenye bajeti mbalimbali za kisekta, kwa kweli ni jambo la kumpongeza sana mama yetu amekuwa msikivu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kulikuwa na changamoto nyingi kuhusiana na wafanyakazi mbalimbali ambao walikuwa wanazungumzia suala la kikokotoo, mama amesikia kilio kile na sasa anakwenda kutatua changamoto ambayo ilikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama amekuwa muungwana sana, mama yetu amekuwa mwadilifu sana. Ni mzalendo sana kwa Taifa hili na ndiyo maana anaendelea kutuletea mipango mizuri na bajeti nzuri, leo hii endapo bajeti hii itapita tunaamini kwamba changamoto nyingi za watanzania zinaenda kutatuliwa kupitia bajeti hii ambayo tuna matumaini nayo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ni Rais ambaye ana misimamo isiyoyumba na isiyoyumbishwa, kutokana na misimamo hiyo ndiyo maana leo mradi wa *SGR* unandelea kwa kasi kubwa, ndiyo maana leo hii mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere umefikia zaidi ya 97%, ndiyo maana leo hii mradi mkubwa unaendelea kuwekezwa kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam na bandari mbalimbali, ndiyo maana kuna mabadiliko na mapinduzi makubwa sana ya sekta ya elimu, afya na miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba mama yetu analitendea haki Taifa hili sana na anawatendea haki watanzania, tuendelee kumuunga mkono, kumuombea kwa Mwenyezi Mungu Allah ampe afya na umri mrefu lakini busara na hekima ziendelee kumtawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebarikiwa sana Tanzania na rasilimali nyingi sana. Moja, miongoni mwa rasilimali ambazo tumebarikiwa nazo ni bahari. Bado mchango wa bahari kwa maana ya sekta ya uvuvi ni mdogo sana kwa Taifa letu. Bado hatujaweza kuwekeza kwenye bahari kasa kwenye uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni ya tatu kwa ya nne kumekuwa kuna mpango wa ununuzi wa meli nne kubwa ambazo zitakwenda kuvua kwenye bahari ya kina kirefu (Bahari Kuu), lakini mpango ule hadi leo bado haujatekelezeka. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali kwa sababu meli hizi nne zilikuwa zina mgao kwamba mbili zitanufaisha Zanzibar na mbili zinakuja hapa Tanzania Bara, lakini sisi kama Zanzibar tulikuwa tunazisubiri kwa hamu kubwa meli hizi kwa sababu kule tunakwenda na uchumi

wa bluu. Meli hizi zitakuja kutusaidia sana kuongeza Pato la Taifa letu pia litakuja kusaidia sana kwenye kutatua changamoto za ajira hasa kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasubiri sana na tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie mradi huu na mpango huu umefikia wapi? Kwa sababu mara nyingi tumekuwa tunaulizia lakini bado majawabu yanakuwa tunasubiria kwamba, mpango wanasema umekamilika lakini hadi leo hii bado jambo hili halijatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la manunuzi. Hizi fedha nyingi ambazo tunazipitisha ama tunazijadili leo, bajeti hii, asilimia kubwa inakwenda kwenye manunuzi. Suala la ku-*comply* na sheria mbalimbali za manunuzi ni jambo moja lakini jambo kubwa ambalo ninataka kulizungumzia ni suala zima la *value for money* kwenye manunuzi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatekeleza miradi mikubwa, ni kweli miradi ya miundombinu inajengwa lakini nisisitize na niiombe sana Serikali kwenda kusimamia manunuzi haya yazingatie zaidi *value for money* na kuweza kuokoa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo lazima tuweke mifumo ya uwajibikaji ambayo iko wazi ili kuona kwamba manunuzi haya yanafanyika kwa utaratibu mzuri na yanazingatia thamani halisi ya fedha ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimalizie kwa kusema kwamba, kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi imehimiza suala la ushirikiano wa Serikali zetu mbili, hasa zile Wizara ambazo si za Muungano. Ninaipongeza sana Serikali ya Awamu hii ya Sita, imeendelea kushirikiana sana na Serikali ya Awamu ya Nane ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, hasa Wizara zile ambazo si za Muungano lakini bado kuna taasisi ambazo ushirikiano wao haujawa imara, hususan kwenye maeneo ambayo Tanzania inawakilishwa kwenye mambo mbalimbali ambayo yako nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali isiishie huku juu kwa Mawaziri kwenye ushirikiano, hadi taasisi zetu ambazo tunazisimamia wahimizane kwenye kushirikiana taasisi ambazo siyo za Muungano zilizoko huku Bara na kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na niiunge mkono hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar kwa mchango wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaomba mniruhusu nimkaribishe Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ambaye ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo, karibu.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa kitinda mimba katika siku ya leo, katika kuchangia bajeti hii ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa shukrani na kuwapongeza Mawaziri wa Mipango na Fedha, vijana hawa wa Singida wenye akili nyingi kwa jinsi ambavyo wanaifanya kazi kwa weledi mkubwa na kwa uaminifu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kushikilia pochi ya nchi lazima uwe mwaminifu na mtu ambaye unachapa kazi na ndiyo maana unatosha sana Mheshimiwa Waziri na tunakupongeza na tunakuamini Mkoa wa Singida jembe letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka nichangie kwenye barabara, ninajua barabara wameongea watu wengi sana lakini barabara za katikati ya nchi, Mkoa wa Singida na Dodoma ni barabara za kimkakati. Kwa sababu unapotaka kwenda popote kwenye nchi hii, kutoka Kaskazini kwenda Kusini, Kusini kwenda Magharibi, Mashariki, popote, lazima utapita katikati ya nchi. Kwa hiyo, tunaposema barabara hizi zitengenezwe kwa kiwango cha lami, maana yake zinatumika na nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akiwa pembeni kule anaweza akawa anamaliza mambo yake kule, lakini ukitaka kwenda Mwanza utakatiza Singida, ukitaka kutoka Mbeya uende Arusha utakatiza Singida. Sasa unatoka huku na lami unafika hapo katikati unaingia kwenye vumbi. Hata kama ulikuwa na gari yako ya maana umetoka nayo huku ukifika pale inaingia kwenye vumbi. Kwa hiyo, ninataka niwaombe Waziri wa Mipango na Fedha, wala msije mkadhani mtaonekana kwamba mmependelea Mkoa wa Singida. Hizo ni barabara ambazo nchi nzima wanazitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayotoka Iguguno ikaenda Simiyu, barabara kama hiyo inaleta pamba kutokea huko Mkoa wa Mara, inapita Singida inakwenda inapeleka Dar es Salaam, inatoa *materials* Dar es Salaam inapeleka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata barabara ya katikati ya nchi, ya Mwanza mpaka Dar es Salaam imelemewa inaharibika kila wakati kwa sababu imekuwa *congested*. Magari yote yanafuata pale lakini hizi barabara tukishaziwekea lami ina maana mtawanyiko. Mtu anayekwenda Musoma hatahangaika kwenda Shinyanga akakatize mpaka Mwanza, akifika Singida anapita Simiyu anakwenda anamaliza. *(Makofi)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayetaka kwenda upande huu anapita, kuna barabara nyingi.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi barabara za katikati tunaomba ziwekwe lami. *(Makofi)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni barabara za kimkakati ambazo zinatumika na nchi nzima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Taarifa; samahani Mheshimiwa Isack. Taarifa Mheshimiwa Massay.

**TAARIFA**

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Francis Isack anachangia vizuri sana na kwa sababu ni jirani yangu, ninataka nimkumbushe na hii barabara inayotoka kwake pale kuja Mtinko na kwenda mpaka Hydom na hiyo ndiyo barabara inayoenda Simiyu na hata hii aikumbuke kwa sababu wapigakura wake na ndiyo barabara kubwa tunayoipitia, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Isack unaipokea Taarifa?

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea. Nimesema barabara za katikati ya nchi, hata Dodoma nimeitaja, ni barabara za kimkakati. Kwa sababu huwezi kuruka, yaani wewe kama unataka kwenda huko huruki hapa, lazima utapita kwenye vumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote, wote lazima mzitetee barabara za katikati ya nchi. Ni eneo liko *located strategically* yaani hapa sisi tuna bahati kuwa hapo kwa sababu lazima upite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Ujenzi anapotaka kwenda jimboni haruki, akitoka Dar es Salaam lazima apite kwenye vumbi hilo. Kwa hiyo, mimi ninataka tu niseme, hizi barabara za katikati ya nchi ambazo ziko chini ya *TANROADS*, zinatakiwa ziwekewe lami ili tuiunge nchi nzima kwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipendezi kuwa umevaa suti, chini unavaa kaptula yaani unatoka na barabara ya lami unafika hapo unakutana na vumbi. Halafu unaharibuharibu gari yako baadaye ndiyo unakuta lami tena mbele. Hii inatuharibia muunganiko wa kinchi. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Fedha toa fedha, Waziri wa Mipango weka

mipango ili hizi barabara za katikati nchi iweze kupitika yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihame hapo niende kwenye suala la maji. Katika nchi yoyote duniani ambayo itahesabika inawatunza watu wake vizuri ni ile inayowapa maji kwa sababu maji ni uhai, maji safi ni kila kitu. Hata kiwanda hakiendeshwi bila maji, gari huendeshi bila maji. Ikiwa tu haina maji injini ina-*knock*. Sasa, sembuse itakuwa watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Profesa, ulipokuwa Katibu Mkuu wa Wizara wa Maji pamoja na Waziri wako wa wakati huo, mlikuwa mna mpango mzuri sana wa kutoa maji Ziwa Victoria kuyaleta mpaka Dodoma. Sasa, leo umeingizwa jikoni kwenye mipango ya nchi, hiyo ilikuwa ni mipango yako ya Wizara ya Maji na Waziri wako, lakini sasa umeingizwa kwenye Wizara ambayo unapanga mipango ya nchi. Ninakuomba uufufue huu mpango ndugu yangu, utakuwa umetibu kidonda cha nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji kutoka Ziwa Victoria ni chanzo cha maisha ya milele. Sisi tutakufa tutakiacha. Maji, lile ziwa Mungu amelipa uwezo. Mto Nile unamwaga maji kwa wingi, kila siku tangu dunia iumbwe lakini lile ziwa halijawahi kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ule mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kuja Dodoma ulikuwa unapitia pale Sibiti unakuja mpaka Dodoma. Tena vizuri zaidi ule mradi kule kote utatumia pampu lakini ukishafika Mkoa wa Singida ukaingilia Sibiti, unakwenda Kijiji kinaitwa Kisana kiko pale jimbo la Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokea pale Kisana-Singida mpaka Dodoma maji yanakuja kwa *gravity*. Kwa hiyo, yatakuwa hayana tena hata gharama kubwa. Sasa mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Fedha, vijana wetu; hebu ufufue huo mpango halafu mpasie jirani yako hapo amwage fedha ili Watanzania wapone maji yafike Dodoma. Sasa wakati yanakuja Dodoma yatapita kwenye jimbo langu na mimi

nitaogelea maji, tena haya yatatumika hata kwenye umwagiliaji. Kwa hiyo, nikuombe sana hili suala la mpango wa maji usije ukaliacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nije kwenye suala la bomba la gesi, nilishawahi kuchangia hapa. Hili bomba liko Dar es Salaam, bomba hili tunalihitaji liende mpaka Mwanza, liende Arusha, liende Mbeya ili tutumie gesi hii kwenye nyumba zetu kama tunavyotumia maji. Mungu ametujalia kuwa na gesi. Tumeshaitoa chini tumeifikisha Dar es Salaam, sijaiona kwenye mpango, huu mradi wa bomba. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango pamoja na Fedha, hebu wekeni hii mipango na fedha zitoke bomba hili litembee nchi nzima. Kama tulivyoweka Mkongo wa Taifa, leo tunatesa na *internet* mpaka vijijini watu wanaangalia *internet*. Ni kwa sababu mkongo umesambaa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili bomba lisambae nchi nzima Tanzania ili tutumie hii gesi vizuri. Tena kuna wazo hili la kupeleka gesi kule Kenya, achaneni kabisa na hili wazo. Wale jamaa watachukua hii gesi wataanza kutuuzia *by-products* za gesi. Ile gesi *by-products* zake ni nyingi; chupa za plastiki, vizibo kwenye *containers* za maziwa na nini. Hebu hii gesi isambae hapa hapa nchini. Sisi bado tuna uwezo wa kuitumia hii gesi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana; hata hizi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mimi ningeomba kabisa hizi kodi za vifaa hivi vya kubadilisha magari ili yatumie gesi, hivi mngevifikiria kuvifutia kodi kabisa ili magari mengi yabadilishwe yaweze kutumia gesi. Hata hii tozo hii, hiki chanzo mngekiweka kama cha akiba. Yaani mngefanya uchochezi kwanza mfute kodi za hivi vifaa, magari mengi yabadilishwe kuwa ya gesi, mwakani hivi, ninajua bado utakuwa Waziri wa Fedha Mama anakupenda na unafanya kazi vizuri ili sasa uje utumie hiki chanzo kitakapokuwa kina magari mengi zaidi lakini kwa sasa utakiwahisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wataacha kubadilisha magari. Wataona mmh, kumbe huku nako tozo imeshaingia.

Acha tu sasa hivi, wewe acha hii tozo iweke akiba, futa kodi kwenye hivi vifaa ili vituo vya kujazia gesi viwe vingi.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa. Kama nchi tunahitaji sana kodi ndiyo maana rafiki yangu analalamika kwake hakuna maji na kwangu na mimi ninahitaji hiyo tozo nipate kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba, unajua ile bei ya gesi imeshuka sana? Kwa hiyo, kiwango kinachoongezeka hakiwezi kuathiri chochote. Kwa hiyo, tusiliweke kama jambo kubwa. Nchi inahitaji kodi na tunahitaji kufanya maendeleo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Isack, unapokea taarifa ya Mheshimiwa Kiswaga?

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa ya Mheshimiwa mimi siipokei kwa sababu, magari ya gesi bado ni machache sana. Tunataka magari mengi yabadilishwe, halafu hiki chanzo tuje tukitumie vizuri wakati magari mengi na kituo chenyewe cha kujaza gesi Dodoma bado hakuna. Bado kiko Dar, leo tunakimbilia kuweka tozo, magari mangapi hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiyo maana ninasema hivi, kodi zifutwe za vifaa vya kubadilisha ili magari mengi yabadilishwe halafu kituo kianzishwe hapa Dodoma na mikoa mingine, magari yawe mengi halafu hiki chanzo tutakitumbukiza tu. Sasa hivi haraka haraka watu wataacha kuagiza hata hayo magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimalizie harakaharaka tu kwa sababu mimi ni kitinda mimba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ninaomba uhitimishe, muda wako umeisha.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nihitimishe tu kwa kusema, Waheshimiwa Wabunge, ule Muswada wa kuja, ile *Finance Bill* kuhusu kupitisha suala la sukari, *NFRA* kununua ni jambo zuri sana na niliwahi kuchangia hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Mheshimiwa muda wako umeisha kabisa tafadhali.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba jambo hilo tulipitishe ili tuwasaidie wananchi wa Tanzania. Hili ndiyo zao lao la maskini ambalo kila maskini lazima anywe chai na uji wenye sukari. Kwa hiyo, niwaombe sana hili tulipitishe kwa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge ninawashukuru sana kwa uvumilivu wenu. Tumefikia mwisho wa shughuli zetu za leo. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumepata nafasi ya kuchangia kwa niaba ya Wabunge wengine lakini pia kwa niaba ya wananchi wetu.

Kipekee sana ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara zote mbili pamoja na Naibu Mawaziri pamoja na Mawaziri wengine ambao mmeweza kushirikiana nasi katika shughuli hii ya leo na Mawaziri kwa kupokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa umakini wa hali ya juu.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, ninawakumbusha kesho asubuhi ni Bonanza. Tupite kwenye *group* letu la Wabunge kufuatilia muda na mahali ambapo tutakutana na tumeshaona wenzetu toka maeneo mbalimbali wamekuja. Kwa hiyo, tunawatarajia Waheshimiwa Wabunge wote tutashiriki vizuri. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo ninaahirisha Kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 24 Juni, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.53 Usiku Bunge Liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 24 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*